ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/NaibWaziri Kiongozi/ Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

46.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
64.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
65Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

66.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
67.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
68. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
69.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
70.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
71.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
72.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
73.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
74.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
75.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
78.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

BARAZA LA SABA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Kwanza – Tarehe 20 Januari, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Mhe. Juma Duni Haji: Mimi Juma Duni Haji naapa kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar katika kazi zangu za uwakilishi na nitaitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitazihifadhi, nitazilinda na kuzitetea kwa dhati Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie. (*Makofi*).

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Mimi Nassor Ahmed Mazrui naapa kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar katika kazi zangu za uwakilishi na nitatumikia kwa moyo wangu wote na nitahifadhi, nitazilinda na kuzitetea kwa dhati Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Kabla ya kuendelea napenda nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza Waheshimiwa hao Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa kuteuliwa kwao kuja kujumuika na sisi katika shughuli zetu hizi muhimu kwa kuendeleza shughuli za nchi yetu. Kuteuliwa kwao bila shaka kama tunavyoelewa ni matokeo mazuri ya viongozi wetu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Katibu Mkuu wa CUF yaliyofanyika mwezi wa Novemba na hatimaye tarehe 11 Disemba, 2009 Mhe. Rais amewateuwa waheshimiwa hao.

Napenda niwakaribishe sana kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe na nawaomba Wajumbe wote mshirikiane nao katika kutekeleza majukumu kwa mujibu wa katiba. Wakati huo huo nawaelekeza watendaji wa Baraza hili wachukue nafasi ya kushirikiano nao kwani wao ni Wajumbe wapya, wawaelekeze na hatimaye waweze kufanya shughuli zao vizuri kwa mujibu wa katiba. Nakushukuruni sana na nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wapya. Ahsante sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Nakala za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 1 Novemba, 2009. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny: Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri naomba kuwasilisha hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 199. Naomba kuwasilisha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati ya mezani kuhusu hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa niaba ya kambi ya upinzani naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya upande wa upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 25

Maslahi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi

Mhe. Haji Mkema Haji - Aliuliza**:-**

Hivi sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wanapokwenda katika vikao vya kawaida na vikao vya Kamati za Baraza wanajitegemea kwa usafiri.

(a) Mhe. Waziri huoni kuwa iko haja kwa Wajumbe hao wakapatiwa usafiri au wakawezeshwa kama wanavyowezeshwa Spika, Naibu Spika na Kiongozi wa Upinzani?

b) Wakati wa vikao vya Kamati za Baraza Wajumbe wanalazimika kuomba usafiri kutoka wizara au taasisi wanayoitembelea. Je, utaratibu huu ni mzuri kuendelezwa.?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, katika kuhakikisha wanatekeleza vyema majukumu yao ya Kikatiba na Kisheria, Baraza la Wawakilishi limeandaa utaratibu wa kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kwa kuwapatia stahiki za aina mbali mbali. Stahiki hizo hutolewa kwa utaratibu maalum. Kuna stahiki ambazo Waheshimiwa Wajumbe wote hulipwa bila ya kujali nyadhifa zao na baadhi ya stahiki hupewa Wajumbe wenye nyadhifa maalum kwa mujibu wa nyadhifa zao maalum walizokabidhiwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwa kweli haja ya kuwawezesha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ipo lakini uwezeshaji huo hutegemea hali halisi ya mapato yetu katika Bajeti ya Baraza la Wawakilishi iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha uliopo. Afisi ya Baraza la Wawakilishi imekuwa ikiendelea kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kikatiba kwa ufanisi na wepesi zaidi kwa maslahi ya wananchi kadri hali ya uchumi wetu inavyoruhusu.

   Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe awe na subra na tushirikiane ili tuone kiasi gani tutaweza kupata ufumbuzi wa kuweza kutatua suala hili.

b) Mhe. Spika, utaratibu wa kuendelea kutegemea msaada wa usafiri kutoka taasisi zinazochunguzwa na Kamati za Baraza wakati wa kufanya kazi kamati hizo sio nzuri na haupaswi kuendelezwa. Hivyo, tunalazimika kutumia utaratibu huo kutokana na hali halisi ya mazingira yetu kwa sasa. Mhe. Spika, ni kwamba Baraza letu halijaweza kujitegemea kwa vyombo vya usafiri na bajeti yetu kwa sasa haituwezeshi kumudu gharama za usafiri kwa ajili ya kamati zake zote wakati wanapofanya kazi za kamati. Hata hivyo, tunaendelea kulifanyia kazi suala hili ili siku zijazo Baraza liweze kusafirisha kamati zake wakati wanapokwenda kuzikagua taasisi za umma hadi pale hali itakaporuhusu.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu mama amesema kwamba Waheshimiwa wana stahiki zao wanalipwa, lakini katika stahiki hizo tunao madereva na wafanyakazi wenye mshahara wa hali ya chini na mshahara huo umepandishwa muda mrefu lakini katika marekebisho bado mpaka leo hawajarekebishiwa.

(a) Je, hilo analifahamu na kama analifahamu ni lini litatekelezwa ili tuweze kupata haki hizo ?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, suala hili ni geni kwangu mimi lakini naahidi nitalifanyia kazi kama inavyotakiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya nyongeza kuhusu swali alilouliza Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, ninavyokumbuka ni kwamba nyongeza tulizofanya tulisema zitaanza kutolewa mwezi wa Oktoba, nafikiri imefanyika na kama haijafanyika basi sisi tutafuatilia kuona kwamba kila mtu anapata haki yake, na kama yupo mtu ameonewa basi wacha atufuate tutarekebisha hali ipasavyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake amekiri kwamba utaratibu wa kuchukua gari kutoka mawizarani siku za kamati sio utaratibu mzuri na isingepaswa kuendelezwa. Pia, amekiri kwamba kuna ukosefu wa fedha ndio maana hali ikadorora hivyo.

Mhe. Spika, napenda kumuuliza kwamba jambo lolote lilokuwa zuri huanzishwa kidogo kidogo. Je, haoni kwamba Baraza linastahiki kuanzisha utaratibu huu kwa kuanzia na kamati yetu kubwa kabisa ya *PAC* ili na nyengine zikafuata ili zile wizara zinazoweza kwenda kukaguliwa zisihisi kwamba zimewafadhili kidogo watu hawa?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakubaliana nae Mhe. Mwakilishi kama nilivyojibu katika kifungu (b) cha swali la msingi ni kwamba sio vyema Kamati za Baraza pale ambapo wanapokwenda kuchunguza taasisi zikawa zinahudumiwa. Ingawa wakati mwengine unapokuwa huna kile cha kufikia pale, basi ni bora upate ule usaidizi uende ukamchunguze mtu kuliko kwamba hukupata ule usafiri ukashindwa kwenda kumchunguza mtu kabisa. Lakini nakubaliana naye kuwa tunaweza tukaanzia

katika Kamati ya *PAC* na hili ni suala la kujipanga kwa sababu Wajumbe wa kamati hii sio wengi gari mbili zinatuwezesha kabisa kutumia kwa ajili ya hizo shughuli zao.

Kwa hivyo, hili nakuahidini kwamba tutashirikiana na uongozi wa Baraza naamini hili tutaweza kulitekeleza kuanzia Kamati ya *PAC* na hizo kamati nyengine tunategemea kila mashirikiano yatapokuwa mazuri katika nchi yetu basi tunaahidi kamati zote itapatiwa gari yake.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika swali hili kwenye kifungu (a) maelezo yanasema kwamba katika viongozi ambao wanapatiwa fursa ya usafiri katika Baraza lako tukufu ni wewe Mhe. Spika, Naibu Spika, na Kiongozi wa Upinzani.

(a) Je, ni kweli Kiongozi wa Upinzani wa Baraza hili amepatiwa fursa ya usafiri na ikiwa ni kweli ni vipi na ikiwa si kweli ni lini wizara yake ina mpango wa kumpatia kiongozi wa upinzani kama ambavyo viongozi wa upinzani wana fursa ya usafiri ?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, katika suala la usafiri mpaka sasa hivi kiongozi wa Baraza ambaye tumeweza kumpatia usafiri ni Mhe. Spika peke yake. Mhe. Naibu Spika bado hatujaweza kumpatia usafiri, tunamuomba radhi kwa hili na vile vile kiongozi wa kambi ya upinzani bado hatujaweza kumpatia usafiri hadi sasa hivi, wote tunawaomba radhi kutokana na hali ilivyo. Mhe. Spika, zile stahiki nyengine za kuwawezesha mafuta wakati wa Baraza hizi tunazishughulikia.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba naamini kuwa stahiki hii tuliyoianzisha ya mashirikiano naamini Mwenyezi Mungu atazidisha neema katika nchi yetu. Lakini Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba wenzetu wamefika mbali zaidi kuliko sisi. Wenzetu wa Kenya Mhe. Spika, ana gari tatu, pia ana ulinzi maalum kama Spika. Kwa hivyo, mimi naomba tuendelee na haya mashirikiano basi naamini neema zote hizo zitakuja.

Nam. 83

Uajiri wa Wafanyakazi katika Taasisi za Serikali

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

Serikali imezuia uajiri wa wafanyakazi katika taasisi zake ili kupunguza wingi wa wafanyakazi katika taasisi hizo.

(a) Je, Mhe. Waziri, huoni kuwa zoezi hili litapunguza ufanisi kwa baadhi ya taasisi ambazo zina upungufu wa wataalamu ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 lakini kwanza Mhe. Spika, nilipokuwa najibu swali la mambo ya utumishi naomba nichukue fursa hii kuungana na wewe kumpongeza kwanza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi wake wa waheshimiwa wawili kujaza nafasi hizi. Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, najua katika Baraza la Wawakilishi kuna Tume maalum ya utumishi, lakini mambo yote ya utumishi hatimae yanakuja katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, nimeomba ilivyokuwa na wao wanaingia kwenye utumishi hii, basi nichukue fursa hii kuwapongeza kwa kazi nzuri kabisa uliyofanya Mhe. Spika, ya kuwaapisha.

Sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.83 kama ifuatavyo:

Katika mwezi wa Oktoba, 2007 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha zoezi maalum la kudhibiti utumishi katika Wizara na Idara zake, kitaalamu zoezi hilo lilijulikana kama (*Establishment Control*) sio kuzuia moja kwa moja ni udhibiti. Moja ya lengo la zoezi hili lilikuwa ni kudhibiti matumizi katika bajeti ya mishahara (*Wage Bill Control*).

Katika zoezi hili serikali ilikusudia kudhibiti ajira katika kada ambazo zilionekana kuwa na watumishi wengi zaidi. Zoezi hili lilitekelezwa kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha kwamba halitaleta athari katika utendaji wa serikali.

a) Mhe. Spika, serikali haikuzuia ajira katika kada zote bali katika maeneo maalum ambayo kimsingi yalionekana yanajitosheleza kiutumishi. Serikali inaendelea na ajira kuziba mapengo katika kada za kitaalamu na kuendelea na ajira kwa wahitimu wanaotoka katika Vyuo Vikuu mbali mbali. Pia, serikali inaendelea kujaza mapengo katika Sekta ya Elimu na Sekta ya Afya ambazo zimeonekana kuwa na upungufu wa watumishi.

b) Mhe. Spika, kutokana na umakini mkubwa uliochukuliwa katika utekelezaji wa zoezi hili, imeonekana kuwa halina athari katika utendaji wa serikali. Hata hivyo, chini ya Mkakati wa Marekebisho ya Utumishi Serikalini ambayo tayari umeshatayarishwa. Serikali

itaanzisha zoezi maalum kwa ajili ya kufanya mapitio ya utendaji serikalini (*Functional Review)* ili kubaini mapungufu katika utumishi wake na hatimaye kuweza kuchukua hatua zinazofaa.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kama alivyoeleza Mhe. Waziri lengo na madhumuni sio kuzuia ajira au kuleta ufanisi katika vitengo mbali mbali. Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri katika kitengo hiki cha Ardhi na Upimaji walitoa watendaji wao ili kwenda kuwapa utaalamu zaidi kwani kulikuwa kuna upungufu wa wafanyakazi katika kitengo kile, baada ya kutolewa watendaji hao matokeo yao baada ya kufanikiwa masomo yao hawakuajiriwa katika kitengo kile ili kuondoa kero mbali mbali kwa wananchi.

(a) Je, suala hili analijua na kama analielewa sijui atalichukulia utaratibu gani ili kuhakikisha watendaji hao waweze kuleta ufanisi katika kitengo hicho.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa kweli hilo suala mimi silifahamu, hiyo ni *very specific case* lakini tutashirikiana na Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kufuatilia suala hilo na kuona tatizo liko wapi na kulipatia ufumbuzi. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Mwakilishi baadaye tuweze kubadilishana mawazo kuweza kuwapata wahusika tuone jinsi gani tunaweza kulifanikisha suala hilo.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa kuna wahitimu wa Chuo cha Afya ambao sasa hivi tayari wameshatimiza mwaka mmoja tangu walipohitimu na kwa kuwa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mahospitalini mwetu mna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi wa aina hii na mpaka leo bado watu hawa hawajaajiriwa. Ni kitu gani kilichosababisha watu hawa wasiajiriwe mpaka leo ?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna watumishi wa Wizara ya Afya ambao wamehitimu mafunzo yao katika Chuo cha Afya. Ni kwamba kulikuwa na matatizo kidogo katika uajiri wao, lakini nathubutu kumueleza Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba mipango yote kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeshakamilika na tuko njiani, nafikiri sio muda mrefu wataalamu hao wataajiriwa.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri Nchi (AR) anayeshughulikia Fedha na Uchumi ni

kwamba kada mbili tayari wameshaajiriwa, wauguzi na *clinical officers*. Kada nyengine zinafuatia na maombi tayari yameshapelekwa ofisi ya fedha.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Fedha na Uchumi naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, wakati alipokuwa akijibu alisema kwamba lengo la kuzuia ajira sio kubana moja kwa moja, bali ni kuweka utaratibu mzuri ili kudhibiti fedha za serikali zisipotee. Lakini inasemekana kwa kiwango kikubwa kwamba, baada ya kuondoa utaratibu mbovu wa wafanyakazi hewa limejitokeza jambo jengine, kuna ajira ambazo hazijulikani, yaani mtu anajiajiri au anapewa kibali cha ajira kwenda sehemu fulani wakati kule hatambuliki au hana sifa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili analijua? Na kama halijui lini atalifanyia kazi? Naomba ni mfahamishe kwamba, atapolifanyia kazi mwanzo aanze Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Suala hili akiligundua ataisaidia kwa kiwango kikubwa serikali, lakini kama tunasema lipo wizara yake italifanyia kazi lini ili kuwa na nia ile ile ya kudhibiti utaratibu mzuri wa fedha za serikali?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba kweli hilo suala lipo na limekuwa likitendeka. Lakini kwa bahati nzuri kwa utaratibu tulionao siku hizi huu wa *central payment system* basi tunabaini. Kwa sababu hapa kuna *paper tight*, kuna wizara yenyewe, kuna utumishi na kuna Wizara ya Fedha, sasa hayo mambo lazima yaowane kwenye huo mtandao. Ikiwa mtu kaingizwa tu kinyemela ,basi upande mmoja kompyuta ile haito-click, itasema kwamba huko hatujapata habari kwa hivyo tunamrudisha, ndio maana tukaweza kuwabaini hao.

Kwa hivyo, kweli kulikuwa na *attempt* hiyo ya kufanywa na baadhi ya watu. kwa sababu baadhi ya walimu wakuu walikuwa wakiona kwamba kuna mapengo labda kastaafu mwalimu basi anafanya mipango mwenyewe anampenyeza mtu. Sasa hivyo vikaratasi tulivibaini na tukaweza kudhibiti huo uajiri haukufanyika. Lakini nakushukuru kwa *observation* yako tutajitahidi kama nilivyosema kushirikiana na hizo taasisi tatu kuona kwamba masuala kama hayo hayatokezei. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 51

Asilimia 25 ya Posho za Walimu

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Mnamo mwaka 2006 katika Sherehe za Juma la Elimu zilizofanyika Wete Pemba, Mhe. Rais baada ya kuzingatia malalamiko ya walimu aliiagiza Wizara kuwalipa walimu posho la asilimia 25% la ufundishaji (Teaching Allowance).

(a) Je, Mhe. Waziri, tangu muda huo agizo hilo limetekelezwa?

(b) Iwapo halijatekelezwa kuna sababu gani za msingi zinazoweza kuhalalisha kupingana na agizo la Mhe. Rais?

(c) Ni lini maslahi ya walimu kwa ujumla *(Scheme of Service)* yataangaliwa upya na kuondokana na matatizo kama hayo?

Mhe. Spika: Manaibu Mawaziri wale wanaohusika na kujibu maswali tusiache na ule utaratibu wa kusogea karibu hapa ili akiitwa tu awahi kujibu muda usipotee ovyo. Mhe. Naibu Waziri endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa sababu swali limeanza na maelezo basi na mimi naomba nitoe maelezo kabla sijajibu swali.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika Sherehe za Siku ya Walimu Duniani mwaka 2007 na wala sio mwaka 2006, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alilikubali ombi la walimu la kurejeshewa posho la kufundishia la asilimia 25 na kuziagiza Wizara ya Fedha na Uchumi na wizara yangu kulifanyia kazi suala hilo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba nijibu swali kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, agizo hilo hadi sasa halijatekelezwa kikamilifu kutokana na serikali kuangalia upya Miundo ya Utumishi ya kada mbali mbali. Hata hivyo, juhudi za pamoja kati ya Afisi ya Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi, Wizara ya Fedha na

Uchumi na Wizara yangu imelifanyia kazi suala hilo na tunatarajia litatekelezwa hivi karibuni.

(b) Kuchelewa kutekelezwa kwa agizo hilo kumetokana na sababu nilizozitaja hapo juu.

(c) Wizara yangu imeshaandaa Muundo wa Utumishi *"scheme of service"*mpya wa kada ya ualimu na kuiwasilisha serikalini kwa mazingatio.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba nimuulize swali. Anakiri kwamba tangu kutolewa agizo hilo na Mhe. Rais mwaka 2007 la kurejeshewa posho la asilimia 25 la kufundishia hadi leo bado halijatekelezwa, lakini wamo katika mpango wa kufanya marekebisho ili litekelezwe.

(a) Je, wakati wa kutekelezwa itaanziwa mwaka 2007 au itaanziwa hapa ilipofikiwa sasa hivi?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali mama kwamba wizara yangu imeshaandaa muundo mpya kwa ajili ya wafanyakazi wa Wizara ya Elimu yakiwemo hayo mazingatio ya posho ya asilimia 25, kwa maana hiyo litakapoanza litaanza hapa ambapo tutaanza kutekeleza *scheme* mpya ya utumishi kwa Wizara ya Elimu . Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana na naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu a, b na c.

(a) Kwa kuwa walituarifu kwamba walimu wa diploma kwa sasa wanapewa shilingi elfu kumi na wale wa *degree* wanapewa shilingi elfu kumi na tano, naomba Mhe. Waziri anifahamishe ni kigezo gani kinachotumika kufanya hivyo?

(b) Kwa kuwa jambo hili linawasababishia ugumu sana walimu kimaisha, na ndio sababu ambayo inawafanya walimu wa Zanzibar kukimbilia Mjini Magharibi, Mhe. Waziri suala hili lini atalitatua ili kuwapelekea wanafunzi wa mashamba Unguja na Pemba kupata haki hii ya kupata walimu?

(c) Msemaji wa walimu ni chama cha walimu, ni kwa nini walimu wanaposema ndani ya chama chao wizara inakuwa mbele kuwabania chama hicho?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, mimi sina taarifa kwamba Wizara ya Elimu inawapa shilingi elfu 10 walimu wa diploma na *degree* kama aliavyosema ikiwa sikukosea shilingi 15 elfu. Ninachokijua mimi ni kwamba wanalipwa mshahara wao kama kawaida. Pesa hizo alizozitaja sina habari nazo.

Mhe. Spika, jibu (b) kama nilivyojibu swali langu kwamba tunatarajia hivi karibuni tutatekeleza agizo hilo la Rais kwa kuzingatia mfumo mpya wa *Scheme of Service* ya Ualimu. Kwa maana hiyo, itakapoanza *Scheme of Service* ndipo ambapo tutaweza kutekeleza hilo agizo na utaratibu huu unaweza ukawasaidia kwa kiasi kikubwa sana. Kwa sababu imezingatia hiyo asilimia 25 na nina uhakika kwamba walimu wataridhika kabisa na mshahara huo ambao wataupata sasa hivi ambao kwa kiasi kikubwa umezingatia matakwa ya walimu.

Lakini suala la Chama cha Walimu kuwa Wizara ya Elimu inawabania, mimi napenda niseme kwamba si kweli kwamba wizara inawabania Chama cha Walimu wanapodai au wanapoleta maombi yao, lakini huwa inawasihi kwamba wakae na wizara ili wapate muwafaka wa masuala yao na sio kuzungumza wao pembeni kama inavyotokea sasa hivi.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuanzia mwaka 2007 Mhe. Rais aliposema walimu wapewe zile fedha, ilikuwa kuanzia wakati ule ni haki yao walimu wapewe mpaka kufikia hiyo siku itakayoanza *Scheme of Services*, na kwa kuwa walimu wanapotangaziwa kupatiwa fedha huanza kukopa kabla ile fedha hawajaipata ili wakiipata wakalipa tu. serikali haioni kuwa kuwanyima malimbikizo ya siku hizo zilizopita ambazo tayari wameshazikopea itakuwa imewaweka walimu katika hali mbaya?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu langu mama kuwa tangu mwaka 2007 Mhe. Rais aliagiza kwamba Wizara ya Elimu na Wizara ya Fedha ishirikiane kuwapatia asilimia 25 ya posho la kufundishia. Lakini kama nilivyojibu katika swali mama kwamba wizara yangu inashirikiana na taasisi ambazo zinahusika moja kwa moja na mambo ya ajira, kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha kwamba mambo yote haya mwisho wake yanaishia katika Afisi ya Rais na

Baraza la Mapinduzi. Kwa maana hiyo, sisi kama Wizara ya Elimu tayari tumeshaliwasilisha suala hili kwa mamlaka inayohusika kwa maana hiyo ya kupatiwa ufumbuzi.

Pia, tamko hilo la Rais halikuagizwa wafanyakazi waende wakakope kwa tamko hilo na kwa maana hiyo, kwa muda wote serikali haiwanyimi au haiwasababishii kuwa wabaki na madeni kwa sababu hawakuagizwa waende wakakope.

Mhe. Spika: Unajua wananchi huwa wanafuata viongozi wao, nikitaja semina hapa Waheshimiwa huwa wanaanza kukopa. Hiyo ni sehemu ya *jokes* tu. (*Kicheko*)

Nam. 31

Ufungaji wa Vituo vya Afya Siku za Mapumziko

Mhe. Ame Mati Wadi (Kny. Mhe. Haji Mkema Haji) – Aliuliza:-

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilianzisha utaratibu wa kufungua Vituo vya Afya mijini na vijijini kwa kutoa huduma siku za Jumamosi na Jumapili pamoja na siku za sikukuu.

(a) Je, kwa nini siku hizi vituo vingi havifunguliwi siku za Jumamosi na Jumapili, wala siku za sikukuu.

(b) Huoni kwamba kutofungua vituo katika siku hizo kunaongeza ugumu wa maisha kwa wananchi wetu kwa kuwa hulazimika kutumia fedha kidogo wapatazo kutoa nauli kwenda mijini kufuata huduma za afya, badala ya kutumia fedha hizo kujinunulia angalau chakula.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake No. 31 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, vituo vinavyotoa huduma kwa Jumamosi na Jumapili hadi sasa ni: Chumbuni, Shaurimoyo, Kidongochekundu, Matarumbeta, Fuoni na Chukwani. Vyengine ni Bwejuu, Muungoni, Muyuni, Jambiani, Kizimkazi Mkunguni, Mtende, Tumbatu Gomani na Nungwi.

Hata hivyo, huduma za afya kwa siku za sikukuu zinapatikana katika Hospitali za Mnazi Mmoja, Kivunge, Makunduchi pamoja na na Wete, Chake Chake na

Mkoani. Wizara ya Afya imo katika jitihada za kueneza huduma hizi katika vituo vyote kufuatana na upatikanaji wa wafanyakazi wa ziada katika vituo hivyo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa nampongeza Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa juhudi yao kubwa ambayo wameionesha katika nchi yetu juu ya kuharakisha maendeleo ya afya katika vijiji vyetu mbali mbali. Moja wapo katika hayo umefika wakati katika maeneo mengi ya nchi yetu nyumba za madaktari zimejengwa ili kunusuru hili ambalo limeulizwa. Mimi swali langu liko hapa.

Katika majibu yaliyojibiwa Mhe. Waziri katika maeneo muhimu ya mkusanyiko wa watu mbali mbali na kwa kuwa katika harakati kama hizi ukiacha Makunduchi, Nungwi, Tumbatu na kwengineko. Je, kijiji cha Kiwengwa ambacho ni muhimu sana kwa mkusanyiko wa watu na harakati za maisha ana mpango gani wa kufikisha huduma hiyo ya kila siku kuweko kwa huduma ya afya kwa siku za Jumamosi na siku za Sikukuu?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kama jibu mama linavyoeleza kuwa tunajitahidi kuweza kupeleka huduma maeneo yote, kidogo tuna upungufu wa hao wafanyakazi, pindipo mambo yakiwa mazuri ya kupatikana wafanyakazi tunamhakikishia Mhe. Ali Suleiman tutampelekea mfanyakazi huyo katika kijiji cha Kiwengwa na maeneo mengine yote ambayo hawapo wafanyakazi hao. Ahsante sana.

Mhe. Aziza Nabahan Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kwa siku ya leo nikauliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Waziri ametwambia kwamba vituo vilivyobakia haviwezi kupatiwa huduma za Jumamosi ya Jumapili kwa sababu hakuna wafanyakazi. Lakini je, kwani hatuwezi kuwatumia wafanyakazi waliokuwepo kwa kuwasaidia posho tu kwa zamu wakawa wanakwenda kule tukaondosha hili tatizo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, suala la kuongeza posho kwa wale ambao wanaingia katika *shift* waweze kuongezwa posho ili waweze kuingia kwa muda wa kazi zaidi. mimi nadhani suala lake si baya lakini linahitaji kufikiriwa vizuri. Kwa sababu suala la kutoa *over time* kwa wafanyakazi hawa inaweza kusababisha mzigo mkubwa katika wizara. Kwa hivyo, kuna haja ya kuzingatia na sisi tunalichukua suala lake tutaliangalia hali itakuwaje. Lakini katika suala letu zima tunavyoelekeza sasa hivi tuweze kuwaweka wafanyakazi wote katika maeneo hayo ili kupunguza hili suala la kuwapa *over time* wale ambao watakuwa wamezidisha muda wa kazi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, mimi naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. licha ya siku za Jumamosi ya na Jumapili na siku za sikukuu, lakini hizi siku za kawaida Kituo chetu cha Pujini daktari huwa haonekani, anaonekana leo, kesho haonekani. Sijui Mhe. Naibu Waziri taarifa hii anayo na kama anayo atatusaidia vipi?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, taarifa ya kuwa Kituo cha Pujini daktari hapatikani kwa muda wote mimi taarifa hiyo sina. Kwa sababu mimi mwenyewe ninapokuwepo Pemba katika kituo ninachopenda kukitembelea mara nyingi ni hicho cha Pujini na Mwenyezi Mungu ananijaalia kila nikienda daktari namkuta, wauguzi nawakuta, sasa hii taarifa ya kuwa siku nyengine wanakwenda na siku nyengine hawendi kwa kweli sina.

Naweza kusema kwamba labda kwa kuwa nimepeleka taarifa kuwa ninakwenda, lakini siku nyengine nazuka tu ghafla nakwenda nasema nataka kutembelea vituo huwa sipangi ratiba wala simpelekei mtu taarifa, nakwenda na ninawakuta. Lakini madhali Mheshimiwa kaleta taarifa yake hii tutajitahidi kuifanyia kazi ili suala hili kama lipo basi lisiweze kuendelea.

Nam. 4

Usajili wa Namba za Gari

Mhe. Amina Iddi Mabrouk – Aliuliza:-

Sheria Namba 7 ya Mwaka 2003 inaruhusu gari yoyote ya kigeni kukaa muda wa miezi mitatu (3) Zanzibar kabla ya kubadilishwa namba yake ya usajili. Vile vile, gari yoyote iliyosajiliwa Zanzibar ikipelekwa Tanzania Bara ikisha tu kusajiliwa huko, zile nambari zake za usajili za Zanzibar ni lazima zirejeshwe kwa mujibu wa sheria.

(a) Je, Mhe. Waziri, sheria inamlazimisha Msajili wa Magari wa Tanzania Bara kurudisha nambari za usajili wa gari ambayo imesajiliwa Bara kutoka Zanzibar.

(b) Mhe. Waziri utaratibu huu wa kurudisha nambari za usajili kutoka sehemu ambayo gari ilisajiliwa kwanza unasaidia nini.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 25(1) inayoitwa *Road Transport Registration and Licencing of Legal Registration.* Mmiliki wa chombo cha Moto kilichosajiliwa na msajili atatakiwa kuomba kufutiwa usajili wa chombo chake ambacho kimesajiliwa kwa mujibu wa kanuni hiyo. iwapo moja ya mambo yafuatayo yatatokea.

1. Iwapo chombo cha moto kitasafirishwa au kitahamishiwa moja kwa moja nje ya Zanzibar na kutolewa taarifa kwa msajili.

2. Iwapo chombo cha moto kitapotea, kitaharibika au kuibiwa.

3. Iwapo chombo cha moto kitakuwa hakifai kutumika.

4. Iwapo chombo hakitakuwa na wajibu wa kusajiliwa kwa mujibu wa vifungu vya kanuni hizi.

(b) Kwa mujibu wa utaratibu wa usajili wa vyombo vya moto, kufutwa usajili wa chombo cha moto kilichohamishwa moja kwa moja hapa nchini husaidia mambo yafuatayo:-

- Kumuwezesha msajili kuwa na taarifa na kumbukumbu sahihi ya vyombo vyote vya moto vilivyoko hapa nchini na vilivyoingia na kutoka kwa wakati.

- Kukiwezesha chombo cha moto kutokuwa na usajili katika maeneo tofauti.

- Kuwa na udhibiti wa kuepuka au kutumika katika kufanyia uhalifu. Pia, kuwa na udhibiti wa ukwepaji wa mapato ya serikali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mara baada ya usajili wa vyombo vya moto kutoka katika Manispaa yetu ulihamia katika *ZRB* na ndio maana leo Mhe. Waziri wa Fedha akawa anajibu maswali kupitia chombo hicho. Lakini kwa mshangao Mhe. Spika, mwanzo wananchi walifarajika sana kwamba kazi inayofanywa pale ni nzuri na huduma inayopatikana kuleta usalama katika vyombo vyetu. Lakini sasa limetokea

wimbi kubwa sana, vyombo mbali mbali vinavyosajiliwa havipati nambari zinazohusika hasa kwenye magari ukiacha mapikipiki au vespa.

Je, Mhe. Waziri alieleze Baraza hili na wananchi wajue, kuna tatizo gani lililokwamisha wakati mtoa huduma anahusika amlipe anayepeleka huduma yake kikamilifu, lakini anapewa namba za bandia ambapo unaweza kusema namba zile zinahatarisha hata usalama wa vyombo vile kwa wananchi wetu wanaotembea katika barabara. ana mpango gani wa kuliondoa tatizo hili?

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kidogo nitoe maelezo kwamba haya masuala ya leseni yanatolewa na *ZRB*. Lakini nataka kusema kwamba kazi zote za kitaalamu zinafanywa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wenyewe, yule bwana anayeitwa *Silve*r kule maarufu kwa jina hilo au ofisi yao ndio wanaopasisha gari, kule *ZRB* ni malipo tu, ni taratibu za malipo naomba hiyo ifahamike. *ZRB* haipasishi gari hawana utaalamu huo.

Sasa uandishi wa magari baada ya kazi ile kumalizwa ni kweli unafanywa na *ZRB*, hapo nakubali kweli kulikuwa na matatizo ya kiufundi ya yule aliyekuwa anafanya kazi ile alikuwa na matatizo kidogo lakini yanafanyiwa kazi. Hilo nakubali ni kweli. Lakini suala la upasishaji na ufundi bado inaendelea kufanywa na Wizara ya Mawasiliano, lakini kazi ya kutoa nambari ni kweli *ZRB* wanafanya baada ya mambo kukamilika yule mtu analipa ndio anapewa nambari. Sasa kweli ule uandishi, vile vibati kulikuwa na matatizo nakiri hilo na tunalijua na tunalifanyia kazi ni matatizo ya kiufundi Mhe. Spika.

Nam. 1

Watalii wa Daraja la Kwanza

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Tunasikia Watalii wa Daraja la Kwanza hupatikana sharti kwanza tutimize mambo yote muhimu na ubora wa huduma, kwanza uwanja wa ndege uwe na sifa zote za Kimataifa, miundo mbinu ya usafiri, ubora wa usafiri wa ndani, mawasiliano, usalama wao na mali zao na mwisho ndio hoteli na huduma zake zinazotolewa.

(a) Je, Mhe. Waziri, Watalii hao wa Daraja la Kwanza na sisi hapa petu tunapokea.

(b) Kwa mwaka 2009 hadi kufikia Septemba 2009 tumepokea wangapi.

(c) Ni hoteli zipi na wanazofikia kwa hapa Unguja na Pemba kama tunazo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 lenye kifungu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Watalii wa Daraja la Kwanza hapa kwetu Zanzibar tunapokea.

(b) Mhe. Spika, lazima nikiri kwamba ukusanyaji wetu wa takwimu hautoi ufafanuzi wa madaraja ya watalii bali hukusanya idadi yote ya watalii wanaoingia nchini. Hadi kufikia Septemba 2009 jumla ya watalii 58,000 walikuwa wameingia nchini na kufikia mwezi Disemba 2009 jumla ya watalii 135,000 walikuwa wameingia nchini ukilinganisha na 128,000 walioingia nchini mwaka jana au mwaka 2008.

(d) Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kueleza katika kifungu (b) kwamba takwimu zetu hazibagui madaraja ya watalii tunaopokea, lakini kimsingi Watalii wa Daraja la Kwanza huwa wanafikia Hoteli za nyota 4 na 5 zilizopo hapa nchini na kwa ujumla hoteli kwa kulingana na *classification* iliyofanywa katikati ya miaka ya 1990 tulikuwa tuna hoteli kumi na nne za nyota 5 ambazo sasa hivi ni kumi na saba, na tulikuwa na hoteli kumi na mbili (12) za nyota 4 ambazo sasa hivi ni 15. Hata hivyo, wizara ina mpango wa kufanya tena *classification*, kwa sababu kama nilivyosema utalii unabadilika mara kwa mara na kwa hivyo matakwa pia ya class za mahoteli huwa zinabadilika.

Kwa upande wa Pemba hoteli zinazofikia watalii wa namna hii ni Fundulagon iliyoko Mkoani Pemba na Mantariff iliyoko upande wa Makangale kule Pemba.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kutokana na hali ngumu ya uchumi duniani, Zanzibar inategemea asilimia karibu 80 au 90 uchumi wake kutokana na utalii. Tegemeo langu kubwa kwamba mtalii anayeingia kwa daraja lake ndiye mwenye malipo makubwa ikiwa daraja la kwanza malipo yanakuwa makubwa na wale tunaowaita vishuka malipo yao huwa madogo.

(a) Je, Mhe. Waziri pamoja na juhudi hiyo ya kuhakikisha kwamba tunaingiza watalii wengi namshukuru mpaka sasa hivi tumefikia kiasi ya watalii laki moja

na thalathini elfu si haba na huenda wakafikia karibu lakini mbili na kidogo, Mwenyezi Mungu atujaalie wafikie huko karibu kufikia mwezi wa saba mwaka huu tuliokuwa nao.

(a) Je, ana mpango gani kuhakikisha wataalamu wake wanampa takwimu sahihi watalii waliokuja daraja la kwanza na waliokuwa daraja la tatu ili mapato yaeleweke na yaingie katika mfuko mkuu wa Hazina ili mapato hayo yanufaishe wananchi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Utalii na Uwekezaji: Mhe. Spika, wazo ni zuri la kukusanya takwimu kwa mchanganuo ule alioupendekeza ili tujue hakika watalii gani wa daraja la kwanza, kiasi gani wanaingia katika nchi yetu. Lakini hata hivyo mchanganuo huo hautatupa sura ya kusema kwamba kwa sababu watalii wa daraja la kwanza wameingia kiasi hiki kwa hivyo wameingiza nchini kiasi hiki. Kwa sababu ukusanyaji wa mapato hauendani na madaraja ya utalii, bali huendana na biashara iliyofanyika katika hoteli. Ahsante.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe, Spika, Mhe. Waziri wakati anajibu majibu yake hapa amekubali kwamba watalii wa daraja la kwanza wanafika. Lakini anasema hawana utaratibu wa kubagua madaraja na pia anasema kwamba hakuna viwango vinavyopangwa kwa madaraja. Sasa nilikuwa nataka nimuulize haoni kama kutokufanya hivyo ni kupoteza mapato ya serikali kwa sababu duniani popote matumizi ya watalii wa daraja la kwanza ni makubwa inaeleweka hivyo na ndio maana hata hoteli wanazofikia ni zile *5 Stars* na sio ndogo ndogo.

Sasa kutokana na hayo mapato yanayotokana na watalii wa daraja hili yatakuwa ni makubwa. Kwa hivyo, haoni kwamba kutakuwa na haja ya makusudi kuchukuwa juhudi kwenda kama huko Fundo la Guu ambako anasema kuwa wanafikia wakapata takwimu watalii hawa wameingia wangapi ili kujua viwango vile vinavyopatikana kutokana na kile kinachoingizwa na watalii hawa ambacho kwa kutofatilia kwao, anaweza kukubaliana na mimi kwamba wanapoteza mapato kwa wingi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Utalii na Uwekezaji: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika suala la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Ali Suleiman Ali kwamba ni wazo zuri kukusanya watalii kutokana na madaraja yao. Na hii kazi si ngumu kwa sababu ni kuchukua takwimu kutoka mahoteli yanayofikia yale kama nyota tano, nyota nne na kadhalika. Lakini kama nilivyosema ukusanyaji wa mapato hautokani na daraja la mtalii bali biashara inayofanyika katika

hoteli na vile vitanda jinsi vilivyotumiwa na wakusanyaji mapato wanatumia madaftari wakati wa kuingia wageni katika hoteli zile. Lakini hata hivyo si vibaya pia kulinganisha takwimu tunazokusanya sisi kupitia bandarini na *Air Port* kulinganisha na takwimu za mapato wanazokusanya *ZRB* ili tujue kama kweli mahoteli yanatoa ripoti sahihi. Kwa hivyo, ukusanyaji hauendani na madaraja bali ni biashara inayofanywa katika mahoteli. Ahsante.

Nam. 117

Uendelezaji wa Wanawake Jimbo la Chambani

Mhe. Abass Juma Muhunzi-Aliuliza**:-**

Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Ajira kwa kazi zake nzuri za uhamasishaji na uwezeshaji kinamama katika maendeleo, na kwa namna anavyoshughulikia kesi za udhalilishaji kijinsia na ajira za watoto.

(a) Kwa kuwa ndani ya Jimbo langu la Chambani wanawake katika Shehia zote wamepata uwezeshwaji kiasi wa miradi na sasa wanashirikiana katika vikundi vyao vya maendeleo na kwa kuwa wamenituma Mhe. Waziri wao nimuombe aende kuonana nao wapate ushauri zaidi, Je, Mhe. Waziri utakuwa na muda huo na kupanga safari yeye na mimi kuwatembelea wanawake hao.

(b) Kwa kuwa wanawake wa Mkoani wamejidhatiti sana katika kuendesha biashara katika bandari ya Mkoani ndani ya mazingira mabaya ya biashara ndogo ndogo, Je, Mhe. Waziri atakubaliana nami kuwa kuna haja ya kuwatembelea wanawake hao ili awape ushauri katika kazi zao.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto- Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla sijajibu suala nililoulizwa nichukuwe nafasi hii nitoe pongezi na shukurani za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa utelezaji wake wa kipengele cha Muafaka na kuweza kuwateuwa Wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui. Baada ya Mhe. Katibu Mkuu kumtambua Rais wa Zanzibar mambo yote kuwa katika njia moja nampogeza sana na nawapogeza sana Waheshimiwa hawa wawili mlioungana na sisi katika Baraza letu hili tukufu la kutunga sheria, Baraza la kutetea haki zetu, Baraza mwanana.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Abass Juma Muhunzi kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, napenda nipokee shukurani za dhati na niahidi kwamba wizara yangu itaendelea kushirikiana na wananchi wa nchi nzima hii ya Zanzibar na sio Chambani peke yake, katika juhudi zote za kuleta maendeleo na kwamba ziara anayoisisitiza sana Mheshimiwa itapangwa na kutekelezwa kwa idhini yako Mhe. Spika, kwa sababu inatia wasi wasi alivyokazania Mheshimiwa ziara hii.

b) Wizara yangu imewatembelea wanawake wanaofanya biashara ndogo ndogo katika bandari ya Mkoani na kugundua kwamba ni kweli wanafanya biashara katika mazingira yasiokubalika, ikiwa ni pamoja na kufanya kazi katika maeneo yaliokatazwa. Kwa hivyo, kwa mashirikiano na viongozi wa Wilaya, Jimbo, pamoja na taasisi nyengine husika, wizara yangu itachukua juhudi ya kuwaelimisha kinamama hao njia bora za kufanya biashara katika mazingira yanayokubalika na ya kiusalama. Ahsante.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa kujibu swali langu, isipokuwa ninalo suala la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe., Spika, katika Bandari ya Mkoani tutakubaliana kwamba ule ndio mlango wa kuingia Pemba mazingira ya watu wanaofanyia biashara ndogo ndogo pamoja na umuhimu wake katika kufuta umasikini ni mazingira magumu na machafu sana kuna msongamano wa magari yanayopakia na wauza maembe na wauza ngisi. Lakini hata vile vibanda ambavyo vimejengwa kwa ajili ya kufanya mikahawa na biashara ndogo Mhe. Spika, ni vibanda ambavyo kwa kweli havioneshi kwamba ule ni mlango wa mji.

Suala langu kwa sababu Taasisi kama ile *ZSSF* ilikuwa ikijitahidi kufanya uwekezaji wa miundo mbinu kuangalia hawa wanaofanya biashara ndogo ndogo pamoja na taasisi nyengine ambazo zinajitahidi kufanya kazi ndogo ndogo, je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuonana na taasisi hizi ili kuhakikisha kwamba zinafanya uwezekezaji wa vibanda ambavyo vitatoa sura nzuri ya mlango wa mji ili kuwapatia nafasi wafanyabishara ndogo ndogo wafanyekazi ili wafute umaskini. Lakini vile vile kueka mlango wa mji wa Pemba kuwa mzuri. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 5

Leseni za Biashara za Kuvusha Watalii

Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Aliuliza**:-**

Hivi sasa visiwani mwetu limezuka wimbi la Kampuni, taasisi na hata watu binafsi hufanya biashara za kuvusha wageni, watalii na hata wananchi wa kawaida kuwapeleka visiwani kwa ajili ya kupiga mbizi *diving*, kuvua, au kutembea tu baharini kwa kutumia vyombo tofauti zikiwemo Boti za mashine, ngarawa ikiwa ni mradi wa wavushaji kujipatia maisha.

(a) Mhe. Waziri, leseni za biashara kama hiyo zinatolewa na taasisi gani.

(b) Je, Biashara hiyo inaendeshwa kisheria au tunafanya tu kienyeji ilimradi mkono wende kinywani.

(c) Ziko taasisi ngapi zilizosajiliwa rasmi kufanya biashara hiyo Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake nambari 5 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Wizara yangu kupitia Afisi ya Mrajis wa Meli Zanzibar inasajili na kutoa leseni kwa vyombo vyote vidogo vidogo vinavyotembea baharini vyenye urefu wa kuanzia mita 4 zikiwemo boti za mashine, ngarawa na kadhalika. Kwa upande wa kupiga mbizi *diving,* Afisi ya Mrajis wa Meli hadi hivi sasa haitoi leseni hizo, ila inatarajia kutoa leseni kama hiyo hapo tu Mamlaka itapoanzishwa rasmi, kwani Sheria ya Mamlaka ndio inayoipa uwezo huo. Hivi sasa wachunguzi *Inspectors* wa meli wanajaribu kushirikiana na wapiga mbizi kwa ajili ya kuangalia usalama wao pamoja na vifaa wanavyotumia.

Nam. 44

Mfumo wa Matangazo wa "DIGITAL"

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza**:-**

Hivi sasa dunia iko katika mkakati wa kuondokana na mfumo mkongwe wa kurusha na kupokea matangazo ya radio na TV wa *Analogue* kuelekea mfumo mpya wa *Digital.*

(a) Mhe. Waziri, je, serikali imejiandaa vipi kukabiliana na mabadiliko hayo ya Teknolojia.

(b) Inasemekana kuwa nguvu za Teknolojia hiyo *signal digital* zinapatikana katika anga la Tanzania Bara. Je, hali kwa Zanzibar ikoje.

(c) Siku zote mabadiliko ya Teknolojia yana gharama zake ikiwemo utaalamu na bei za vifaa. Je, Serikali inachukua hatua gani kuwahamasisha wafanyabiashara ili kuangalia uwezo wa wananchi wetu kumudu kununua vifaa vitakavyotumika katika mfumo mpya wa *Digital*.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kabla sijamjibu napenda kuchukuwa nafasi hii kuwapongeza sana Wawakilishi walioapishwa leo na tunaahidi kwamba tutashirikiana nao kwa karibu kabisa katika Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kabla ya kujibu suala Nam. 44 lenye kifungu a, b, na c nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli hivi sasa dunia iko katika mchakato wa kuondokana na mfumo mkongwe wa urushaji na upokeaji wa matangazo ya Radio na TV wa *Analogue* na kuelekea mfumo mpya wa *Digital*. Hii ni baada ya makubaliano ya mkutano wa nchi wanachama wa shirika na Mawasiliano la Kimataifa *ITU – International Telecommunication Union*.

Mkutano huo uliofanyika Geniva mwaka 2006, nchi wanachama walikubaliana kuanza rasmi matangazo ya Televisheni kwa ajili ya *Digital* yaani *Digital Video Boadcast – DVB* na kuanzisha huduma mpya ya redio za *Terrestrial Digital Audio Broadcast – TDAB* kuanzia Julai 2006.

Mhe. Spika, hivi sasa tumo katika kipindi cha mpito ambapo matangazo ya *digital* yanatakiwa kwenda sambamba na matangazo ya *analogue*. Tarehe ya mwisho ya kipindi cha mpito ambacho tunatakiwa kufunga mitambo ya *analogue* ni Juni 2015 kuwa kwa matangazo ya televisheni katika bendi ya *UHV* na Juni 2020 katika bendi zote mbili ya *UHF* na *VHF*.

Mhe. Spika, hii ina maana vifaa vyetu vingi tulivyokuwa navyo majumbani kwetu na tunakoendelea kuvinunua pamoja na hizi TV zinazoletwa ambazo si mpya havitofanya kazi itapofikia kipindi hicho na wenzetu waliopo katika nchi zilizoendelea wao tayari wameshaanza kuhamia katika mifumo hiyo ya *Digital* ndio maana TV nyingi hizi zinaletwa nchini kwetu.

Mhe. Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Zanzibar kama ni nchi iliyoungana na Tanganyika na kuzaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianza kuchukua hatua za utekelezaji wa mpango wa mageuzi mara tu baada ya kupitishwa kwa azimio la *ITU* Juni 2006 kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kuandaa mpango wa kitaifa kuwezesha mageuzi hayo, ambao tayari mpango huo umeshapitishwa kwa sekta nzima ya habari.

ii. Kufanya utafiti wa wasikilizaji redio na watazamaji televisheni ili kufahamu gharama zitakazohitajika kwa ajili ya mageuzi na kutathmini athari za kimazingira zinazoweza kutokea kwa vifaa hivyo visivyoweza kutumika kutafutiwa mwahala pa kutupwa.

iii. Kukamilisha maandalizi ya rasimu na sera ya utangazaji kuongoza sekta hiyo humu nchini kupitia teknolojia hiyo ya *Digital*.

iv. Kutoa mafunzo kwa watendaji wa vituo binafsi na vya serikali katika mifumo ya matangazo na mawimbi ya *Digital*.

v. Kuwapatia uwelewa wananchi juu ya faida, hasara na athari za mageuzi ya teknolojia ya utangazaji kutoka *Analogue* kuelekea *Digital*.

vi. Kuifanyia marekebisho Sheria ya Utangazaji, namba 7 ya 1997 ili iende sambamba na mageuzi ya teknolojia hiyo ya *Digital* ambayo leo inawasilishwa hapa Barazani..

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa masuala ya utangazaji sio katika mambo ya Muungano, Zanzibar kama nchi imepewa mawimbi yake, ambayo yanasimamiwa na Tume ya Utangazaji Zanzibar moja kwa moja kutoka *ITU* Geniva. Kwa hiyo, suala la kuwa nguvu za Teknolojia hiyo kuwepo Tanzania Bara pekee naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba hili sio la kweli.

Kuna wananchi kadhaa tayari wameshaanza kupokea hapa kwetu Zanzibar kupitia *satellite* zao wanazomiliki za kimataifa kama vile *Sky Digital* na *DS TV* ambayo ni sehemu ya hiyo *Sky Digital* ambayo wanapokea moja kwa moja majumbani.

(c) Ni kweli kwamba mabadiliko ya Teknolojia yana gharama zake. Vituo vya kutangazia vitalazimika kubadilisha mitambo ya kutangazia na wananchi watalazimika kununua vifaa vitakavyoweza kupokea matangazo ya digital. Kwa hali hiyo, serikali itashauriwa kutoa msamaha wa kodi moja kwa moja wa vifaa hivyo vinapoingizwa nchini itakapofikia wakati huo. Hatua hii itahamasisha wafanya biashara kuagiza vifaa hivi na wananchi wetu kuweza kumudu kununua vifaa hivyo vya *Digital* itakapofikia kipindi hicho kilichopangwa cha matangazo hayo kuhamia na kuanza majaribio ya matangazo ya *Digital* hapa Zanzibar.

Hivi sasa vifaa hivyo ni ghali huko ulimwenguni kama ilivyo kawaida ya teknolojia mpya yoyote ambayo huwa inakuja hapa nchini kwetu kama vile ya simu za mkononi ilipokuwa mwanzo ilikuwa ghali lakini huendelea kupungua bei kila muda wa uzalishaji unapoendelea kufika. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija-Aliuliza:-

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba waandishi na watangazaji tayari wamepata mafunzo ningeomba atwambie hadi sasa ni watangazaji wangapi na waandishi wa serikali wamepatiwa mafunzo haya.

(b) Wataalamu wanatwambia kwamba ili kuweza kupata matangazo haya kwenye televisheni zetu ni lazima tuunganishe na kifaa maalum. Naomba nijue ni kifaa gani na je, Zanzibar tayari kimefika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba niseme kwamba tayari mafunzo kupitia semina mbali mbali zilizoandaliwa na Tume ya Utangazaji hapa Zanzibar zimeshatolewa na bahati nzuri moja nilibahatika mimi kushiriki ilitolewa pale *Palace Museum* na wahusika wakuu wa sekta ya habari hapa Zanzibar.

Lakini mafunzo ya moja kwa moja tayari yametolewa kutia waandishi wetu wa Habari wanne ambao walipata mafunzo mbali mbali yaliyotolewa Tanzania Bara na nje ya nchi na hivi sasa kuna mpango maalum ambao Tume ya Utanganzaji imeandaa kupitia kila kituo ambacho wao huwa wanawapa leseni ya kutoa matangazo hayo ikiwa ya Tv au ya Redio au Redio FM pamoja na Redio nyenginezo basi huwa wanapitia kila kituo ili kutoa taaluma vipi namna ya kuhama kutoka *Analogue* kwenda *Digital* na mawimbi ya *Digital* yatakuwa wanafanyakazi vipi.

Kwa hiyo, taaluma hiyo pamoja na mafunzo haya sio kwamba tunasema yamemalizika lakini yataendelea kuanzia hivi sasa mpaka Mwenyezi Mungu akitujaalia mwaka 2015.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Mwakilishi arudie suala lake la pili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, wataalamu wanatwambia kwamba ili uweze kupata matangazo kwenye televisheni zetu ni lazima tuunganishe na kifaa gani na je, Zanzibar kipo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kuna kifaa maalum kinachoitwa *Desk Top Unit* yaani *DTU* hicho hupokea matangazo yaliokuwa na *Analogue* hivi sasa na mle ndani kuna kitu kinaitwa *Convasion Unit* huyabadilisha yale mawimbi au zile *signal* hubadilishwa kutoka *Analogue* na kutokea kwenye *Digital* na baada ya hapo huingia kwenye seti ya TV. Kama Mhe. Spika, utakumbuka hapo zamani palipokuwa na teknolojia mpya imeshaanza lakini sisi tulikuwa tunaendelea kupokea TV za zamani TV zetu zote ilibidi kitiwe kitu kinaitwa *crystal* kuweza kupokea matangazo.

Sasa kwa hii teknolojia mpya iliyokuwepo na hizi TV zilizokuwepo sasa baadhi yake zitaweza kufanya kazi ikiwa hicho kifaa cha *Desk Top Unit* kitapatikana na ndio maana nikasema kwamba watu wengine tayari majumbani kwao wameshaanza kutumia hii wale waliokuwa na *DSTV* basi wanapewa kifaa kinaitwa *Receiver.* Lakini ndani yake kuna kitu kinaitwa *Desk Top Unit* ambacho kinapokea matangazo ya *Digital.* Lakini hayo yanabadilishwa kwenda kwenye mfumo wa zamani ili TV ipate kuonesha kwa *Analogue*. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abass Juma Muhunzi-Aliuliza:-

(a) Mhe. Spika, mabadiliko ya mfumo huu wa Teknolojia yanaonesha kwamba yatakuwa na gharama kubwa sana kwa sababu suala la mawasiliano ni suala la Muungano. Je, Serikali ya Muungano inasaidia vipi katika kufanikisha mabadiliko haya ili kuona kwamba Zanzibar haitumii gharama kubwa zaidi.

(b) Kwa sababu suala hili linagusa moja kwa moja maisha ya watu ni kwa kiasi gani serikali imejizatiti kuwahamasisha na kuwaelimisha watu kuhusu mabadiliko haya na namna ambayo yataathiri maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba niseme kwamba Sheria ya Mawasiliano ya Tanzania ni ya Muungano. Lakini nimetaja katika majibu yangu ya awali kwamba Sheria ya Mawasiliano ya Utangazaji sio ya Muungano. Sheria ya Mawasilinao inasimamiwa na chombo kinachojulikana kwamba *TCRA*, Mamlaka ya kusimamia Mawasiliano katika sheria yao hiyo inataja wazi kwamba masuala ya utangazaji hayatokuwa ya Muungano na katika sheria hiyo yanatajwa wazi. Lakini Zanzibar itakuwa na mamlaka yake huru na wananchi kusimamia sekta ya Habari na Utangazaji.

Kwa hivyo, naomba nisahihishe kwamba sheria ya Mawasiliano ndio ya Muungano lakini sheria ya Bahari na Utanganzaji si ya Muungano. Kwa hivyo, sheria hiyo tunasimamia sisi wenyewe na hatutegemei kupata chochote kutoka kwa wenzetu katika sheria ambayo tunasimamia sisi wenyewe.

Mhe. Spika, suala lake la pili Mhe. Abass Juma Muhunzi ameuliza gharama ambazo watakazopata watu ambapo tunachukuwa hatua gani kuwafahamisha hivi sasa. Hivi sasa tayari Tume ya Utangazaji imeshaanza Program maalum kupitia vyombo vya habari mbali mbali kuelimisha kwamba hivi vifaa tunavyovinunua basi tuwe makini ndani ya kununua huko, kwa sababu kuna vile vifaa vya kisasa na vile vya zamani.

Lakini hivi tunavyonunua kwa sasa tunaweza kutumia kwa muda wa miaka 5 ndio maana bado serikali haijachukuwa hatua ya kupiga marufuku vifaa hivi visiingizwe nchini ili wafanyabiashara nao waendelee kupata riski zao. lakini riski zile zitapatikana kwa muda wa miaka 15 itakapofika mwaka 2015 basi vifaa hivi vitakuwa havifai kutumika na vile vichache ambavyo vitafaa kutumika ndio itabidi sasa vinunuliwe iwe hiyo *Desk Top Unit*.

Lakini kwa kuwa tunajua maisha yake pia si marefu sana vifaa hivi vina maisha kati ya miaka 5 mpaka 7 kwa yule anaetengeneza nakupa maisha ya vifaa hivi kuanzia miaka 5 mpaka 7. Kwa hiyo, ndio maana sasa hivi serikali haijachukuwa hatua yoyote ya kuzuia kuingia vifaa hivi kwa sababu tunajua wananchi wanaendelea kufaidika mpaka pale tarehe ya kuhamia itapokuwa tayari. Kwa hiyo, hiyo taaluma tunaendelea kutoa Mhe. Spika, na kwa kutumia kiriri hiki chako pia tunaendelea kutoa taaluma hii pia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kutokana na utaalamu huu uliopo na teknolojia hii ya kuingia katika *Digital* kutoka *Analogue* tuna TV kama tatu hivi Tanzania zimo katika mtandao wa *satellite.* Lakini TV yetu bado haijaingia katika mtandao wa *satellite.* Hii ni kutokana na kwamba bado hatujaingia katika *digital* au kuna matatizo mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, hii inatokana na kwamba bado hatujaingia kwenye mfumo wa digital.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa uhai na afya njema na kuweza kusimama hapa kuwasilisha taarifa ya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997.

Mhe. Spika, lakini kabla sijafanya kazi hiyo naomba uniruhusu kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Abeid Karume kwa kuweza kuwateua ndugu zetu wawili Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kuwa wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi kutoka chama cha upinzani (CUF).

Mhe. Spika, tunawakaribisha waheshimiwa hawa ili waweze kuungana nasi katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wetu.Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Nam. 7 ya 1997.

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) kwa kuiongoza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wakati tulipowasilisha mswada huu katika kamati hiyo. Namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa msaada mkubwa uliotuwezesha kuupitia mswada huu na kufanya marekebisho ambayo sasa hivi yametuwezesha kuleta mswada huu Barazani.

Lakini pia nimshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii pamoja na Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa waliyoipa wizara yangu wakati wa kupitia mswada huu.

Mhe. Spika, Tume ya Utangazaji ni taasisi ya serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya 1997 na kuanza kazi zake rasmi mwaka 2002.

Mhe. Spika, majukumu ya msingi ya tume hii ni kama haya yafuatayo:

1. Kugawa mawimbi ya kutangazia (*frequency)*.

2. Kutoa leseni kwa vituo vya utangazaji vinavyoanzishwa hapa Zanzibar.

3. Kusimamia na kukuza biashara ya vifaa vya utangazaji humu nchini mwetu.

Mhe. Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake na kukabili changamoto za mabadiliko ya teknolojia ya utangazaji duniani, wizara imelazimika pamoja na mambo mengine kuchukua hatua ya kuifanyia marekebisho sheria yake na kuingiza vipengele vyenye kukidhi viwango vya maazimio ya kimataifa na ongezeko la mahitaji mapya katika Sekta ya Utangazaji duniani.

Mhe. Spika, madhumuni ya waraka huu ni kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Nam. 7 ya 1997 ili iende na mahitaji ya sasa. Mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii yanakusudia kuingiza mahitaji ya utangazaji *(digital)* kufuatia mageuzi makubwa ya Sekta ya Utangazaji duniani, mwelekeo wa mageuzi hayo na kubadilisha sekta ya utangazaji kutoka mfumo wa sasa wa *analogueueeeee* kwenda katika mfumo mpya kabisa wa *digital*.

Mhe. Spika, sababu za kufanyiwa marekebisho ya sheria iliyopo. Kwanza takriban mwaka wa tatu tangu mataifa mbali mbali yalipokubaliana kutiwa saini azimio la *Regional Radio Conference (RRC)* ya mwaka 2006 huko Geneva, lenye madhumuni ya kubadili mfumo wa teknolojia ya utangazaji kutoka *analogueueeeee* kwenda katika mfumo wa *digital*. Azimio hilo limeweka utaratibu ambao unapaswa kufuatwa na nchi jirani na zile nyengine zinazoweza kuathirika na mabadiliko hayo ya mfumo mpya wa teknolojia ya utangazaji.

Mhe. Spika, Hiki ni kipindi cha mpito cha utekelezaji wa malengo hayo, baada ya kipindi hicho kumalizika mnamo mwaka 2015 utangazaji kwa *analogueueeeee* hautapaswa kuomba ulinzi yatakapotokea maingiliano ya utangazaji wa *digital*.

Mhe. Spika, shughuli za utangazaji hapa Zanzibar zinaongozwa na Sheria Nam. 7 ya 1997 kama nilivyoeleza hapo mwanzo, sheria hii inasimamia urushaji wa matangazo kwa njia ya sauti na picha lakini haikutaja moja kwa moja kuwepo kwa utangazaji kwa njia ya *digital*. Hivyo, ipo haja ya kuifanyia marekebisho

sheria hii na kuandaa kanuni ili kukidhi matakwa ya Sera ya Utangazaji Zanzibar na mabadiliko ya teknolojia hii mpya ya *digital*.

Mhe. Spika, waraka huu tunapendekeza kufanyiwa marekebisho katika Mswada wa Sheria ya Kuweka Utaratibu Mpya wa Utoaji wa Leseni ya Urushaji wa Matangazo kwa njia ya *digital* yenye kutoa nafasi ya kuwepo kwa huduma tatu tofauti. Huduma hizo zinahusu yafuatayo:

1. Msambazaji wa ishara ya ujumbe *(Multiplex operator)*

2. Mtayarishaji wa Maudhui *(Content Operator)*

3. Huduma ya ziada *(Additional service)*

Hivyo, utaratibu wa leseni unaopendekezwa unazingatia nyanja hizi tatu. Baadhi ya vifungu vya Sheria Nam. 7 ya 1997 imerekebishwa sehemu ya kwanza ya mswada inayozungumza mambo ya utangulizi ambayo yamo katika kifungu cha kwanza mpaka cha nne kimewekwa mapendekezo ya tafsiri.

Sehemu ya pili inayoanzisha Tume, umbile, kazi, uteuzi wa Katibu Mtendaji na Mwenyekiti pamoja na Mrajis na masharti ya usajili pia yamewekewa mapendekezo ya sifa.

Sehemu ya tatu inayoshughulikia mambo yote yanayohusiana na leseni zitakazotolewa yamewekwa mapendekezo makubwa ya kimuundo.

Vile vile, sehemu ya sita inayoweka mambo mbali mbali ikiwemo makosa na adhabu na uwezo wa Waziri kutengeneza kanuni muhimu kwa utekelezaji mzuri wa kuvipa nguvu vifungu vya sheria ambayo ipo. Imewekwa mapendekezo ya mabadiliko ya faini vile vile.

Mhe. Spika, Hitimisho, mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii ni muhimu sana kufanyika ili twende sambamba na mabadiliko ya teknolojia na kuweza kufikia lengo la kuingia katika teknolojia ya *digital* ifikapo mwaka 2015. Hata Waheshimiwa Wawakilishi mbali mbali wamekuwa wakitueleza tumejiandaa vipi kama serikali kuingia katika mfumo mpya wa teknolojia.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, natumai kuwa Wajumbe wamepata muda wa kutosha wa kupitia mapendekezo haya, naomba sasa washauri vizuri ili sheria hii iweze kufanyiwa marekebisho ipasavyo na tuweze kuipitisha kwa ajili ya utekelezaji. Pia, kuweza kukabiliana na hayo mabadiliko ya teknolojia ambayo mwaka 2015 kama tulivyosema kwamba teknolojia hii ya *analogue* itakuwa imeshapitwa na wakati.

Mhe. Spika, baada ya hayo, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya hadhara hii nikiwa na afya njema, ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi katika Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997.

Mhe. Spika, pia kwa niaba ya kamati yangu napenda kutoa pongezi kwa Mhe. Rais kwa kutimiza Katiba yake kama inavyotaka kuwateua Wajumbe wawili kutoka kambi ya upinzani. Nachukua fursa hii kuwapongeza Wajumbe hao Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa kuteuliwa. Naamini kwamba tutashirikiana vyema katika kutekeleza azma ya wananchi wetu wa Zanzibar kuwaletea maendeleo ya pamoja.

Mhe. Spika, afya njema ni neema kubwa sana ambayo mara nyingi kuonekana na kuthaminiwa kwake ni pale mwanadamu anapoikosa kutokana na maradhi mbali mbali ama mitihani iliyomzunguka na hatimae kushindwa kutekeleza yale aliyokusudia ama anayotakiwa kufanya kisheria. Hivyo basi, ni busara sana kuitumia neema hii katika mambo mema na miongoni mwa mambo hayo ni hili la kuwatumikia wananchi wetu ambao wametutuma kuwawakilisha na kuwafikishia salamu zao ikiwa ni pamoja na matatizo yao mbali mbali katika Baraza hili Tukufu.

Mhe. Spika, Baraza lako Tukufu lina majukumu mazito. Majukumu hayo makubwa ni yale yaliyoelezwa na Katiba katika kifungu cha 88 ambapo kifungu cha 88 (1) (a) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, kinaelekeza kwamba ”Baraza la Wawakilishi litakuwa na kazi ya kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo”.

Mhe. Spika, ifahamike kwamba, mantiki ya kifungu hicho sio tu kutunga sheria mpya, lakini inajumuisha kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali ambazo kutokana na mabadiliko ya wakati na haja nyengine yoyote itakapotokezea na kupelekea haja ya marekebisho ya sheria husika. Katika kutekeleza hili, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imewasilisha mbele ya Kamati yetu, Mswada wa Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji, Zanzibar Nam.7 ya mwaka 2010 kwa kuirekebisha Sheria ya Utangazaji ya Zanzibar Nam. 7 ya

mwaka 1997, kwa ajili ya kwenda sambamba na mahitaji ya utangazaji wa *digital* na kuondokana na mfumo uliopo sasa wa *analogueuee*, kufuatia mageuzi makubwa ya utangazaji duniani.

Mhe. Spika, Kamati yetu imefarijika na kuwasilishwa kwa Mswada huu ambao utasaidia kukua na kuimarika kwa Sekta ya Utangazaji Zanzibar na kuimarisha uhusiano mkubwa baina ya Vyombo vya Habari vya Serikali na vya Watu Binafsi na hatimae kuimarika kwa Demokrasia na Utawala Bora nchini.

Mhe. Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Mhe Ali Juma Shamuhuna. Aidha, shukurani hizi pia zimwendee Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa kuhudhuria mbele ya Kamati wakati Kamati ilipoujadili Mswada huo. Kuhudhuria kwao kumeipa faraja Kamati na zaidi kuweza moja kwa moja kuyapokea maoni ya Kamati kuhusiana na marekebisho kama yanavyoonekana katika waraka wetu wa marekebisho.

Mhe. Spika, sitakuwa muungwana iwapo nitashindwa kuwashukuru na kuwapongeza Watendaji wa Wizara hii ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wanaohusika kwa mashirikano wanayoyatoa kwa Viongozi wao na hata kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa mbele ya Kamati, wakati Kamati ikitekeleza kazi zake za kawaida na hata kupitia Miswada na Bajeti za Wizara hii.

Mhe. Spika, sasa nigeukie upande wa Kamati yetu. Mhe. Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mzuri waliouonesha kwa kuupitia kwa kina mswada huu na hatimaye kuupitisha katika ngazi ya Kamati ili leo hii ujadiliwe katika Baraza lako Tukufu. Naomba niwatambulishe Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Ame Mati Wadi	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Haji Ali	-	Mjumbe
6.	Mhe Mohamed Ali Salim (Mullah)	-	Mjumbe
7.	Mhe. Haji Faki Shaali	-	Mjumbe
8.	Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	-	Mjumbe
9.	Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	-	Mjumbe
10.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
11.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
12.	Ndg.Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Spika, kwa kweli Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar ya mwaka 2010 umekusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997, ambayo hujulikana kwa lugha ya Kiingereza *(The Zanzibar Broadcasting Commission Act, 1997).* Miongoni mwa mambo ya msingi na ya pekee ni ukweli kwamba ili uweze kutoa fursa zaidi ya kukuza na kuimarisha Sekta ya Habari Zanzibar.

Mhe. Spika, Sekta ya Habari ni muhimu sana katika kuendeleza nchi yetu, kwani ndio inayochochea ari ya wananchi katika kufanya shughuli za ujenzi wa Taifa lao. Habari zinapopatikana kwa wakati na usahihi, zinakuwa ni kioo kwa kila mtu. Mhe. Spika, nchi haijengwi kwa matofali pekee, lakini uwazi na uwajibikaji ni misingi imara ya kuimarisha Utawala Bora na hatimae kuisaidia serikali kuwajibika ipasavyo kwa wananchi wake.

Kufikia kiwango hiki cha uwazi na uwajibikaji katika ujenzi wa Taifa letu, sekta ya habari inayotekeleza majukumu yake kisiasa na kiufanisi inahitajika sana katika ustawi wa jamii. Jamii inayo habari kwa kila tokeo na ukweli halisi wa mabadiliko ya ulimwengu, ni lazima ustawi. Ni ustawi huu Mhe. Spika, ambao Kamati yetu inausimamia.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, sekta hii inahitaji uangalifu mkubwa sana ili kuimarisha ustawi wa wananchi, heshima na mali zao. Wanahabari wanadhima kubwa sana ya kuhakikisha wanafuatilia habari za ukweli na uhakika. Aidha, wanahitajika kuheshimu maadili ya habari muda wote wa utekelezaji wa majukumu yao, sanjari na hili, mfumo wa *digital* unaokusudiwa kutumika sasa bila ya shaka utawasaidia wanahabari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, imepiga hatua kubwa sana katika sekta hii ya habari. Hii inatokana na kukua kwa vyombo vya habari vya Serikali na Watu Binafsi. Zanzibar ya leo ni ya uhuru wa habari, wananchi wa leo sio tu kuwasikiliza watangazaji wale wale waliowazoea wa TVZ na Sauti ya Tanzania Zanzibar, ama kusikiliza taarifa hizo hizo zinazotangazwa kwa siku mbili au zaidi bila ya mabadiliko, bali tokea kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Utangazaji na hatimae marekebisho yake, ni kuendelea kuwanufaisha wananchi wetu kusikiliza na kupata taarifa za uhakika za televisheni na redio yetu, lakini pia kusikiliza na kupata habari mbali mbali kupitia redio binafsi na *cable* zilizoanzishwa kwa mnasaba wa kukuza demokrasia nchini mwetu.

Mhe. Spika, ni matumaini yetu basi kwamba iwapo Mswada huu utapita na hatimae kuwa sheria, kutawafanya wananchi wetu waendelee kupata haki hii ya habari kwa ujuzi na umahiri wa hali ya juu.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi na sifa zote hizi, Kamati yetu inasikitishwa sana kudharauliwa kwa redio yetu na kuonekana ni kwa ajili ya matangazo ya vifo tu! Aidha huzuni zetu pia zinahusiana na kudharauliwa kwa televisheni yetu ya TVZ ambayo pamoja na ukweli kwamba ni televisheni ya kwanza ya rangi Afrika Mashariki, sasa inaonekana kuachwa nyuma na televisheni nyengine Tanzania na ulimwenguni kwa ujumla, katika maendeleo ya sayansi na teknolojia. Ni matumaini yetu kuwa, kupitia marekebisho haya ya Sheria yetu ya Habari Zanzibar, imani hizi potofu miongoni mwa wananchi zitaondoka kwa vyombo vyetu hivi kuimarika zaidi na kutekeleza majukumu husika kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba mswada huu uliowasilishwa mbele ya Kamati haukuwa mkubwa, ni wenye sehemu mbili tu, sehemu ya kwanza ni utangulizi ambayo imejumuisha jina fupi, kuanza kutumika na kusomwa sambamba na Sheria Nam. 7 ya mwaka 1997, sehemu ya pili inaeleza marekebisho katika kifungu cha 2, kufutwa kifungu cha 4 na marekebisho ya kifungu cha 6,7,10,12,14 na 15. Aidha, wakati Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilipoupitia mswada huu, wajumbe walipendekeza marekebisho kadhaa, baadhi ya hayo ni haya yafuatayo:

Mhe. Spika, kwa kuanzia, tafsiri ya maneno yaliyomo kwenye ukurasa wa 162, katika kifungu cha 3, yawekwe kwa mpangilio wa herufi (*alphabetical order*), pamoja na maneno hayo kuandikwa kwa herufi ndogo kwa mnasaba wa sheria mama. Kufanya hivi kunatoa sura nzuri na uandishi mzuri wa sheria zetu, ikiwa ni pamoja na kumrahisishia mtumiaji kupata neno anapolitafuta.

Pia, Kamati imependekeza marekebisho ya neno ”chombo” lililopo katika kifungu cha 5, kijifungu cha (4), mstari wa tatu kutoka juu, lisomeke ”taasisi”. Mhe. Spika, neno ”taasisi” linaleta maana halisi iliyokusudiwa ukilinganisha na neno ”chombo” ambalo lina maana nyingi na tata, jambo ambalo halishauriwi katika uandishi wa sheria. Sheria nzuri ni ile isiyo na utata ambayo hata mwananchi wa kawaida akiisoma anafahamu yaliyokusudiwa. Aidha, kutumia maneno yenye utata sio tu hupelekea kupotosha maana iliyokusudiwa, lakini pia kunapelekea ugumu wa utekelezaji wa sheria husika.

Mhe. Spika, baada ya kuyapitisha marekebisho ya kufuta kijifungu cha (3) cha kifungu cha 6 cha Sheria mama, Kamati imeshauri kuwa, vijifungu vya (4) na (5) vya kifungu hicho, visomeke vifungu vya (3) na (4).

Mhe. Spika, Kamati yetu imefanya marekebisho ya herufi kwa baadhi ya maneno ambayo yalitokana na makosa ya uchapaji kama ifuatavyo:-

Ukurasa wa 163 kifungu cha 6 mstari wa kwanza kutoka juu, neno ”kipwa” lisomeke ”kipya”. Mhe. Spika, kwa kawaida ingeonekana marekebisho haya hayana haja kwa mintarafu kwamba mswada wa lugha ya Kiingereza hauathiriki na makosa haya ya uchapaji, lakini kwa kuzingatia kwamba miswada hii inapowasilishwa mbele ya Kamati na hata Barazani, imetafsiriwa ama imeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Ni vyema Kamati ikafanya marekebisho ili usahihi upatikane inapojadiliwa na hatimae kurekebishwa kwa miswada hii.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 6 B, maneno ya pembeni (*marginal note*) yamerekebishwa na yanatakiwa yasomeke ”kusita kuwa mjumbe” badala ya ”Muda wa Wajumbe” ili kwenda sambamba na maudhui yanayokusudiwa kwenye kifungu hicho.

Mhe. Spika, matumizi ya alama na vituo yamezingatiwa na Kamati yetu, wakati wa kujadili mswada huu ambapo katika kifungu cha 7 (b) mstari wa pili kutoka juu alama ya kituo kidogo (,) imewekwa baina ya neno ”redio” na ”televisheni”. Aidha kiunganishi ”na” kiwekwe baina ya neno ”televisheni” na ”video”. Marekebisho haya yamefanywa ili kuleta maana iliyokusudiwa katika kifungu hicho. Alama na vituo vina nafasi muhimu sana katika uandishi wa sheria na vinaposhindwa kutumika ipasavyo, maana halisi inayokusudiwa katika kifungu ama sheria husika, itashindwa kufahamika.

Mhe. Spika, ukiupitia mswada wa Kiswahili kama ulivyojadiliwa katika Kamati, utaukuta umekosa kifungu cha 8, ambapo baada ya kifungu cha 7 katika ukurasa wa 163, kifungu kinachofuata ni namba 9. Kwa mnasaba huu, Kamati imependekeza kutafsiriwa kifungu hicho kwa maana ile ile iliyomo katika mswada wa Kiingereza kama inavyoonekana kama waraka wetu wa marekebisho.

Mhe. Spika, kabla sijamalizia, kwa ruhusa yako naomba nichangie tu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kwahani. Mhe. Spika, naamini kwamba wakati huu wa dunia ya habari umefika wakati sasa wa kushughulikia mambo yetu mengi kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu. Mhe. Spika, pia si vibaya kusema kwamba hivi sasa katika nchi yetu ya Zanzibar tuna tatizo kubwa lililojitokeza la umeme. Lakini kwa kuwa tumesema habari ni sehemu muhimu ya wananchi wetu kupatiwa kwa kila siku, naipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa jitihada yake kubwa ya kuhakikisha kwamba wenzetu wa Sauti ya Tanzania Zanzibar wanafanya kazi zao bila ya kukosa.

Hii ina maana kwamba tatizo la umeme ni sehemu moja lakini na wananchi kupata habari ni sehemu ya pili. Kwa kutumia uwezo wao mdogo waliokuwanao wanajitahidi kutokana na uwashaji wa *generator* na hali ngumu

waliyonayo wananchi kupata habari kwa kutumia redio zao za mkononi, au redio zinazotumia betri za madukani.

Mhe. Spika, hii inaonesha dhahiri kwamba habari ni sehemu moja muhimu na ni sehemu moja wapo ya mwananchi kumweka karibu na lolote ambalo linaweza kutokea, kwa faida yake yeye na kwa faida ya wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, nakuja kwenye hitimisho baada ya maelezo hayo mafupi yenye ufafanuzi mpana. Naomba nikushukuru tena kwa niaba ya kamati yangu kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu mswada huu.

Aidha, si busara kushindwa kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa ustahamilivu wao na usikivu ambao kwa kweli umenifanya nimalizie hotuba yangu bila kuchoka, ingawaje nikiwa bado nina hamu ya kuendelea, lakini kutokana na kanuni zinazotuongoza ni lazima nikomee hapa.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia maelezo ambayo nimeyatoa awali na kwa umuhimu wa mswada huu nachukua nafasi hii kutamka kuwa mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani, tunauunga mkono mswada huu kwa asilimia 100 na tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, waujadili na kuunga mkono mswada huu kwa asilimia 100. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana tena tukiwa hai katika Baraza hili, kwa nia ya kutekeleza yale tuliotumwa na wananchi wenzetu wa Zanzibar kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, sitakuwa na mchango mkubwa sana kwa sababu Mswada wenyewe nao si mkubwa sana. Hata hivyo katika kifungu cha 6(b) ni vyema iongezwe ibara ndogo (d) yenye kuongeza neno “kufa kwa mjumbe wa bodi”.

Mhe. Spika, katika kipengele cha uhodhi au umiliki hapakuwekwa ufafanuzi mzuri ambapo bado sio Wazanzibari wengi wenye uwezo wa moja kwa moja wa kuanzisha vyombo vya utangazaji. Hivi sasa inasemekana Wachina wanataka kuanzisha idhaa yao hapa Zanzibar, Je, suala hili limeangaliwa vipi?

Mhe. Spika, jamii inahitaji huduma ya kuelimishwa kwa njia tofauti ya vyombo vya habari kama zilivyofafanuliwa. Aidha, vibali na ukwasi wa vyombo, ni vyema marekebisho yangeweka wazi vipaumbele au huruma kwa baadhi ya wadau wanaohodhiwa na Kamisheni ya Utangazaji. Mfano halisi. Mhe. Spika,

ni jinsi vyombo vyenye kutoa elimu ya kiroho (Radio za kidini) ambazo zina umuhimu mkubwa katika jamii na kwa utulivu wa Taifa letu ambapo hutozwa kodi sawa na radio za muziki ambazo hupata matangazo. Wafadhili na wadhamini wa mashirika na makampuni ambao hupendelea zaidi idhaa za muziki kutangaza mambo yao, vyenginevyo vyombo hivi vya dini vikubali navyo kutoka katika mfumo wa ucha Mungu kwa waumini ambapo kwa jamii yetu itakuwa ni hasara.

Mhe. Spika, kuzifikiria idhaa hizi za FM za kidini ni muhimu kwani ikiwa Tume ya utangazaji haikuzifikiria zitakufa. Idhaa kama ya Adhana FM mbali na tatizo la umeme ambalo limeinyamazisha, lakini zipo fununu kuwa mmiliki wake ameonyesha kunawa mikono. Pia, makampuni yenye kutoa huduma za minara na *Frequency* wamekata huduma zao na wao wanashindwa kwa sababu zile zile za kukosa wafadhili na wadhamini.

Mhe. Spika, pia idhaa ya Al Noor nayo inakumbwa na tatizo hilo hilo. Hivyo, kwa hali hiyo kuwe na unafuu wa idhaa za kidini katika mpangilio mzima wa leseni na malipo mengine ili zihuike.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kutaka ufafanuzi wa maeneo mawili yenye kutoa vibali vya matumizi ya *frequency* kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, kwani inasemekana kuna vikwazo vya idhaa za FM za Zanzibar kupata vibali huko Dar-es-Salaam kupeleka matangazo yao, lakini FM za Tanzania Bara wanapata ruhusa hiyo hapa Zanzibar, tunaomba ufafanuzi katika hili.

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza naomba na mimi nitoe mchango binafsi kwa niaba ya Wilaya yangu ya Chake Chake, lakini kwa niaba ya watu wa Pemba, wanasikitishwa hivi sasa kwamba hawapati matangazo ya televisheni kwa muda mrefu. Kwa hivyo, na wao kwa kupitia jukwaa hili la wawakilishi, ambapo ndipo anapoweza kueleza matatizo yao. Basi wanaomba na wao wafanyiwe utaratibu ili waweze kuona Idhaa ya Televisheni ya Zanzibar, kwani wanakosa kuona mambo mengi yanayotokea Zanzibar, wanashindwa kusikia taarifa za habari zanazotokea Zanzibar.

Vile vile, Mhe. Spika, wanakosa kuona maendeleo yote yanayotokea Zanzibar hasa wakati huu wa maelewano na maridhiano katika nchi yetu. Kwa hivyo, wanaiomba Idara hii ya Televisheni au Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, basi wafanye kila linalowezekana ili wananchi wa Pemba nao waweze kufaidi matunda ya Mapinduzi hasa kwa vile yamewekwa na mzee wetu Sheikh Abeid Aman Karume Marehemu, Mwenyezi Mungu amrehemu akhera aliko. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kuwa mchangiaji wa mwanzo ukiacha hawa wachangiaji rasmi, maana yake nasema hawa ni wachangiaji rasmi kwa mujibu wa kanuni, sasa mimi ni mchangiaji wa hiyari, nimeamua mwenyewe.

Mhe. Spika, mimi kwa bahati nzuri ni Mjumbe wa kamati iliyohusika kupitia mswada huu ambao ni mfupi sana na jina langu bahati nzuri limetajwa na Mwenyekiti wangu Mhe. Ali Suleiman Ali. Ni kweli nathibitisha ni Mjumbe wa kamati hiyo. Pia, nathibitisha nimeshiriki katika kuupitia mswada huu mfupi ulioletwa Barazani. Kwa maana hiyo nina uelewa kwa kiasi cha marekebisho ya mswada huu tunaoujadili.

Mhe. Spika, kimsingi huu mswada hauna mazonge ni marekebisho madogo ambayo yamekuwa *motivated* na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ndio kimsingi hasa ya marekebisho haya. Lakini Mhe. Spika, itabidi tuseme yaliomo ndani ya marekebisho na pia tuseme yaliomo katika sheria mama yenyewe, ili mawazo yetu yende vizuri.

Mhe. Spika, nikianza na kifungu cha 7 cha sheria mama ambacho kinarekebishwa kwa kuongezwa kifungu (b) ambapo hiki kinazungumzia suala la kudhibiti na kusimamia shughuli za utangazaji zinajumuisha vipindi vya redio, televisheni na video.

Mhe. Spika, suala hili mimi naliona kwa kweli ni gumu sana, kwa ulimwengu wa leo kudhibiti vipindi vya redio, kudhibiti vipindi vya televisheni. Afadhali hizo video kidogo zinaweza kudhibitiwa uingiaji wake. Lakini haya mambo mawili Mhe. Spika, mimi nayaona ni magumu, kwa nini nikasema magumu.

Mhe. Spika, unajua sasa hivi habari tunazipata kwa kupitia hiyo televisheni na redio. Lakini pia sasa hivi watu wanapata habari kwa kupitia kwenye kompyuta zao zilioko majumbani, kompyuta sasa hivi ni *multipurpose*, kompyuta ni redio, kompyuta ni televisheni, kompyuta ni video, kompyuta ni kila kitu katika ulimwengu wa leo.

Sasa udhibiti wa habari unakuwa mgumu sana. Lakini Mhe. Spika, hata tukija kwenye hizo televisheni. Mhe. Spika, ukija kwenye maeneo ya Mji Mkongwe hata kwenye baadhi ya ng'ambo sasa hivi, watu wengi wameunganishwa na hizi *cable* televisheni ambapo mtu anaona moja kwa moja kwenye televisheni anayoitaka duniani *live*, kwa hivyo, huna njia ya kuichuja.

Mhe. Spika, na ulimwengu wa leo sifikirii kwamba itafika siku serikali ipige marufuku tuseme hatutaki *cable* televisheni, tutakuwa hatueleweki. Kwa hivyo, nasema tujitahidi, lakini kwa kweli hili suala mimi naliona ni gumu na naliona

ni zito. Ama kudhibiti uingizaji wa video hilo linawezekana kwa asilimia 10, uwezekano huo upo. Maana kudhibiti kwa asilimia 100 haiwezekani. Mtu akiwa na video *cassette* yake bwana akitaka kuingia ataingia tu, wala huna njia ya kumzuia. Lakini nasema haya mambo ambayo ni moja kwa moja mtu anapata matangazo kwa kupitia vifaa vyake alivyokuanavyo nyumbani, kwa kweli mimi nasema hili jukumu walilopewa hawa wenzetu naona ni gumu.

Jengine Mhe. Spika, ni kwamba hata ukiangalia vyombo vyetu vya ndani sasa hivi. Angalia televisheni ya serikali. Televisheni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mara nyengine inajiunga na televisheni nyengine za nje, hivi kweli utajua nini kitaoneshwa wakati wewe umejiunga pale *live*, unaweza uka *predict* mbele kunakuja nini. Kwa hivyo, ndio nikasema haya msuala ni magumu. Siku hizi kuna FM za BBC ambazo zinajiunga moja kwa moja na matangazo ya moja kwa moja kutoka Nairobi. Hivi wewe unaweza uka- *predict* nini kitatangazwa. Ndio nikasema kwa kweli siwezi kusema moja kwa moja kwamba ni *utopia* hii sheria, lakini niseme kwamba utekelezaji wake mimi nauona ni mgumu sana kwa ulimwengu wa leo kudhibiti haya mambo.

Mhe. Spika, jengine ambalo naliona lina ugumu katika sheria hii, hapa nimezungumza pamoja na sheria mama, kwamba tunafanya marekebisho katika suala la leseni, kuna marekebisho yanafanywa katika suala la utolewaji wa leseni. Lakini mimi naangalia yale masharti ya leseni yenyewe.

Mhe. Spika, ukiangalia sheria mama kuna masharti yaliyowekwa kwa waliopewa leseni. Nafikiri iko katika kifungu cha 15 cha sheria mama kifungu kidogo cha (3). Kwa bahati nzuri sheria yenyewe inakuwa ni kwa lugha ya Kiingereza hakuna sheria ya Kiswahili bahati mbaya, mswada tu unakuja kwa Kiswahili. Kwa hivyo, nitaisoma kama ilivyo Mhe. Spika, ili nisije nikaharibu maana halafu nitatafsiri.

Kifungu cha 15(3):

> *"Subject to this section it shall be the duty of every person holding a broadcasting licence under this Act.*
>
> (a) *to present all news factual accurate in partial in non partisan manner as allowed by the law".*

Mhe. Spika, nasema bado ni gumu katika vyombo vyetu vingi vya habari na hata vya serikali. Lakini nataka nitumie fursa hii kuishukuru sana Zenj FM kwa hili. Kwa kweli Mhe. Spika, Zenj FM hili wanalitekeleza. Kama wao wenyewe hawapo hapa basi napenda muwapelekee salamu. Kwa sababu mara zote wanapomuhoji mtu, kama kuna mkutano, basi watakapohoji sehemu A, basi hawakubali ni lazima watakwenda na sehemu B hiyo ni lazima watafanya

hivyo. Lakini kama kuna tatizo basi hawamchukui mhusika mmoja kumuhoji, ni lazima watakwenda na kwa mhusika wa upande wa pili. Bado wengine hawajaiga suala hili. Kwa hivyo, nasema hawa wenzetu kwa kweli walipopewa leseni suala hili wameliheshimu.

Tuje kwenye suala (B)

> *" To present current affairs in a balance clear factual accurate in partial manner".*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili nalo nasema lina matatizo, kwa sababu kuna redio nyengine, mimi sisikii taarifa ya habari, wakati wote utasikia magoma ama wakati mwengine utasikia mawaidha. Mimi nadhani hata kama redio ni ya kidini, lakini kuwapasha habari wananchi wake nadhani ni jambo la wajibu, kutumia kama dakika 10 kuwapa habari wananchi wake ya matukio yanayotokezea, nadhani huu ni wajibu wa kisheria ambao umo katika masharti ya leseni. Ndio nasema bado utaona hayafuatwi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, labda niizinduwe Tume ya Utangazaji kwamba hii sheria itabidi waisimamie kikamilifu. Kwa sababu dini hata kama imekusudiwa, sawa wewe waache tu watumie over 99 *percent* ya programu zao kwa mambo ya dini, lakini hata kutumia ile 1 *percent* pale kwa kutoa habari kwa wananchi, nadhani hii haiwezi ikawaharibia wala haitawafanya kama ni redio ya Kiislamu basi itakuwa redio haijatoka kwenye Uislamu na kama ni madhehebu mengine ya dini nyengine bado nadhani itakuwa haijatoka katika maadili ya dini yake.

Lakini kuna mambo ya kimaendeleo au kuna majanga yametokea katika nchi nadhani si wajibu wa redio ya serikali tu wananchi kupewa habari. Hata vyombo vya habari vya binafsi hii ni *role* yao kwa mujibu wa matakwa ya leseni. Lakini nasema haya Mhe. Spika, kwa vyombo vyengine vya habari huyaoni. Sasa sijui Tume ya Utangazaji inasubiri mpaka lini mambo haya kwamba kwa nini hamuwazindui hawa na wakati ni sharti moja wapo la leseni.

Mhe. Spika, jengine vile vipindi vinatakiwa viwe vya *high standard*. Lakini kwa kweli ukiisikiliza redio binafsi kwa baadhi lakini vipindi vyao sio *standard.* Kuna redio moja ukiifungua utasikia vichekesho chekesho tu, hakuna hasa kitu *substantial* kinachotangazwa. Kwa hivyo, kuwa na redio nyingi za aina hii sijui kaka zinasaidia sana nchi au vipi. Inaweza ikasaidia ajira kwa vijana wawili au watatu na ajira ni kwa vijana wawili au watatu, kwa sababu siku hizi watu wanatumia mambo ya teknolojia ya kileo. Nadhani na umma ilikuwa ufaidike na hili.

Jengine Mhe. Spika, ambalo mimi linanichanganya. Unajua ZFA Chama cha Mpira cha Zanzibar, hawataki kushiriki katika michezo ile ya kombe la Taska kwa sababu kuna matangazo ya ulevi. Lakini kuna redio ambazo zimepewa leseni na SMZ wanatangaza matangazo ya ulevi zipo. Kwa hivyo, mambo haya bado hatujajua nini tunakitaka na nini hatukitaki. Maana ikiwa timu ya mpira ya nchi unasema tushiriki Taska kwa sababu kunatangazwa ulevi, lakini kuna redio nyengine zinatangaza ulevi na *condom*. Ipo redio moja inatangaza na mambo ya ulevi na *condom*. Ikiwa unatangaza biashara ya *condom*, unatangaza ulevi hizo ndio *ethics* za Zanzibar na humu sheria imesisitiza *ethics* za Zanzibar. Kwa hivyo, nasema Tume ya Utangazaji bado hawajajipanga kufanya kazi sawa sawa.

Mhe. Spika, jengine ambalo naona bado halijasimamiwa vizuri na Tume ya Utangazaji, ni kuhusu hili suala la msisitizo juu ya vipindi au programu zetu kuwa zinakwenda sambamba na utamaduni wetu wa Zanzibar na utamaduni wa Afrika. Unajua mimi napata tatizo ukiniambia utamaduni wa Afrika ni upi. Maana Afrika hakuna utamaduni mmoja. Hivi ina- *make sense* Zanzibar kukubali kila utamaduni wa Afrika. Nadhani tungesisitiza utamaduni wa Zanzibar na utamaduni angalau wa Tanzania unafanana. Lakini kuwa na msisitizo wa kuwa na programu zinazokwenda sambamba na utamaduni wa Zanzibar au utamaduni wa Afrika.

Mhe. Spika, katika Afrika wakati mmoja nilikuwa nasikiliza redio, nadhani ilikuwa ni BBC, kuna mzee mmoja ni Mrwanda, bwana huyu alikuwa anahojiwa na kusema kwamba katika kabila lao wao mwanawe akioa, kwanza mkwewe lazima mama mkwe lazima aje alale na baba mkwe. Ndio, alisema kwamba yeye bahati nzuri mwanawe baada ya kwishakuoa kwanza ikabidi yule mke wa mwanawe akalale naye yeye akazaa naye mtoto mmoja, halafu tena ndio akamwambia haya kijana chukua mkeo sasa. Lakini kwanza ngoma lazima aianze baba. Huo ndio utamaduni wa Afrika na anatangaza kwenye redio anahojiwa moja kwa moja unamsikia. Huu ni utamaduni ambao ni wa kuweza kuuchukua sisi.

Kwa hivyo, ndio nikasema sio kila utamaduni wa Afrika wa kuweza kuuchukua. Kwa hivyo, mimi nadhani msisitizo uwe ni utamaduni wa Zanzibar. Kwa sababu hata huo wa Tanzania mwengine unaweza ukawa hatuuwezi tukaufuata ndani ya Tanzania, ukenda katika jamii yetu hii ya Tanzania. Kwa hivyo, kuna tamaduni nyengine kwetu sisi ni ngumu na huwezi kuzitangaza wala kuzionesha. Lakini kwa wenyewe ni kitu halali kabisa wala hakina mazonge.

Kwa mfano, Mhe. Spika, nimeona kitu mimi ambacho kinafanywa na kina uhalali wa kutosha kabisa, uhalali wa kiutamaduni yaani wa kimila. Kuna

wakati mmoja nilikwenda kufanya *research* katika kijiji cha Mdaula mwezi mmoja nilikaa pale na wenzangu. Kwa hivyo, ikawa pale kijijini pana harusi, wiki nzima ngoma usiku na mchana. Palikuwa na Msikiti mdogo tu hausaliwi wanaosali ni watu wawili tu, lakini ile mitungi ya pombe yote imewekwa pale kwenye baraza ya Msikiti basi watu ndio wanakaa na kupiga vitu. Nilikuwa na mwenzangu mmoja ni mtu wa Kiembesamaki hapa Unguja, sitaki kumtaja jina ni mtu wa dini sana, yale mambo yana muuma, lakini ndio utamaduni wa wenyewe pale ni kitu halali ambapo unaweza ukakitangaza kile kwenye redio na kuonesha kwenye televisheni kwa upande wa kule sio tatizo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tulikaa pale, akawa anatolewa nje mtoto mwari alikuwa anachezwa, baadae tukaona pandikizi la jari linatolewa nje, mwari katimia. Yule mwari kabebwa na mjomba yake, kwa mila zao pale wakati wa kutolewa nje kwenye ngoma watu wanachenza nje basi yule mjomba ndio anambeba yule mwari. Kwa hivyo, anambeba yule mjomba wanazunguka kwenye duara wanacheza halafu anamuweka katikati pale kafungwa kitambaa cheusi kichwani, halafu kapewa mkia wa ngombe ndio anacheza cheza. Halafu vijana wanakwenda pale wanamgusa, halafu wanawingwa kama mbwa, wee wee. Sasa ule ni utamaduni wa Kiafrika na ni utamaduni wa Kitanzania. Lakini huwezi kuutangaza wala kuuonesha katika vyombo vyetu vya habari.

Kwa hivyo, nadhani msisitizo ulikuwa ni utamaduni wa Zanzibar, tusitoe *loophole* katika sheria kama hizi. Kwa sababu sheria kama hii mtu ukishampa leseni hapa akaonesha mambo kama haya ninayoyatolea mfano, huwezi kumfunga kwa sababu sheria imetoa mwanya utamaduni wa Afrika ndivyo inavyozungumza, uoneshe mambo yanayokwenda sambamba na utamaduni wa Zanzibar na utamaduni wa Afrika. Kwa hivyo, kuonesha haya kuna ni sawa kisheria kiutamaduni atakuwa hayuko sawa, lakini hii sheria ndio imeshatoa *loophole* hiyo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nasema tuna kazi kubwa, lakini tume itabidi kwa kweli ijipange vizuri na isimamie vizuri.

Mhe. Spika, na mimi nije katika hii biashara ya vifaa vya utangazaji. Hili halimo katika mswada, lakini limo katika sheria hizi za vyombo vya habari. Mhe. Spika, jukumu hili nafikiri tumelipa mwaka jana au mwaka juzi, wizara hii kusimamia kudhibiti hivi vyombo vya utangazaji, vikiwemo TV, redio na vyombo vyengine vinavyohusiana na mambo ya utangazaji. Mhe. Spika, sijui wizara imetoa muongozo gani kwa wafanyabiashara mpaka hivi sasa. Labda Mhe. Waziri atatusaidia. Kwa sababu ukiangalia sasa hivi, pamoja na Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali, alikuwa anasisitiza vyombo hivi na baadaye vitamalizika, lakini hatuna haraka ya kuvizuia kwa sababu baada ya muda wa miaka saba vitakuwa vimemalizika *Ok* sawa.

Lakini sasa ukiangalia uingizaji wa TV chakavu, deki zile za zamani zimekuwa ni nyingi kupita kiasi. Kama utazichukua TV ziliomo madukani za mitumba pamoja na deki za televisheni, kila nyumba ya Zanzibar ukaipeleka deki moja basi deki nyengine zitakosa watu bado. Hivi ni vitu ambavyo vina sumu ndani ya nchi vimekuwa vingi kupita kiasi. Sasa huoni kwamba tutakuwa tunaifanya Zanzibar dampo la vitu vya hatari.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana na hoja yake kwamba hawawezi kuvizuia moja kwa moja. Sawa tusivizuie moja kwa moja. Lakini je, kuwa na udhibiti angalau ile idadi inayoingia ikapungua. Vipi unaweza ukadhibiti Mhe. Spika. Kwanza ni kuwadhibiti wafanyabiashara, maana nadhani katika nchi biashara inawekewa utaratibu si kila mtu tu anaweza kuchukua biashara yoyote. Sio kuwa mimi naweza kwenda Dubai nikaona nichukue hichi na hichi, nadhani biashara hiyo tunayo basi sasa hivi ibadilike. Tuwe na wafanyabiashara ambao wanatambulikana kuwa wanashughulika na biashara gani na hawa biashara gani, lakini kuwaachia tu kiholela holela mambo kama haya, siku moja nchi itakuwa ni dampo la vitu vibovu na itakuwa kwa kweli ni hatari. Mhe. Spika, ni lazima tufike pahala biashara kama hizi ziwe na udhibiti.

Mhe. Spika, Tukiangalia leo mafrigi na mafriza haya, hivi kweli yanalazwa nje, mbona Muzamil halazi nje yake na wala Suma, sijawahi kuona hata siku moja mafrigi na mafriza yamelazwa nje, ikiwa atayalaza nje basi hatoyakuta siku ya pili.

Lakini nina hakika yale yanayolazwa nje kama vile Kibanda Maiti pamoja na sehemu nyengine mitaani, hata ukapita usiku wa manane basi husimamishi gari yako na kukujia hamu kusema ulipakie moja, kwa sababu siyo.

Mhe. Spika, Muzamil pale wakati anapofunga hutia kufuli nyingi, Suma vile vile pamoja na mlinzi, lakini sehemu zile nyengine hata walinzi hakuna, kwa nini kama ni biashara. Kwa kweli ni masuala ya kujiuliza kama kweli ile mali, yaani ukute mafrigi au mafriza 10, 20, 50 mpaka 100 yamelazwa nje na hata mlinzi hayupo, maana yake nini, hii inaashiria ni *useless items*, ndio maana yake.Kwa hivyo, ndio ninasema hili nalo ni la Tume ya Utangazaji au vipi, lakini wizara ndio hii nadhani hakuna matatizo.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa kama nilivyozungumza kwamba marekebisho yenyewe ni madogo sana na nilishiriki katika kufanya hayo marekebisho.Kwa hiyo, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja *(Makofi)*.

Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kutuwezesha kushiriki katika mkutano wetu huu wa leo.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nikawa mchangiaji wa pili kuhusu marekebisho ya mswada huu wa Tume ya Utangazaji.

Mhe. Spika, marekebisho haya ambayo wenzetu wametuletea, kwa kweli ni muhimu na kama Mhe. Waziri alivyotuelezea katika mswada huu, kuwa madhumuni ya kufanya tume yende sambamba na mabadiliko au wakati. Nakusudia kuingiza mahitaji ya kisasa ya utangazaji ya *Digital* na kuondokana na ule mfumo wa zamani wa *Analogue*.

Kwa mnasaba huu ni dhahiri kwamba wenzetu hawa wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo wanakusudia kutuondosha hapa tulipo na kutupeleka katika eneo jengine la kisasa zaidi.

Kwa hivyo, mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni, tunakubaliana na mabadiliko haya yaliyofanywa na tunayaunga mkono. Kwa sababu ni mabadiliko muhimu na mambo ambayo kila wakati tumekuwa tukipiga kelele kwenye Baraza hili, kwamba tubadilike ili twende sambamba na wakati.

Mhe. Spika, tukizingatia zaidi kuwa wenzetu walioanza mwisho hivi sasa inaonekana wametutangulia mbele sana, lakini sisi tulioanza mwanzo kwa mujibu wa historia tunaonekana bado tunasuasua. Kwa kweli tunaamini kwamba mabadiliko haya ya sheria yataiwezesha Tume hii kuelekea kule ambako tunakuhitaji.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na wasaidizi wake wote akiwemo Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote wa wizara hii, kwa kazi zao nzuri wanazozifanya pamoja na matatizo mbali mbali wanayokabiliana nayo katika utekelezaji wa kazi zao.

Mhe. Spika, marekebisho yaliyofanywa si makubwa na kama mswada ulivyo si makubwa kwa maandishi, lakini ni makubwa kwa faida yake pamoja na yale yaliyokusudiwa.Lakini pamoja na marekebisho haya ambayo yanatakiwa kwenda na wakati, Mhe. Spika hivi sasa dunia inaiona kwamba sekta ya habari

kutokana na umuhimu wake kama ni muhimili wa nne, ukitoa ile mihimili mitatu ya dola. Kwa kweli wanaichukulia Sekta ya Habari ni muhimili wa nne kutokana na umuhimu wake.

Kwa sababu Sekta ya Habari au Vyombo vya Habari vinaweza kusaidia au kupotosha jamii. Hapo ndipo unapoonekana ule umuhimu wa jambo lenyewe.

Mhe. Spika, katika sehemu ya marekebisho ya mswada huu, kuna tafsiri moja kwenye tafsiri ambazo zimetolewa katika marekebisho haya ni hili neno linalotajwa hapa, kwamba neno utangazaji.

Kwa mujibu wa marekebisho haya imeelezwa kwamba maana ya utangazaji ni kutoa picha, sauti kwa njia ya habari na huduma na kunakili ilivyokusudiwa kwa ajili ya kutoa, kuburudisha na elimu kwa umma. Hivi ndivyo wenzetu walivyotutafsiria neno utangazaji.

Lakini mimi nitalichukulia zaidi hili neno elimu kwa umma. Mhe. Spika, hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefungua milango wazi kwa kuanzisha Vituo vya Habari Binafsi vikiwemo vya redio, televisheni na hata magazeti, ili viweze kusaidiana na vile vyombo vya serikali katika kutoa habari.

Kwa kweli zamani tulishuhudia kwamba hakukuwa na jambo hili na tulikuwa tumezoea tu, kuna magazeti ya serikali kama vile Ukweli Ukidhihiri Uongo Hujitenga, Zanzibar Leo, Sauti ya Tanzania Zanzibar, Televisheni Zanzibar. Kwa maana hiyo, ni vyombo ambavyo huwa vinatoa taarifa au habari mbali mbali pamoja na elimu kwa umma.

Baada ya serikali kuona kuna umuhimu kwa sekta binafsi sasa na wao kusaidia na serikali katika kufanya kazi hiyo, ndipo milango ilipofunguliwa na tunashukuru *alhamdullah* hivi sasa tunazo redio nyingi za binafsi ambazo zimefunguliwa. Isipokuwa sijapata kuona kituo cha Televisheni Binafsi kwa hapa kwetu, lakini redio kwa bahati nzuri zipo nyingi na zinatoa taarifa.

Kwa hivyo, hiyo ni hatua moja kubwa katika nchi yetu ambayo inakwenda na wakati.

Mhe. Spika, unapozungumzia elimu kwa umma, ambapo ndio dhana nzima ya utangazaji. Maana yake ama kusaidia jamii katika kuwaelimisha iwe kwa mazuri au matukio mabaya. Nadhani nimeeleweka.

Kwa sababu unapotoa elimu kwa umma si lazima uwe unatoa elimu kwa yale mambo mazuri tu yanayofanyika, hata kutoa taarifa za mambo mabaya ambayo

yanafanyika pia ni kuelimisha jamii. Kwa maana hiyo, hii ni kazi moja kubwa ya kutuunga pamoja na vyombo vya habari kwa jumla *(Makofi).*

Lakini inavyotakiwa taarifa zinazotolewa na vyombo hivi ziwe za aina zote mbili na jambo la msingi ziwe ni sahihi au matukio sahihi na wala sio ya kubuni ama kwa sababu nyengine ambazo pengine zinaweza kuleta mtafaruku katika nchi.

Mhe. Spika, mimi binafsi ninavipongeza sana vituo binafsi vya redio vya hapa Zanzibar. Kwa sababu ni miongoni mwa wasikilizaji wakubwa wa redio hizi za watu binafsi, kwa kweli wamekuwa wakisaidia sana jamii katika kutoa elimu za mambo yote mawili.

Kwa kweli wanajitahidi sana na ninawapongeza sana na wanasaidia sana. Kwa sababu vyombo vyao hivi vinaonekana vinakwenda na wakati, kwani ni vyombo ambavyo vinasikika katika maeneo ya mbali. Nathubutu kusema wakati mwengine kuliko hata vyombo vyetu vya serikali, yaani vina nguvu sana, kwa maana hiyo vinasaidia jamii na ninavipongeza sana.

Nadhani katika kutoa habari au elimu kwa jamii nafikiri baadhi ya maeneo kuna mipaka. Sasa sijui Sheria hii ya Tume inaeleza vipi na mimi sijapata kuisoma, kwa sababu tumepewa hapa leo asubuhi na kujaribu kuangalia kwa haraka na tulikuwa tukiangalia zaidi yale marekebisho ambayo yamewasilishwa.

Isipokuwa ninachoamini ni kwamba wakati tunapopitisha sheria na wala sio hii tu, bali ni sheria nyingi kuna kuwa na maeneo yenye mipaka. Mhe. Spika, mbali na redio hizi binafsi kutoa taarifa mbali mbali za nchi yetu pamoja na za nje katika kuelimisha jamii na kuwaeleza yale matukio ni mabaya yanayotendeka.

Lakini kuna jambo moja ambalo nataka nimuombe sana Mhe. Waziri kupita kwako Mhe. Spika, atupe ufafanuzi kwa sababu linaleta athari katika jamii, vile vile nataka kujua mipaka ya vyombo hivi iko vipi, kuhusu suala zima la kutangaza kwa kuandama kwa mwezi.

Mhe. Spika, redio zetu hizi kwa kweli baadhi ya wakati zimekuwa zikitoa taarifa za kuandama kwa mwezi wa Ramadhani, lakini taarifa zao zinakuwa zinawasumbua wananchi, yaani taarifa zao zinakuwa na utata na kuwachanganya wananchi sana.

Kwa sababu mwananchi anaposikia kwenye redio kwa mfano Zenji FM inatangaza mwezi umeandama, kwa hiyo kesho ni mwezi mosi Ramadhani.

Pengine taarifa zile zilizopelekwa pale sio sahihi, labda zimetangazwa kwa utashi wa jambo fulani, lakini mwananchi mwengine wa kawaida anakuwa hafahamu, isipokuwa yeye amesikia redio imetangaza na kusoma takbir na kusema kuwa mwezi umeonekana sehemu fulani pamoja na mambo mengine na wengine wanafuata *(Makofi)*.

Kwa hivyo, ndio maana niliposema kwamba ni lazima wananchi wajue mipaka ya vyombo hivi kuhusiana zaidi na masuala ya kitaifa, kwa sababu suala la kuandama kwa mwezi ni suala la kitaifa.

Nadhani vyombo vya watu binafsi viwe vinanukuu kuandama kwa mwezi kutoka vyombo vya serikali au serikalini na kuwatangazia wananchi. Lakini leo utasikia chombo cha habari binafsi kinatangaza moja kwa moja kwamba mwezi umeonekana sehemu fulani bila ya serikali kutangaza kuandama kwa mwezi ule. Suala hili linatupa matatizo katika jamii.

Mhe. Spika, ndio maana niliposema kwamba mipaka ya vyombo binafsi iko vipi au imepewa uhuru wa kutangaza tu, kwa kuwa ndio wanatangaza au katika masuala kama haya ya kitaifa yanapofika mipaka yao iko vipi. Kwa hivyo, ikiwa hakuna mipaka basi ni vyema kuwa na mipaka, kwa sababu tutawachanganya wananchi wetu na zaidi tukitilia maanani kwamba vyombo vyao hivi vinafika mbali zaidi.

Kwa mfano ninapokuwa Pemba kwenye kamati mara nyingi Sauti hii ya Tanzania Zanzibar haipatikani vizuri, basi huwa tunapata taarifa nyingi kutoka redio ya Zenji FM na nyengine kutoka Dar-es-Salaam ndio tunapata taarifa. Lakini yetu inakuwa na matatizo licha ya wakati huu kuwa tunakabiliwa na matatizo ya umeme, kwa kweli kabla ya matatizo ya umeme.

Kwa maana hiyo, inaonekana hizi redio binafsi zina nguvu zaidi.

Mhe. Spika, kuna haja ya kuviangalia vyombo vyetu vya habari vya serikali, yaani Televisheni Zanzibar na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Kwa nini nimesema hivyo, kwa sababu mara ya mwisho mwezi huu ulioandama, basi vyombo hivi vilikuwa havisikiki, ndio maana niliposema kwamba watu walipata taarifa katika vyombo vya habari binafsi kuhusu kuandama kwa mwezi.

Kwa bahati nzuri safari hii hakukuwa na matatizo na mambo yote yalikwenda sawa na wala hakuna wale waliotangulia mwanzo na wengine mwisho. Kwa kweli yale matangazo yao yalisaidia na wananchi wengi walipata habari kupitia vyombo hivi binafsi.

Mhe. Spika, wengine walikaa na kusubiri Sauti ya Tanzania Zanzibar pamoja na Televisheni Zanzibar, lakini kwa wakati ule vilikuwa havisikiki. Kwa hivyo, nasema ilikuwa ni heri kwani tulikwenda sambamba wananchi wote wa Zanzibar, yaani tulifunga na kufungua pamoja, kwa maana hiyo halikuleta utata. Isipokuwa tatizo linakuja pale ambapo kutakuwa na tofauti ya kimawazo pamoja na mtazamo.

Kwa kweli suala hili Mhe. Waziri nadhani atupe ufafanuzi zaidi kuhusu mamlaka ulipewa vyombo hivi katika kutangaza. Kwa sababu nadhani ni busara vyombo hivi vitusaidie kutangaza taarifa ambazo tayari zimeshatolewa na serikali, katika masuala kama haya ya kuandama kwa mwezi pamoja na mengine. Huu ni mfano tu, lakini ni kusambaza taarifa muhimu za serikali basi iwe ni jukumu la vyombo vya serikali kuliko vyombo vya binafsi.

Mhe. Spika, mbali na marekebisho ya sheria hii ambayo wenzetu wametuletea ambayo yanakusudia kwenda na wakati. Lakini marekebisho haya ni vyema yakenda sambamba na ubora wa vyombo vyetu. Kwa maana hiyo, ninaposema ubora wa vyombo vyetu ninamaanisha maslahi ya wafanyakazi wa vyombo hivi, majengo pamoja na vitendeakazi.

Kwa sababu vyombo hivi vya habari vina kabiliwa na changamoto nyingi sana. Kwa mfano utakapokwenda katika jengo la Televisheni Zanzibar ni aibu tupu, yaani huwezi kuamini kwamba televisheni ile ni ya taifa, kwa upande wa Sauti ya Tanzania Zanzibar hali ndio ile ile, yaani ni aibu tupu.

Kwa hivyo, tunapoelekea kwenye mabadiliko ya wakati basi tubadilike katika maeneo yote pamoja na hali ngumu ya maisha na kifedha lakini ni lazima serikali itoe kipaumbele kwa sekta hii kama ni muhimili wa nne. Kwa maana hiyo, itoe kipaumbele kwa watumishi wa kada hii ya habari, yaani maslahi mazuri ya wafanyakazi ili wapate moyo wa kufanyakazi.

Pamoja na hayo, tusiwe tunakwenda na mabadiliko ya kutoka kwenye *Analogue* kwenda *Digital*, lakini wafanyakazi wetu maslahi yao yako pale pale nadhani tutakuwa hatujafanya chochote. Kwa maana hiyo, mabadiliko haya yaende sambamba pamoja na kuyafanyia marekebisho *scheme of service* za wafanyakazi wetu, ili waendane na wakati, kwa sababu wenzetu Bara wametutangulia.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana utakuta watangazaji wetu wengi wazuri wanatoka hapa na kwenda Bara, hili tumekuwa tukilisema kila wakati na ndio kazi yetu kusema na kutaendelea kusema, kwamba maslahi ya wafanyakazi lazima yarekebishwe.

Kwa mfano leo unamkuta mpiga picha hapa tunashinda naye kutwa tokea asubuhi mpaka usiku anasimama pale na akiondoka anapewa shilingi elfu mbili, hivi kweli *reasonable* kiwango hicho cha shilingi elfu mbili. Mtumishi yule anakitumikia chombo hiki ambacho ni kikubwa Baraza la Wawakilishi, tokea asubuhi mpaka usiku anapewa shilingi elfu mbili na fedha hizo mpaka ahangaike adai.

Pengine tunaweza kumaliza kipindi chote hiki cha mkutano mzima na wala hawajapewa hata shilingi, yaani wanakuja na kurudi hata shilingi moja Mhe. Spika. Sasa sijui sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaweza hivyo, yaani tunaweza kuja hapa na kukaa mpaka tukaondoka hatujatia kitu chochote mfukoni litakwenda hili Baraza, basi litakuwa halendi. Kwa hivyo, na wenzetu hapa lazima tufike pahala tuwafikirie *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kuna kipindi fulani tuliwahi kutoa wazo hapa, kwamba hivi hakuna uwezekano wa wafanyakazi wa vyombo hivi, ambao wanatumikia chombo hiki na wao kuwekwa kwenye orodha ya wafanyakazi wa hapa kwa wakati wa kikao. Ninachokusudia kuhusu masuala ya maslahi wanayolipwa wafanyakazi wetu hapa, kwa sababu tunao watumishi wengine ambao wametoka sekta za nje ya Baraza, lakini maslahi yao yanatoka hapa.

Lakini hawa wenzetu wanahangaika kwa kututumikia pamoja na kutoa taarifa pamoja na elimu kwa jamii na matokeo yake kwa kweli hayapendezi. Kwa hivyo, ndio maana unakuta wakati mwengine hawapo au unaweza kuiona kamera ipo pale inazunguka ama taarifa hazitoki vizuri, kwa sababu hakuna ile ari au hamu ya kufanyakazi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Naibu Waziri muko pamoja. Kwa kweli Mhe. Waziri wa Fedha tuviangalia vyombo hivi pamoja na uhaba wa fedha, lakini vyombo hivi ni muhimu sana, kwa hiyo *ceiling* yako uiangalie na uwape kipaumbele pamoja na vyombo hivi vya habari likiwemo na Gazeti la Zanizbar Leo *(Makofi)*.

Kwa kweli Gazeti la Zanzibar Leo Mhe. Spika pamoja na kwamba halimo kwenye tume hii, lakini gazeti hili linafanyakazi vizuri sana na linahitaji kuwezeshwa pamoja na kwenda na wakati.

Sambamba na kubadilisha vyombo vyetu vya redio na televisheni, lakini tusisahau na Gazeti la Zanzibar leo nalo linahitaji kwenda na wakati. Kwa mfano hivi sasa gazeti letu bado linatumia zile picha za *black and white*, hivi kweli linakwenda na wakati.

Mhe. Spika, juzi tulishuhudia hapa wakati wa Sherehe za Mapinduzi gazeti la tarehe 11 na 12 ya Zanzibar Leo yalikuwa ya rangi na kila mmoja alipenda. Kwa kweli ni magazeti mazuri yaliyotoa taarifa nzuri na wananchi waliyapenda, lakini wanashindwa kufanya vile kutokana na ufinyu wa bajeti pamoja na matatizo mengine mbali mbali.

Gazeti la Zanzibar Leo tulifanya marekebisho ya sheria hapa na kulifanya kuwa shirika, lakini bajeti yake utaikuta ile ya wakati ule si shirika na sasa hivi ni shirika haina tofauti. Kwa kweli watashindwa kupiga hatua, na watashindwa kuleta mabadiliko katika gazeti lile kwani gazeti hilo ni muhimu kwa wananchi na taarifa zake mara zote zinakuwa ni za ukweli.

Kwa kweli Mhe. Spika, mimi mchango wangu ni huo namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha aliangalie sana Gazeti la Zanzibar Leo pamoja na vyombo hivi vya habari ili kuwawekea *ceiling*. Mhe. Spika, mimi naomba tuwape nyenzo ili tuwawezeshe waende na mabadiliko ya wakati huu, bila ya kufanya hivyo basi bado tutakuwa tunaimba hapa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia kidogo katika Mswada huu wa Tume ya Utangazaji. Mhe. Spika, mswada ni mfupi lakini malengo yake ni makubwa sana na muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Mimi niwapongeze wizara kwa kufikiria suala hili angalau hivi sasa, ingawa tumechelewa kidogo lakini angalau wamelifikiria hilo. Sisi leo tunafikiria kubadilisha sheria tuliyokuwa nayo Tume ya Utangazaji ili tuende sambamba na matarajio ya kuingia katika teknolojia mpya.

Nafikiria mwishoni mwa mwaka jana wenzetu wa Kenya nilikuwa nasikia wanafurahia kwamba wao tayari wameshafika, sasa ikiwa wenzetu hapo jirani tayari wao walisherehekea kuingia katika utaratibu huu, sisi leo ndio kwanza tunabadilisha vifungu vya sheria ili vituwezeshe hatimae kuingia huko. Mhe. Spika, nasema tumechelewa lakini angalau na sisi tumetanabahi na kujaribu kwenda huko, si hatua mbaya bali ni hatua nzuri.

Mhe. Spika, katika suala hili bahati nzuri wizara ina miliki mambo mawili. Kwanza hii tume inamilikiwa na wizara halafu ina vyombo ambavyo vinatoa matangazo. Kwa hivyo, tunapochangia huwa tunaifanya *assessment* ya wizara kama mmiliki wa tume lakini pia tunaviangalia vyombo vyake katika *performance* yake kwa jumla. Hili ni jambo muhimu kwa sababu yenyewe ina tume lakini pia ina vyombo ambavyo inavimiliki. Mhe. Spika, ingelikuwa haina vyombo ambavyo inavimiliki tungaliiangalia tume katika kuvisimamia

vyombo binafsi, lakini bahati nzuri tunaiangalia wizara kama mmiliki wa Tume ya Utangazaji lakini pia *performance* yake katika vyombo vyenyewe. Hasa hapa ndio tuna tatizo kidogo.

Mhe. Spika, kwanza niende katika mswada wenyewe katika kifungu cha 4 kinasema sehemu ya 4 inaondolewa ya mswada huu ambao tumepewa hivi asubuhi kama Mhe. Salmin Awadh Salmin alivyozungumza. Ukiangalia katika mswada kifungu hicho ambacho kinaondolewa Mhe. Spika, kina majukumu ya waziri ambayo yako kifungu (a), (b), (c) na (d) na pia kuna kifungu cha 2(a) na (b) ambayo ni majukumu makubwa sana.

Mhe. Spika, mimi nilitaka kujua kwa nini tukaondoa majukumu haya ya waziri katika mswada huu na pia majukumu haya yatatekelezwa na chombo kipi badala yake. Kwa sababu hatukuambiwa kwamba kinakuwa *repelled* lakini badala yake kitasimamiwa na chombo gani? Vile vile, tumeambiwa madhumuni yake ni kuingia *the proposed amendment intend to change the analogue system*. Mimi nilikuwa najiuliza kwamba kumuondolea waziri majukumu kama kifungu cha 4 kinavyopendekeza, vinasaidia nini kuingia katika mkondo huu wa *digital* au kama bado majukumu yataendelea kama yalivyo yatakuwa ni kikwazo namna gani. Hayo mimi naomba kuelimishwa.

Mhe. Spika, suala la pili ni kifungu cha 5(c) hapo panafanywa mabadiliko ambapo kabla hiki kilikuwa kinapendekeza kwamba kuwe na Wajumbe wasiozidi wanne ambao watachaguliwa na waziri. Lakini kipengele ambacho kipo na kinafutwa kuna *not less than four not more than eight are the member appointed by minister*. Pia, hapa nilikuwa nataka kuelewa mapendekezo haya nayo yana maana gani.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo ni zuri na nalipongeza ni kuekewa vigezo vya *Executive Secretary* wa Kamisheni. Hapo mwanzo katika mswada huu alikuwa anateuliwa tu, lakini katika marekebisho haya yameekewa sifa zake ili kuteuliwa, hili ni jambo zuri kwamba mtu ambaye atakuwa na nafasi hii awe ni mtu mwenye maarifa na elimu, ana uzoefu hili ni jambo zuri.

Mhe. Spika, ni bahati mbaya kwamba mwenyekiti hakuwa na sifa hapo kabla lakini katika marekebisho haya hakuekewa sifa. Kwa hivyo, Mhe. Rais ni mtu wa hekima kubwa, lakini ni vizuri kumsaidia kama ambavyo tumemsaidia kwa Katibu Mtendaji wakati mwengine marais wetu wana hekima nyingi na shughuli nyingi kwa hivyo tusipowasaidia kuwawekea vigezo kama ambavyo tumeweka vigezo kwa Katibu Mtendaji hivyo anaweza akachaguwa mwenyekiti kwa hekima zake lakini akawa taaluma yake, uzoefu wake, busara zake sio kubwa na hivyo huyumbisha utendaji wa chombo hiki muhimu.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri kwamba mwenyekiti, aekewe sifa za kitaaluma na kiuzoefu ili tupate mtu ambaye atakuwa ameiva na atakuwa mtu ambaye anaweza kuhakikisha kwamba tume yetu inaongozwa vizuri.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo naomba nipatiwe maelezo ni marekebisho ya kifungu cha 9 katika marekebisho hayo ya kifungu hicho ukurasa wa 9 sheria ambayo inaletwa kurekebishwa naomba ninukuu. *"The chairman shall be head and supervisor of the day to day activities on the Commission and shall preside the meeting of the commission".* Katika marekebisho ambayo yameletwa ni kwamba sasa amepunguziwa mamlaka ile *day to day* yameondolewa yeye ni mtu wa vikao tu. Kwa hivyo, ningeomba kuelimishwa kwa nini majukumu yake yakaondolewa na kwa marekebisho haya sasa majukumu yake hayahitajiki tena au amepewa nani kuyasimamia.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo naomba maelezo ni kifungu cha 12 (b) ambapo *a company registered Zanzibar at least 20% of whose share holding is beneficially owned by Zanzibar Government.* Sasa marekebisho ambayo yanafanywa ni kwamba asilimia 51 za *share* zimilikiwe na Wazanzibari. Kabla ya hapo zilikuwa ni asilimia 20, mimi najiuliza kwamba nini sababu ya marekebisho haya.

Mimi nadhani kwamba hali yetu ya uchumi haijawa nzuri kwamba Wazanzibari sasa *economical* wako juu kiasi ya kwamba sharti la kuongeza asilimia ya ubia iongezwe. Mimi hapo nahisi hali kidogo ni ngumu zaidi kuiondoa kutoka 20 kuipeleka 51 nina wasi wasi wa kupunguza uwezekano wa kupata *registration* ya makampuni haya hapa Zanzibar. Mimi ningeshauri kwamba ingewekwa pale pale 20 kwa hali ya uchumi ilivyo.

Mhe. Spika, wakati nasoma hii sheria ambayo tumepewa hivi asubuhi katika ukurasa wa 11 nimeona jambo ambalo hili nahisi liangaliwe katika marekebisho haya kwa sababu kwa maoni yangu linaweza kuwa kikwazo cha mambo mengi. Mhe. Spika, ukurasa wa 11 wa sheria kifungu cha 12(4) naomba kunukuu. *"The Commission under any circumstances shall not permit any person to have both radio and television station at a time especial to be granted only one of them".*

Mimi sijui ni kwa maana gani hiki kifungu kikawekwa labda wakati huo kilikuwa na maana, lakini nafikiri kwa hali ilivyo sasa ikiwa mwananchi ana uwezo wa kumiliki redio, televisheni na gazeti ningeshauri kwamba kifungu hiki kingebadilishwa ili tume yetu ikawa na uwezo wa kutoa leseni kwa wananchi wetu ili wakasaidia kutoa taaluma na mambo mengine ili kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, kitu chengine ambacho naomba nikitilie mkazo kidogo ni kuhusu suala la maadili. Hili ni jambo la maana sana kuona kwamba vyombo ambavyo vinapewa leseni vinahakikisha kwamba maadili ya nchi yetu yanatunzwa isiwe sababu mtu ana redio yake au televisheni yake akachangia kwa njia moja au nyengine katika upotoshaji wa maadili ya nchi yetu. Mhe. Spika, bahati nzuri kifungu cha 15 (3c) cha sheria hii ambayo tunayo sasa kimeeleza vizuri sana kama kinavyosema. *To encourage the development of Zanzibar and Zanzibaris expression by providing a wide range programming that reflects Zanzibar opinions, ideas, values and artistic creativitiy by the displaying Zanzibar cultures and entertainment program.*

Hili ni jambo muhimu kwa vyovyote vile tume ina wajibu wa kuhakikisha kwamba kifungu hiki wanakisimamia vizuri sana, pamoja na uchakavu wa mitambo wa Redio Zanzibar na Televisheni Zanzibar, lakini kwa kiasi kikubwa hili wanajaribu kuli-*observe* pamoja na kwamba televisheni yao haina vifaa vya kileo, redio Zanzibar kusema kwake ni matata matata lakini bado pamoja na hayo yanajaribu kuhakikisha kwamba maadili ya nchi yetu kwa kiwango kikubwa yanatunzwa. Kuna wakati wanateleza teleza na ukiwaambia basi wanajirekebisha lakini kwa kweli lazima wapewe nafasi yao kwani wanajitahidi.

Mhe. Spika, kuna vyombo ambavyo vinapewa leseni na Tume yetu ya Utangazaji halafu vinaachiwa tu vinakwenda ovyo. Mhe. Spika, bosi wangu hapa Mhe. Haji Faki Shaali ameisifu sana Zenj FM na mimi katika baadhi ya mambo nakubaliana naye nawasifu sana kwani wanajitahidi sana, wanafanya kazi vizuri sana. Mhe. Spika, lakini katika suala hili la maadili wanahitaji kusimamiwa kidogo na wakiachiwa wanaweza wakatufikisha pabaya. Kwa hivyo, yeyote aliyekuwa mwenyewe lazima Mhe. Waziri awe mkali katika hili aone kwamba *value* na *culture* ya Zanzibar inakuwa *preserved* na chombo hiki.

Mhe. Spika, mimi ni msikilizaji wa Zenj FM lakini si mara moja si mara mbili ni kwamba redio Zanzibar haiwezi hata siku moja kutangaza *condom*, sasa ikiwa redio ya nchi haiwezi wala hairuhusiwi kutangaza *condom* haiwezekani kwa redio nyengine ya binafsi hata ikiwa mwenyewe ni nani ikaruhusiwa kutangaza *condom*. Mhe. Spika, ni lazima nchi iwe na *value* zake ambazo ziwe *presereved* zisiachiwe kumong'onyolewa hapo, tukiacha watu wakianza kuzimong'onyoa kweli *erosion* hii itatufikisha pabaya.

Mhe. Spika, kama alivyosema mwenzangu hapa kuhusu pombe, pombe katika vyombo vyetu si televisheni si redio Zanzibar hivi ni vyombo vya nchi haviruhusiwi kutangaza mambo hayo. Ndio maana kama mwenzangu mmoja alivyosema ni kwamba tumeacha pesa nyingi kupitia matangazo ya ufadhili wa pombe, leo iweje Zenj FM iruhusiwe kutangaza pombe. Mhe. Spika, ni

kwamba waache walevi watakaolewa walewe siri siri, lakini tusiporomowe *culture* ya ulevi katika nchi au tuwaache wazinifu watakavyozini wazini siri siri lakini tusi-*promote* mambo haya katika nchi.

Hili ni jambo ambalo tume hii inapaswa kulisimamia na ni jukumu lao kuona kwamba hii tabia kama chombo kinakiuka maadili kwa mujibu wa kifungu hiki cha 15 (3c) wana wajibu wa kuwaita na kuwaambia waingie katika sheria. Mhe. Spika, mambo mengine wanafanya kazi vizuri lakini katika hili lazima waone kwamba wana wajibu wa kuhakikisha kwamba maadili na *culture* ya Zanzibar wanafanya kama vile redio za taifa zinafanya.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo niliseme ni kwamba Mhe. Haji Faki Shaali alizungumza masuala ya *redio active decay* hili ni muhimu na wenzetu wa Kenya wana kitengo maalum kinachoshughulikia masuala haya. Sasa sijui kama niko ndani ya wajibu wa tume hii au ndani ya wizara hii, lakini serikali haiwezi kuliachia suala hili tukawa hatuna udhibiti nalo, mambo haya taathira kubwa ya mazingira na yanaweza yakatufikisha pahala ambapo siku moja hatukutarajia.

Kwa hivyo, ningeshauri Mhe. Waziri yeye angeliangalia uwezekano wa namna gani wenzetu wameshapiga hatua katika kuangalia kwamba dhana hizi za *electronic* ambazo zimechakaa zinatafutiwa utaratibu wa kuwa zisiingie tu katika majaa, mashamba na majalala kwa kweli bila ya kudhibiti masuala haya basi yanaweza yakatufikisha katika mambo makubwa ya mazingira.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni kwamba suala hili la Tume ya Utangazaji inahusiana na leseni ya minara na mambo mengine. Bahati mbaya au nzuri Tume ya Mawasiliano nayo inashughulikia pia na utoaji wa leseni ya minara na mambo mengine yanayohusiana na mambo haya ya *telecommunication* ama iwe ya habari au ya simu.

Mimi ningetaka kujua katika masuala haya ambayo yanatolewa hapa Zanzibar hasa ya minara ya mawasiliano ya simu waziri analiambia nini Baraza katika suala hili kuona kwamba fedha ile inayopatikana pale hatimae hazina ya Zanzibar inafaidika au ndio kwa sababu iko chini ya Tume ile ya Bara yeye kama waziri wa utangazaji hana namna ya kuona kwamba fedha ile inaingia katika mfuko wetu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa sina mchango mkubwa kwa sababu mswada wenyewe ni mfupi sana na kwa hayo machache kama alivyosema Mheshimiwa mwenzangu na mimi namfuata naunga mkono mswada huu.

Mhe. Spika: Mhe. Saidi Ali Mbarouk, nakushukuru hasa pale uliposema kwamba wale wanaolewa walewe kwa siri na wale wenye habari nyengine pia wafanye kwa siri sio kwa kificho. Nakushukuru sana.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kutoa maoni na mchango wangu japokuwa pengine hautakuwa mrefu kuhusiana na suala hili la marekebisho ya Sheria ya Tume ya Utangazaji ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kama wenzangu walivyotangulia kuchangia kwamba mswada wenyewe ni mdogo sana kwa hiyo nao pia unatufanya tuwe na maneno machache, lakini tutajitahidi kuweka michangio ya hapa na pale ili iweze kufahamika.

Mhe. Spika, nataka nianze kwenye suala zima la mswada huu sio mambo makubwa sana lakini ningependa kupata kuelewa zaidi wala sio jambo muhimu sana, ni suala la lugha tu. Mhe. Spika, katika kifungu cha 5 na kifungu cha 10 kuna neno limeandikwa kuondosha *paragraph* na kuweka *paragraph* mpya. Sasa sijui neno hili ni Kiswahili au tungepata neno ambalo linafanana na hapo.

Mhe. Spika, pia nataka niungane mkono na Mhe. Waziri Kivuli pale aliposema katika kifungu cha 6(b) ambacho kimerekebishwa badala ya kusema muda wa kusita kwa Mjumbe lakini limesahauliwa suala zima la ugonjwa au kifo. Kwa hivyo, tungeomba na hayo yawe miongoni mwa sababu za kusita kwa Mjumbe.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la utoaji wa leseni wameshatangulia wenzangu kuzungumza lakini na mimi ningesema kidogo kama Mnadhimu wangu alivyozungumza hapa kwamba sisi wanapokuja watu kwetu kupata leseni tunakuwa hatuna hiana, tunawapa. Lakini sisi tunapokwenda kutaka kule kwao huwa wanatunyima. Mimi nadhani ikiwa sisi tunaweza kunyimwa hivi kuna ubaya gani na sisi kuwakosesha wengine na hasa kwa kuwa tuna sababu za kutosha ni kwamba suala zima la maadili bado ni mtihani katika redio zetu pamoja na sifa nyingi tutakazowapa kwa kazi zao wanazozifanya, bado masuala ya maadili yanakiukwa kwa hali ya juu.

Sijui ni kwa sababu ya huo utandawazi wa kutoka kwenye *analogue* na kwenda kwenye *digital*. Lakini nadhani kuna masuala ambayo kama Zanzibar lazima tuyaangalie kitamaduni zetu na ndio tunapozungumza kuwa sio kwa maana ya utamaduni wa Kitanzania ata sisi hatuko huko. Mhe. Mnadhimu amezungumza mengi hapa na ametoa mifano lakini mimi nitatoa mifano miwili midogo ambayo kwa hapa kwetu itakuwa ni ajabu kuambiwa kwa mwanamke anapelekwa kutahiriwa. Ndio au mwanamke amefiliwa na mumewe shemegi zake anachaguliwa mmoja kurithi. Kwa hivyo, tunatofautiana sana tunapovuka

tu bahari kwenda upande mwengine. Sasa ni lazima maadili ya kizanzibari kwa asilimia mia moja yawe yanazingatiwa katika suala zima la utoaji wa leseni na sipingi kama alivyozungumza Mhe. Said Ali Mbarouk kwamba hakuna haja au ulazima wa kwamba mtu akishapewa leseni ya kufungua redio asipewe na kufanya kitu kingine. Ikiwa anao uwezo na ametimiza masharti mimi nadhani tumuachie afanye kwa mujibu wa uwezo wake, lakini chini ya udhibiti wetu.

Mhe. Spika, ninaposema udhibiti wetu haya masuala kama waswahili wanavyosema, “kama kitanda hujakilalia hukijui kunguni wake wanatafuna vipi”. Au mvaaji wa kiatu pengine yeye ndiye anayejua kinambana wapi. Sasa Mhe. Spika, unapokuwa ni mwanachama wa kusikiliza hizi redio unakumbana na vitu vingi ambavyo mimi ningeiomba sana Tume ivishughulikie kwa nguvu zake zote.

Hili Mhe. Spika, pengine labda linatokana na pale alipozungumza Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii kwamba watu wana kawaida ya kuvidharau vyombo vyetu hususan televisheni ya Zanzibar na redio yetu. Pengine ni kwa sababu ya haya maadili kwa upande mmoja, ingawa kwa upande wa pili tunayo matatizo yetu ambayo itabidi tujirekebishe kama ni kupitia Tume au Wizara inayohusika iyaone masuala haya.

Mhe. Spika, masuala yenyewe kwanza ni lazima unapotaka kujirekebisha ni lazima ujijue pale ulipo, unapotoka na unakotaka kwenda. Sasa nadhani Tume ya Utangazaji ina wajibu wa kujua hasa historia nzima ya Zanzibar kuhusiana na masuala haya na tunakwenda nayo vipi mpaka tena ikawa panazungumzwa kuwa sisi tumetangulia wengine wametufuata nyuma lakini wanatupita, hebu tutizame kitu gani kimetufanya hivi. Hilo ni suala la kuona namna gani tunashughulikia.

Mhe. Spika, suala la televisheni kila mtu na wengi watanikubalia hivyo kwamba sisi Zanzibar ndio tulikuwa wa kwanza katika Bara la Afrika hasa kusini mwa jangwa kumiliki televisheni ya rangi ambayo aliianzisha Mzee wetu Mhe. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na ilianza rasmi mwaka 1973. Sasa tutizame tangu mwaka huo mpaka leo tunafanya nini, sijui kama hao watu wa televisheni wenyewe wanayo hiyo sherehe hasa ya kuanzishwa kwa kila kitu, sijui sitaki niwasemee. Lakini kama haipo wanatwambia nini?

Sasa tukianza kufanya dharau sisi wenyewe unaambiwa mzazi, mtoto anatizama kisogo cha mzazi wake, sasa usitegemee kama wewe utafanya manyago yako halafu huyu mtoto ataweza kwenda vizuri, atakutizama wewe unavyofanya na yeye atafanya pengine kuliko vile kwa sababu waswahili wanasema mrithi huzidi. Kwa hivyo, ni lazima tutazame makosa yetu wapi tumekosea, turekebishe vipi, tufanye vipi na ushauri pia tusiukatae.

Jengine ni suala zima la hizi fani, fani kama ya utangazaji. Enzi za Mhe. Najma Halfan na wenzake ilikuwa mtu anasoma habari unapenda kumsikia na sijui kwa sababu nilikuwa sijawa na akili nzuri sana pengine bado mdogo sikuwa na uwezo wa kuchambua, lakini nilikuwa sifiki pahala nikaweza kutoa dosari ya neno fulani lililozungumzwa au jinsi lilivyotamkwa.

Mhe. Spika, *Zenji FM* pamoja na sifa zote tunazowapa, matatizo yao ni vyema tuwaambie lakini Tume ndio iwe msimamizi mkubwa wa haya matatizo. Kwa sababu hata kama chombo kile si cha serikali lakini bado kipo Zanzibar kwa mtu mwengine yeyote wa ndani ya Zanzibar au nje basi atahesabu kwamba hiyo ndio Zanzibar ni chombo chao hicho, kuwa hawajui hata kutamka jina la nchi. Hili nina ushahidi, ni jana tu walikuwa wanatangazia suala zima la mafuriko na tetemeko yaliotokezea HAITI, lakini wanashindwa, sijui ni pozi nyingi lakini mimi sisemi pozi hawajui.

HAITI mtangazaji anasema Hait, sasa sijui kama kuna mtu atakua na *interest* ya kukaa kusikiliza vitu kama hivi, mwisho atabaki kungojea vile vionjo tu vilivyobaki pale, jaje lahe na mambo mengine, lakini ile mantiki ya kwamba vyombo hivi maana yake ni kutupasha habari kwa yanayopita nje na bahati nzuri au mbaya katika kipindi hiki ambacho tuko katika mpito wa kuwa hatuna umeme una hamu ya kusikiliza kinachotokea nje huko duniani basi unakwenda kukuta vitu vya ajabu ajabu na machofu uliyokuwanayo unakuwa unashindwa kuona umuhimu wa vitu vyengine, inakuwa labda vitu vile viko pale kama *toys.*

Sasa hapa nataka nipanue ile mada ya maadili, maadili sio tu kutazama utamaduni wa mambo kama inavyozungumzwa kutangaza *condom* na vitu kama hivyo visivyohusu vya ulevi na kadhalika, lakini hata ile *tone*, matamshi, ladha za maneno zinavyozungumzwa Mhe. Spika, kuna haja ya kutosha kuwaelimisha vijana wetu ili tunapokaa ikiwa ni sisi wenyewe au wale ambao watakuwa wanasikiliza hizo habari basi waweze kupata kitu ambacho kinaingia akilini, anaelewa kwamba sasa imetajwa London ni London, imetajwa Zanzibar ni Zanzibar. Siku hizi watu hata kuitamka hii Zanzibar hawajui, mtu badala ya kusema Zanzibar anasema Zanzibaa, anamalizia baa. Sasa mimi nadhani hii inatupeleka kubaya.

Kwa hivyo, ni vyema kwa vyombo vyetu vya serikali lakini hata kwa vyombo vya watu binafsi basi tuhakikishe kwamba watu wanaokaa kufanya hii shughuli wanaifanya kwa mujibu wa inavyotakiwa kimatamshi, kimaadili, lugha, zisichukuliwe tu lugha za mitaani ikawa zimo kwenye vyombo vya habari kidogo zinatushushia hadhi ya lugha yetu ya Kiswahili ambayo tunajivunia. Na mimi bado nitaendelea kusema kwamba Kiswahili ni utamaduni wa Zanzibar na ni lugha yetu zaidi kuliko kusema ni lugha ya Tanzania.

Mhe. Spika, Watanzania wana lugha zao, pengine ya kwanza, ya pili, Kiswahili ni ya tatu au kwa kupendelewa ni ya pili, lakini kuna wengi wanaifanya ni ya tatu kwa sababu baada ya lugha ya kijijini kwake lugha inayofuata ni ya Kiingereza halafu ndio anazungumza Kiswahili na ushahidi tunao. Kama Watanzania wanakaa pahala pamoja wanazungumza wenyewe kwa wenyewe masuala ya ndani ya nchi lakini bado unamkuta baba wa Kikerewe au Kisukuma anamwaga Kiingereza kama vile anatoka Ulaya. Sasa hii inaashiria kwamba Kiswahili si lugha yao.

Kwa hivyo, bado nataka niseme kwamba najivunia kama Zanzibar kuwa sisi ndio Waswahili na Kiswahili ni chetu na ni utamaduni wetu ni lazima tuutukuze na tuuenzi na tusiwape fursa wengine kuharibu kupitia hivi vyombo vyao ambavyo wanavifanyia kazi. Pamoja na kwamba asilimia 51 tunasema iwe yetu lakini ni lazima tuone jinsi gani tunasimamia maadili kuanzia ya lugha, matamshi na mambo mengine yanayohusiana na utamaduni wetu kama ambavyo upo usiharibiwe na vizazi vyetu viweze kuja kurithi.

Mhe. Spika, nakubaliana sana kwamba kuna haja ya kwenda na wakati sasa na kweli katika karne hii ya 21 utakapobakia nyuma sijui nani atakuelewa, vyenginevyo utakuwa unasindikiza watu tu popote pale unapokwenda ikiwa hukuwa pamoja na watu katika kuji-*tune* kutoka katika utamaduni mmoja kwenda wa pili. Sasa hili Mhe. Spika, isiwe tunalizungumza kwa maneno tu, kwa sababu pamoja na kwamba haya ni maendeleo lakini maendeleo yanaathari zake kimazingira, kimaadili wakati mwengine ikiwa wenyewe hamko makini na kitamaduni.

Sasa katika hili Mhe. Spika, naomba sana na wenzangu wamelizungumza hapa kwa kumalizia malizia kwamba, kuna suala zima la vitu ambavyo ni *radio active.* Wenzetu ambao wametangulia katika kufanya haya masuala ya mabadiliko na sisi ndio tuko nyuma tunajikongoja wamewahi kufanya kwamba haya maeneo yetu sisi ndio dampo, nina ushahidi yamesemwa hapa, yanalala mafriji nje hakuna anayeuliza lakini Suma kwake anakomea kwa *remote*. Sababu ni hiyo kwamba yale mengine hayana maana, lakini haitoshi tu kwamba hayana maana, itakapofika kwamba sasa haya ni taka tunataka kutupa wenzetu ndio wameshatutupia, sasa na sisi tutataka kutupa shughuli ndio iko hapo Mhe. Spika.

Nimeshawahi kusema nafikiri hapa hapa ndani ya Baraza sijui kama ilikuwa ni semina au katika kikao lakini naomba na leo kwa ruhusa yako Mhe. Spika, nilirudie.

Mwaka 2002 nilikuwa Uingereza nikaona kuna kesi baina ya wananchi na serikali yao kulingana na kwamba miaka ya nyuma ilikuwa hilo eneo ambalo wao wanaishi lilikuwa halikaliwi na lilikuwa likitupwa hivyo vitu.

Kwa sababu wenzetu mambo hayo wameanza zamani. Sasa katika miaka ya sasa hivi kuna athari ambazo situ za kimazingira kama tunavyoona sisi, lakini wao wanapata athari kubwa zaidi kwamba ile kuwa wako karibu na maeneo yale na pengine katika maeneo hayo wengine wamekaribia kujenga karibu karibu inawezekana hivyo. Athari yake imekwenda mpaka katika uzazi na imeonesha picha pale ya watoto kiasi wanane mpaka kumi wote wako aina moja kike na kiume, wana athari mkono wao wa kushoto kama sikosei wana vidole vitatu, yaani hauko wa kawaida kama sisi tuliokuwa na vidole vitano, naambiwa kama bata.

Hiyo inatokana na athari ya kwamba hilo eneo lilikuwa ni eneo lililokuwa likitupwa vitu vya aina hiyo kwa muda mrefu na kwa sababu ya pahali popote duniani kama tunavyoelewa *population* inakua watu wanaendelea kujenga majengo sehemu mbali mbali ambazo zamani zilikuwa hazikaliwi sasa hivi wanakaa kama ambavyo sisi tunakaa, maeneo ya majaa pia imekuwa sisi tunajenga majumba. Sasa hiyo imepelekea katika eneo lile watoto wanaozaliwa wote wana matatizo kidogo wako kama taahira na wana hiyo athari ya kimaumbile katika miili yao. Sasa kesi ambayo wale wazee wana-*claim* kulipwa kutoka serikalini.

Sasa lile ndilo linalonishughulisha mimi hapa kwetu baadae itakuwaje. Kwa sababu ikiwa eneo kubwa kama Uingereza kule imefikia hivyo sisi ambao tuko hapo na hapo, jaa liko chini ya dirisha au wanaouza hayo mafriji ndio nyumba ya jirani sijui tutakuwa tunayatupa wapi na tutafanya vipi mpaka athari kwetu iwe ndogo. Nina wasi wasi hiyo athari ambayo watoto wale wa Kiingereza wanayo sisi watoto wetu watakuwaje, naogopa kwamba wetu sisi wasije wakakosa sehemu kubwa ya viungo katika miili yao na sijui watakuwa wamekaa vipi kimaumbile na Audhubi llahi Mindhalika, lakini ni vitu ambavyo mwenzio akinyolewa wewe utie maji.

Hii ni changamoto kubwa ambayo kama wizara lakini kama nchi pia inatukabili kuona jinsi gani tunajipanga kulifanya hili. Kwa sababu bahati mbaya sana kwamba tumejiachia. Mimi nasema tumejiachia kuruhusu vitu vingi kwa idadi kubwa sana na bado vinaingia, pamoja na kwamba vipo vingi imesemwa hapa kwamba zitagawiwa hizo *DVD* zilizopo huko kila nyumba basi kuna zitazobakia hazina mtu na bado zinaingia. Sasa sijui utupaji wake utakwenda kivipi mpaka tunusurike iwe salama. Nina wasi wasi baadae viumbe watakaokuja kuzaliwa miaka 50 ijayo kama si mbali watakuwa wana *shape* zipi sijui ambazo zitakuwa haziko za kawaida.

Mhe. Spika, sasa hili ni suala ambalo napenda nimalizie lakini niliache kwamba ni changamoto kwa wizara na tume nzima kuona jinsi gani kuanzia sasa wanaweza kujipanga au kutafuta namna ya kuweza kwenda kutupa hivi vitu ambavyo vina athari kubwa si ya kimazingira tu bali ndani ya maumbile ya mtu, binadamu husika. Nakushukuru Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza. Mhe. Spika, mswada nimeuangalia na kwa kweli umezingatia mambo mengi muhimu, lakini mimi ningependa kuchangia mambo haya yafuatayo:

Jambo la kusikitisha ni kwamba mambo mengi sana ya kihistoria ya kimaendeleo yameanza Zanzibar, lakini kwa bahati mbaya huwa kama tunaanza wenzetu ndio wanaendeleza. Kwa hivyo, suala la redio na televisheni, sio televisheni peke yake hata redio vile vile Zanzibar ilikuwa ikisikilikana mpaka watu wa Mombasa walikuwa wanahusudu redio ya Zanzibar namna gani watangazaji walivyokuwa na lugha fasaha ya kuzungumza na vile vipindi vyake vilivyokuwa vikizungumzwa.

Vile vile, televisheni ya Zanzibar ilianza mwanzo na kwa kweli ilikuwa katika Afrika ya Mashariki tulikuwa na sifa nzuri sana. Kihistoria mambo mengi Zanzibar yameanza, umeme, dini, kila kitu Zanzibar kimeanza mwanzo wenzetu wakaendeleza.

Mhe. Spika, la kusikitisha ni kuona kwamba mfano wa Tanzania wameanza mambo ya leseni za *private television* hata za *government,* miaka kidogo tu iliyopita sio miaka mingi, lakini wenzetu wameshaendelea sana utakuta watu wengi wanapenda kufungua televisheni za Tanzania Bara kuliko televisheni yetu au redio za kule kuliko zetu sisi. Sasa tukiangalia vile viwango vya huduma kwetu sisi kila siku vinazidi kushuka kule vinapanda na ndio maana kila siku wateja wanaangalia zaidi televisheni za Tanzania Bara kuliko za nchini mwetu.

Kwa hivyo, sasa ni wakati ambao ni aibu mfanyabiashara kutoka Unguja akenda akitangaza biashara yake kupitia televisheni ya Dar es Salaam, lakini anaangalia ni *viewers* wangapi wanaangalia ili yeye aweze kwenda kutangaza biashara yake. Ikiwa TVZ *viewers* ni wachache sana basi atakwenda katika televisheni ambayo inapendwa au inaangaliwa sana. Hata gazeti vile vile anaangalia ni gazeti gani lina wasomaji wengi zaidi ndio anapeleka matangazo yake.

Mimi ningeomba kwamba licha ya kuwa tuna uwezo mdogo, licha ya kuwa televisheni yetu ni kongwe sana, lakini iko haja ya kufikiria njia gani ya kuweza kuboresha TVZ na STZ ili ziweze kuwa katika ushindani na kuwavutia zaidi Wazanzibari na nchi jirani kuweza kutumia kutangazia katika televisheni hizo ili zipate mapato zaidi, lakini vile vile ziwe na mvuto wa aina yake.

Mhe. Spika, tukiangalia katika sheria mama kwenye kifungu cha 12 ambacho kimerekebishwa, mimi labda nipongeze sana, kwa sababu hii sheria ilipotungwa pale mwanzo ilikuwa *very probity*. Kwa mfano ukiangalia kifungu cha 12(b) *"A company registered in Zanzibar at least 20% of whose share holding is beneficially owned by Zanzibar Government"*. Hiki kinaondoka. Kwa hivyo, hii ni *step for word* kwamba sasa hivi inakuja sheria inabadilishwa inatengua hiyo ya kifungu (b) na (c) serikali kujitoa katika *share* ya hiyo *broad casting.*

Lakini basi, kama alivyosema ndugu yangu Mhe. Said Ali Mbarouk kwamba Wazanzibari uwezo wao ni mdogo, sasa humu katika sheria imewekwa Mzanzibari. Mimi ningeomba ibadilishwe iandikwe Wazanzibari, yaani hata ikiwa Wazanzibari 50 watajumuika lakini waka *hold* 51% share ya ile kampuni basi waruhusiwe kuwa na kampuni hiyo ya televisheni au redio. Mhe. Spika, hilo ninataka lizingatiwe na lirekebishwe.

Vile vile, katika sheria mama ukurasa wa 11 hicho hicho kipengele cha 12 utakuta *tradition* bado zipo na hizi ndizo zinazokandamiza hii Sekta ya Utangazaji. Hapa juu Alhamdullilahi imezingatiwa imeondoshwa tunashukuru sana. Lakini chini hapa kwenye nambari nne inasema,

> *"The commission under any circumstances shall not permit any person to have both Radio and television station at a time especially to be granted only one of them"*.

Hii ni *restriction* ambayo inamfanya mtu ambaye ana televisheni na redio ni *easy* kuweza kuzi-*run.* Kwa sababu habari atakazopata katika letevisheni ndio zile zile atazopata katika redio. Kwa hivyo, ile *main power* yake anaitumia *to the both companies at the both areas.* Lakini kuna sababu gani ya kum-*restrict* mtu asifanye hivyo. Samahani sijakiona kama kifungu hiki kimefutwa, lakini kama kimefutwa *that is very good*.

Kwa hivyo, nasema kwamba mimi naunga mkono kwamba *restrictions* kama hizi ndizo zilizokuwa vikwazo vikubwa sana vikafanya *private sector* kuingia katika mambo ya utangazaji na kwa hali hiyo, ikafanya sekta hii idumae. Nafikiri kuwa mswada huu utatoa fursa nzuri zaidi kwa *private sector* kuungana moja kwa moja kwanza kuweza kutumia vituo vyetu kupitia

matangazo ya biashara lakini vile vile na wao kufungua vituo hivyo vya televisheni na redio ambavyo vitasaidia kuongeza idadi ya ajira na vile vile idadi ya vituo hivyo ambavyo vitatusaidia sana katika kuleta maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia na ninaiombea kila la kheri.

Mhe. Spika: Wakati nazungumza kwamba tunamalizia kwa maoni ya Mhe. Nassor Ahmed pale pale limejitokeza ombi moja. Kwa hivyo, pengine simuda mrefu tuangalie. Nimkaribishe basi Mhe. Juma Duni Haji.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kubadilisha uamuzi wako na kunipa fursa. Nimekuandikia ki-*note* hapo kwamba nikate mate ndio tunavyosema kule kwetu.

Mimi naunga mkono huu mswada mia juu ya mia, isipokuwa muda wote huu kwa sababu nilikuwa najifunza, nilikuwa ninawasiliana na wahusika kuna suala la msingi la kitaalamu ,kwa hivyo, nikaona bora niulize. Kuna hii kamisheni itakuwa inatoa mawimbi ya watu kufanya haya mambo, mawimbi yamewekwa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo lakini bahati nzuri mawimbi yanakuwa na kamisheni lakini sisi tulikuwa na madaraka ya mawimbi yetu yaani *coded* Gineva ilikuwa ni *plus* 259. ni *code* yetu hiyo Zanzibar tofauti na ile ya Muungano.

Sasa naomba kumuuliza waziri mambo mawili atusaidie, la kwanza kwamba hiyo *code* ipo au imekufa na kama imekufa ninavyojua suala hili halimo katika orodha ya Muungano. *I am to be corrected*.

La pili, mawimbi kwenye Serikali ya Muungano yanatolewa na kamisheni fulani inayoitwa Kamisheni ya Mawimbi. Sasa nikauliza haya tutakayotoa kwenye kamisheni yetu tunamegewa kama vile tunavyomegewa vitu vyengine au tuna access ya kutoa mawimbi kama watu tunaojitegemea?

Mhe. Spika, sikuwa na zaidi.

Mhe. Spika: Muda wa kumalizia unakaribia sasa nijue tu kama kuna wachangiaji wengine ili nitoe rai. Naona wapo, tukubaliane basi tukapumzike.

(Saa 6:55 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)
(Saa 11: 00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mohamed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, kunipa nafasi hii ya mwanzo katika jioni hii ya leo. Kwa kweli marekebisho haya ya mswada ni marekebisho muhimu sana kwa sababu Tume hii ya Utangazaji Mhe. Spika, ndio iliyo na majukumu makubwa katika kuongoza uwanja mzima wa Habari Utangazaji katika nchi hii ya Zanzibar. Kwa sababu hiyo na kwa kuwa habari zinaweza zikaunganisha watu au zikatenganisha watu basi tume hii ina jukumu kubwa sana ambalo limepikwa na Taifa.

Mhe. Spika, vyombo vya Habari katika jamii hususan Redio na TV ambazo watu wengi wanakuwa na nafasi zaidi ya kuvisikiliza au kuviangalia basi umuhimu wake ni mkubwa sana na kutokana na umuhimu wa vyombo hivyo ndio maana yakafanywa marekebisho haya ili lipatikane lililozuri zaidi la kutumia. Kwa sababu mara nyingi sheria inapotungwa kuna mambo huwa hayajulikani wakati mwengine mpaka pale sheria inapotekelezwa ndipo yanapojitokeza yakaonekana kwamba kumbe hili tulilisahau au kumbe hili tuliliweka lakini sivyo tulivyoliweka linavyostahiki lingekuwa hivi.

Mhe. Spika, kwa sababu hiyo ndio maana ikawa tunafanya marekebisho ya sheria mbali mbali zinazoletwa katika Baraza hili. Lakini Mhe. Spika, kabla sijenda mbali sana labda nianzie hapa wenzangu walipozungumza kuhusiana na vyombo vikuukuu au vyombo vikongwe vinavyoletwa hapa nchini kwetu na wakati mwengine wala sio vikongwe vyengine ni vipya, lakini kuna tatizo moja kubwa sana.

Vile vikongwe ndio tumeambiwa muda wake baada ya miaka mitano pengine vitakuwa havifanyi kazi tena na ingawa tumeambiwa kuwa na umri wake huwa miaka mitano mpaka saba. Lakini mimi nasikitika kusema kwamba mimi nina TV sasa hivi miaka 20 na naitumia na inafanyakazi. Kwa hivyo, inawezekana kabisa vyombo hivi vikongwe vilivyoletwa vikakaa muda mrefu zaidi kuliko ule uliotarajiwa. Hilo silo nililolikusudia.

Mhe. Spika, nililolikusudia hapa ni kuwa kuna udhibiti gani wa kuvipima vyombo vinavyoletwa viwe vipya au vikongwe kwa sababu vyombo vipya navyo vinaletwa lakini vinaletwa vyombo ambavyo ni feki kwa lugha ya kisasa. Sasa vyombo vya aina hii vinaingia katika maduka wananchi wananunua, muda wake unakuwa mfupi mno wa kutumia. Je, serikali imeweka mpango gani wa kuviangalia vyombo vinavyoingia kuonekana kama hiki kweli ndicho chombo halisi kinachotoka katika kampuni hii iliyoandikwa katika chombo hiki hilo moja.

Lakini pili kwa hivi vikongwe je, serikali ina mpango gani ulioandaa wa kuviangalia kuwa chombo hiki kinachoingia kweli kitachukuwa muda angalau

wa miaka 5 na kuwa pia hakitaleta athari nyengine yoyote ambayo huko kwao kilikotumika kilikuwa tayari inaaza kuleta athari hiyo. Hili nadhani Mhe. Spika, lina umuhimu mkubwa sana kufanyiwa maarifa.

Mhe. Spika, wenzetu hapo ndugu zetu, kaka zetu hivi karibuni tu wamevunja ma-TV mengi sana baada ya kuzichunguza na wakaona zina matatizo mbali mbali. Sasa sisi tusijifanye jaa la kuleta vile vilivyoshinda vikaja huku kwetu kwa sababu huko kwao hawana pa kuviweka tena, na ili tusifanye jaa basi kuna haja ya kuwa na huo mpango wa kuviangalia vinavyoletwa kabla havijaingia dukani vikachunguzwa vinavyofaa vikaingizwa dukani visivyofaa vikarejeshwa.

Mhe. Spika, kama likifanyika hilo basi kuna uwezekano mkubwa wa kuwasaidia wananchi wa nchi ya Zanzibar. Lakini isipofanyika hilo basi tungoje siku moja tuje kujilaamu ama katika Baraza hili au pahali pengine popote kutokana na mambo yanayoweza kujitokeza ambayo hayakutazamiwa lakini pia hayakufanyiwa uchunguzi mapema yakaonekana.

Mhe. Spika, labda nikitoka hapo kidogo nigusie tu pale alipogusia mwenzangu baadae akachachirishwa kwa bahati mbaya. Katika mabadiliko haya yaliyofanywa Mhe. Spika, kuna baadhi ya mambo ambayo yangestahiki nayo yabadilishwe, lakini kwa bahati mbaya hayakubadilishwa inawezekana walioandaa mabadiliko hayo hawakuyaona, inawezekana walioandaa mabadiliko wameyaona haya madhara yote na ndio hasa inavyostahiki kuwa. Lakini kwa sisi tunayoyaangalia hivi sasa, basi tunahisi na haya nayo yangefanyiwa mabadiliko.

Moja katika hilo ni lile alilolitanguliza Mheshimiwa wa ubavuni kwangu, la kifungu 12 (4). Ilipotajwa hiyo 4 nilidhani kuwa hiyo ni 4 ya mwanzo iliyobadilishwa. Lakini kumbe sio ile 4 ya mwanzo ya kubadilishwa hii ni kifungu cha 12 (4) si kifungu cha 4, maana yake cha 4 kilifutwa maana yake katika kifungu cha 12 hakijafutwa kitu. Hii inazungumzia habari ya mtu akiwa na televisheni tena asiwe na redio na akiwa na redio asiwe na televisheni.

Mhe. Spika, ama kwa mawazo yangu waliobadilisha hawakuipitia yote hii sheria kwa umakini au kama waliipitia hiki kiliwaponyoka kidogo katika kusoma. Kwa sababu kama alivyozungumza hapa Mheshimiwa ni kuwa unapokuwa na vyombo viwili kama vile ilivyo *ITV* na *Redio One* unaweza kufanya mambo yako kwa vizuri zaidi. Ukija upande wa redio mambo ni yale yale yanaletwa kwa upande wa redio na waliokuwa hawana TV watayasikia. Ukija kwenye upande wa televisheni wale waliokuwa hawasikilizi redio wataona kwa macho yao na kusikia kwa masikio yao yale yaliozungumzwa.

Mhe. Spika, Kwa hivyo, atakuwa na nafasi ya kuunganisha na kusambaza taarifa zile kwa vizuri zaidi na kwa upeo mpana zaidi kuliko akiwa na chombo kimoja tu. Hili nadhani halikuonekana siamini kama limeachwa kwa makusudi, lakini naamini kuwa kwa bahati mbaya jicho liliruka wakati wa kusoma. Kwa hivyo, naamini pia vile vile kwa sababu hiyo Mhe. Waziri hili atalifanyia marekebisho yanayostahiki ili twende sambamba na mawazo haya na ili wananchi wetu waweze kupata taarifa za habari kwa njia inayostahiki.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nahitaji nilizungumzie na zaidi labda Mhe. Waziri aje anijuilishe au anithibitishie maneno nitakayoyasema kama ni kweli au si kweli. Mhe. Spika, katika mkutano huu tutakuwa na sheria tukijaaliwa kama tulivyoambiwa inayohusiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka. Naomba nijue kwa sababu ninavyoelewa hakuna sheria ya TV na Redio hizi zetu sisi tulizonazo hapa. Sasa kama ni kweli hakuna sheria hiyo basi itakuwa tumechelewa sana kuileta hiyo sheria ikapitishwa hapa Barazani laa kama iko angalau nitajiwe tu kwamba ni sheria namba ngapi na aina gani nikaitafute na mimi niiseme. Hili Mhe. Spika, nalo lilikuwa ni miongoni mwa mambo ambayo yalikuwa niyazungumze katika kutafuta ufanisi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije katika marekebisho ukurasa wa 164 kifungu cha 11 cha marekebisho, ambacho kinarekebisha kifungu cha 14 cha sheria mama, ukikisoma kifungu hicho cha 14 kuna 1,2,3,4,5,6 na 7. Mhe. Spika, pamoja na utaalamu wangu wa Kiswahili niujuao nimeshindwa kukielewa kifungu cha 14 (7) makusudio yake hasa ni kitu gani kwa sababu kinasema ikiwa baada ya leseni ya kutangaza kutolewa muda usomaji mmoja. Usomaji wa pili ikiwa baada ya leseni ya kutangaza kutolewa muda uliotajwa kwenye leseni hiyo kumalizika kabla ya kutangaza pamoja na masharti yaliyowekwa wakati wa kutolewa leseni hiyo, kuna kitu hapa kilikuwa kiendelee hakipo.

Vyenginevyo nitakuwa sijui Kiswahili lakini nikiwa najua Kiswahili Mhe. Spika, hapa palikuwa na kitu pameachwa kwa sababu hii haijakamilika. Kwa hivyo, hii nayo ningependa ikiwa kuna kitu kimeachwa basi tuambiwe kitu gani kilichoachwa ikiwa imekusudiwa hivi tuambiwa maana yake kwa sababu mimi bado sijaipata.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kuna habari nzima ya hawa wenzetu wanaotufanyia kazi yetu wale pale. Mhe. Spika, hawa wanafanyakazi kubwa, wanafanyakazi ya kuwatangazia wananchi mambo yao kwa sababu mambo yanayozungumzwa ndani ya Baraza hili yakaamuliwa siyo yetu sisi ni mambo ya wananchi wenyewe.

Kwa hivyo,kazi wanayoifanya ya kuyachukuwa wakayapeleka wananchi wakayaona wamepangia nini na kitu gani kitakuwa vipi jambo limefanya pahali

gani wakajua japo hawajenda basi kwa kweli kazi wanayoifanya ni kubwa na mimi naweza kusema wao wana kazi zaidi kuliko tunayoifanya sie maana sisi tunafanya tukiwa tumekaa kitako na wao wanafanya wakiwa wamesimama.

Mhe. Spika, natasaf na nasema kwa masikitiko kuwa jamani angalau hivi visenti vichache wanavyogaiwa basi angalauu wangegaiwa kwa wakati, kwa sababu mimi hawajaninongoneza lakini ninavyoelewa kuwa wana deni wanadai hawa mpaka hivi sasa. Sasa Mhe. Spika, ikiwa ni hivyo basi sijui lakini nahisi kuwa ule mzigo tuliowatwika baadae na sisi wenyewe tunakwenda kuukalia juu sawa sawa na unavyomtwika Punda ndani ya soji lake na ukamtilia mizigo ukisha na wewe mwenyewe ukapanda pale juu. Kwa hivyo, ili Mhe. Spika, tuwapunguzie mzigo ule sisi wenyewe tuteremke basi angalau iwe tunawapatia haya mambo yao kwa wakati kama inavyostahiki.

Mhe. Spika, mswada huu ni mdogo tena ni mdogo sana katika miswada midogo na huu umo. Nikisema sana nitakuja kuunda mswada wangu mwenywe na hilo silo nililokusudia. Nakushukuru ahsante naunga mkono hoja.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi jioni ya leo kunipa nafasi. Naomba kutumuia muda mfupi kuelezea machache kuhusu mswada huu.

Kwanza Mhe. Spika, ni jambo la maana ya kupongezwa kwamba tukihisi kwamba kuna matatizo katika sheria zilizotungwa tukatayarisha masahihisho na kuweka hali kuwa ya muelekeo na ufanisi lakini ni uzuri kwamba tufanye kuupitia kwa umakini zaidi sheria nzima na kutumia wataalamu mbali mbali hasa ikiwa sheria ile imepitwa na miaka isiyopungua 10. kwa kuwa kuna mambo mengi yamejitokeza basi kuna haja ya kupitia sheria ile kwa undani zaidi ili tuweze kufanya mabadiliko ambayo hayatakuja tena katika kipindi kifupi kijacho.

Kwa hivyo, si kwa wizara hii tu lakini kwa wizara nyingi ambazo zinafanya mabadiliko katika sheria ni jambo la busara kwamba zisiharakishe sana kufanya yale mabadiliko lakini aone kwamba ile sheria imepitiwa vizuri zaidi na kuona kwamba vifungu tafauti vinafanyiwa mabadiliko yanayostahiki hilo la kwanza Mhe. Spika.

Pili, Mhe. Spika, kabla sijaingia katika mswada wenyewe kuna wataalamu ambao wanakuja kutoka mawizarani na sisi Wajumbe huwa tunachangia vitu vingine kwa ujumla. Sasa wakati mwingi huwa tunaelekeza pale ambapo tunaona pana kasoro au panahitaji marekebisho. Lakini wakati mwengine tunakuwa hatulengi ile sehemu ambayo ni husika kwa mfano leo tunaizungumza Tume ya Utangazaji, inawezekana maelezo yaliyotokana au

huko nyuma yaliwahi kutoka kuelekezwa wizara hii maalum kwa hii Tume ya Utangazaji. Sasa ni juu ya wale wataalamu kuweza kuyakubali haya na michango yetu na pale panapohusika ambapo sisi tunatoa michango jenerali ambayo hatujui ni wapi hasa inaelekezwa. Kwa hivyo, wale wataalamu inapaswa waichuje hii michango yetu na waielezekeze zile sehemu zinazohusika. Mfano mimi naweza kusema kuwa siwezi kuelewa kwa hivyo naomba sana wakati wa michango yetu hata kama ni jenerali lakini ni tatizo.

Mfano Mhe. Spika, hapa limezungumzwa tatizo la maadili, sasa wenyewe watu wa wizara wanajua maadili nani anayashughulikia ni hii Tume au ni nani kwa hivyo masuala yale yaweze kuekewa pahali pake.

Mhe.Spika, wasi wasi wangu sikukifahamu kifungu kimoja wapo katika vilivyorekebishwa kifungu namba 6. Sasa kina rekebisho moja linasema hivi : Kifungu cha 6 cha sheria mama kinarekebishwa kama hivi ifuatavyo, halafu inakwenda zake mpaka inafika namba 4 Mjumbe alieteuliwa chini ya kifungu cha (1c) atakuwa mtaalamu wa utangazaji na mawasiliano au habari kwa jamii.

Mjumbe mwengine kutoka vyombo binafsi. Sasa hapa kidogo nimechanganyikiwa mimi kwa sababu wale Wajumbe walitajwa wanne na hapa inaonekana kama ni wawili na suala hili hili kama Mjumbe kuna chombo binafsi anaweza kuwa yoyote yule lakini sio katika wale wataalamu na inavyotakiwa hasa yule anaetoka chombo binafsi awe mtaalamu zaidi kuliko huyu anaetoka chombo cha serikali kwa sababu yule ndie tunamuhitaji utaalamu wake ambao pengine upande wa serikali si rahisi kupatikana. Kwa hivyo, kifungu hiki kidogo naomba kiangaliwe kimekusudiwa nini hasa katika mantiki yake.

Mhe. Spika, kama ambayo nilianza mwanzo kusema kwamba mswada ulikuwa ufanyiwe upitiwe kwa undani kabisa ili tuweze kubaini kwa mfano kifungu ambacho kilitajwa katika namba 12 kifungu kidogo cha 4 hata kwa menejimenti, hata kwa ufanisi basi mtu anapokuwa au muekezaji wa ndani anapokuwa na kituo cha televisheni na anapokuwa na kituo cha redio inakuwa gharama ni ndogo kuliko kumwambia kuwa wewe uwe na televisheni na redio tu. Kwa sababu sasa hivi Mhe. Spika, tumesema kwamba vijana wanaofanya kazi humu wanahitaji kupewa mafao yao. Kwa hivyo, na huyu muekezaji mwenye kituo cha televisheni au kituo cha redio ana wafanyakazi na anahitaji kuwalipa.

Kwa hivyo, ikiwa atakuwa nao watakaofanyakazi kwa ajili ya kituo chake cha redio wakati huo huo anafanyakazi kwa ajili ya kituo chake cha televisheni inakuwa zile gharama za uendeshaji si kubwa kama ambavyo ukimwambia mmoja tu mwenye redio au TV.

Pengine ndio kilichopelekea kwamba tukawa na redio tupu sasa hivi Zanzibar za binafsi bila ya kuwa na TV kwa sababu uanzishaji wake unahitaji gharama kubwa, yaani tukieka hii motisha mwenye kituo cha redio anaweza kwa leseni ya kubadilisha leseni akaongeza na kituo cha televisheni hawa hawa wenye redio wanaweza kujitokeza wakaweka na televisheni. Kwa mfano Mhe. Spika, sisi bado hatujakuwa na televisheni ya kimasomo, mimi nimeona Pakistani kuna kitu kinaitwa *Victual University* wanasomesha tu wao ukifungua kuna darasa naona *channel* kama 3 mpaka 4 Pakistan. Sasa kwa nini sisi ikiwa hatuna televisheni ambayo kila ukifungua wewe unasomo moja.

Sasa hivi tuna ukosefu mkubwa wa elimu hasa masomo ya Sayansi ni rahisi sana kuweza kulibadilisha hili suala tukawa na televisheni hiyo mwalimu mmoja tu anasomesha Unguja na Pemba hapa na anaweza akajibu masuala japo kuwa kwa siku ya pili akajibu maswali ya wanafunzi wote kutoka kila pahali. Kwa hivyo, lazima twende katika hatua ambayo tuna- *courage* kwa baadhi ya matatizo yetu ambayo afikirie njia vile vile ya kuweza kuoanisha hizi *opportunity* za kutoa televisheni pamoja na redio kwa leseni moja ambayo ina *operate* kama walivyosema wenzangu Mhe. Spika, kwamba mswada huu ni mdogo na kwa kweli tungeutegemea kwamba utatoa vipengele vingi vya kuweza kutusaidia katika baadhi ya matatizo ambayo tulionayo.

Kwa mfano Mhe. Spika, nilitangulia kuuliza asubuhi leo hapa kwamba televisheni kama nne za Tanzania zote ziko katika mtandao wa *satellite*, nilisema tatu pale lakini nakumbuka ni nne,. Kwa hivyo, kukitokezea matatizo yoyote ya kimawasiliano kwa sababu kile kituo kimeshatiwa katika mtandao wa *satellite*, basi wananchi wenye vile vyombo vya *satellite* katika majumba yao yaani madishi wanaona mawasiliano bila ya matatizo yoyote.

Sasa katika kazi za Tume hii ya Utangazaji bila shaka mojawapo ni kuukuza ule utangazaji si ku-*control* na kuweka tu. Sasa tuone kwamba na sisi tunakwenda kwa kasi ya kufikia hapo ili TVZ iingie katika mtandao wa *satellite*.

Mhe. Spika, angalia *satellite dish* sasa hivi katika nchi za Kiafrika mimi nafikiri ni peke yetu ambao hatupo katika mtandao. Kwa sababu ukifungua hii *satellite* iliyo na hizi ITV na nyenginezo unaweza ukapata Msumbiji, Angola, Uganda na kadhalika. Ukifungua *Arab Set* unapata hizi za hapa karibuni *Horn of Africa* kama Somalia, Djibout wote wamo katika mtandao wa *satellite*. Huko Somalia ambako hata serikali hakuna kila mmoja ana mrau tu juu ya bega wanakwenda mbio, bado televisheni yao imo katika mtandao wa *satellite*.

Sasa kwa nini Zanzibar ambako tuko katika hali nzuri na wataalam tunao *Alhamdulillah* haufiki wakati tukasema kwamba mwaka 2012 basi TV yetu iingie katika mtandao wa *satellite*. Tukijipa *challenge* Mhe. Spika, ndio tutakapofika, lakini tukisema sisi bado tuko hivi hatutofanya kazi. Mimi namtegemea Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa sababu ni mtaalam alikuwa achukue *challenge* hii na atuingize katika mtandao wa *satellite* itakapofika 2012, ili mitambo yetu ikifeli hapa basi wale wenye madishi waseme jamani leo mnamuona Rais kafanya hivi, Waziri Kiongozi kafanya hivi lakini mtandao wetu umefeli.

Mhe. Spika, nafikiri hii Tume ya Utangazaji badala ya kuiweka katika *scope* ya kuangalia tu mambo, lakini tuipe na *scope* ya ku-*expand* utangazaji wetu na kuweza kweli kweli kuingia katika mtandao wa kidunia.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba niunge mkono hoja na kumtakia Mhe. Waziri kila la kheri ili aweze kutufikisha katika hali ya utulivu na usalama.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, najua kusema ni sunna hapa Barazani. Kwanza naunga mkono hoja hii, lakini napenda sana kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Pia, nampongeza yule aliyeuliza swali asubuhi sijui nani, namna Mhe. Mahmoud alivyojibu lile swali leo kusema kweli ameweka wazi mwenendo mzima wa habari na hatari zake hapa Zanzibar. Mhe. Spika, Mhe. Mahmoud kweli ni Naibu Waziri wa Wizara hii na anaielewa ile fani na teknolojia yenyewe. Mhe. Spika, nampa hongera sana Mhe. Naibu Waziri, kama ana *degree* akachukue *Phd* huko. Tunakutegemea bwana.

Mhe. Spika, kama ulivyo mswada wenyewe kwamba ni mdogo na mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa. Lakini nieleze ile hofu ambayo Mhe. Zakiya Omar Juma ameieleza pamoja na Waheshimiwa wengine ya ifikapo mwaka 2015. Tabaan watu wa visiwa hivi sasa watakuwa hawana tena nafasi ya kupokea habari, kama ndivyo nilivyomfahamu Mhe. Naibu Waziri, ni wachache tu watakaopokea habari.

Mhe. Spika, nadhani wakati umefika Zanzibar tukubali kuwa dampo. Nasema hili ni jambo la lazima *by hook or by crook.* Sisi tunaona wenzetu hawa kina Mhe. Zakiya Omar Juma wakenda kule wanatuletea mitumba hii shilingi hamsini elfu unapata TV, lakini kesho kutwa TV hiyo itakuwa haifanyi kazi haina maana. Hebu tuangalie ifikapo kesho kutwa hii mitumba iliyokuwepo na hapa itakuwa pia haifanyi kazi tena tutaipeleka wapi. Tuna taratibu gani ya kuviharibu kwa sababu vitakuwa havifai tena lazima vitupwe, kama vitupwe, vitatupwa wapi na kwa utaratibu gani.

Bahati nzuri wenzetu wa Europe wamejua utaratibu wa kutupa walete Africa tena kwa gharama zetu si gharama zao, tunakwenda tunachukua tunawapunguzia ile kazi ya wao kuviharibu tunachukua sisi tunavileta huku. Je, ikifika 2015 na hiyo 2020 nini tutafanya. Hili ni lazima tuliangalie sana. Mhe. Spika, Zanzibar tuna tabia ya kupuuza.

Mhe. Spika, ningependa Mhe. Waziri anieleze kwa uwazi kabisa mitambo yetu ya redio ya Dole sina hakika nayo iko katika mtandao gani, huo wa *analogue* au *digital*. Lakini nina imani kwamba utakuwa katika huo wa zilipendwa. Sijui nini hatima ya mitambo ile muda mfupi ujao na Wizara imejipanga vipi kuwa na vituo au mitambo ya redio ya hiyo *digital*.

Mhe. Spika, jengine kwa maelezo ya Mhe. Naibu Waziri leo asubuhi ina maana ndugu zangu wa Pemba wakate tamaa ya kupata mawasiliano ya TV kwa sasa hivi. Nilivyomfahamu ni hivyo na hivyo ndivyo ilivyo. Kwa sababu mitambo yetu ile ni ya muda mrefu imeshazeeka, ni wazi kabisa hata hizo *spare* zenyewe kuzipata ni tabu, viwanda hivyo sasa haviko tena katika kutengeneza hizo *spare* za *analogue* watu wanakwenda kwenye huu mtandao tunaouita wa kileo. Ndio maana tulikuwa hatujui kwa nini Pemba kwa muda mrefu tumekuwa tukipiga kelele hapa, kila bajeti inayokuja Pemba televisheni hawaoni lakini leo tumejua kwa nini. Kwa hiyo, hofu ya kwamba pengine mpaka 2015 au zaidi ndio watu wa Pemba wataweza kupata taarifa kupitia TVZ.

Mhe. Spika, jengine hivi karibuni Pemba kimefunguliwa kituo kidogo cha Redio ya Jamii cha Micheweni. Ningependa kujua tu kama kituo kile na mitambo ile ndio ya kileo au ile ile ya kizamani. Kama ya kileo basi lazima tuwapongeze, lakini kama ni ya kizamani sijui tutafanyaje kesho kutwa. Kama ya kileo ni vizuri tunawapongeza tena sana, lakini kama ya kizamani ambayo kesho kutwa itakuwa nayo ni *useless* nadhani tumechemsha. Sipendi kutumia neno hilo lakini ndio ukweli.

Mhe. Spika, sioni tabu kusema kwa sababu aliyefungua mitambo ile juzi ni Mhe. Rais, sasa kama juzi tumempeleka Mhe. Rais pale kwa shangwe, hoi hoi na vifijo lakini kesho kutwa ikawa inaambiwa nayo haimo tena katika mwelekeo mzuri nafikiri haikuwa jambo la busara.

Mhe. Spika, nikija kwenye mswada wenyewe kwenye marekebisho ya kifungu cha 14 “Mipaka ya Mamlaka na Utoaji Leseni” namba 6 anasema “Ikiwa tarehe ya kumalizika muda wa leseni imefikiwa na tume haijafikia uamuzi wa kuhusiana na ombi la kuitoa tena leseni, leseni hiyo itaendelea kufanya kazi mpaka ombi la kutoa tena litakapokubaliwa au kukataliwa na tume”

Mhe. Spika, nadhani huu ni ukiritimba, kuwe na sababu zipi za msingi. Ikiwa mtu amepeleka leseni miezi mitatu kabla, miezi mitatu ile ishe leseni hiyo haijatolewa. Hebu tujiulize kuna kitu gani kikubwa hata kifanye miezi mitatu mizima, kama kuna tatizo watu wenyewe tuko hapa hapa hakuna mtu anayetoka Makka wala Baghdad, wote tuko hapa hapa miezi mitatu inakwisha nini kikubwa.

Lakini pia kifungu hakikusema, tumesema tu leseni ya zamani itaendelea, kwa muda gani, lazima kuwe na *time* maalum, pengine baada ya kipindi fulani lazima leseni hiyo iwe imepatikana. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipe ufafanuzi kidogo.

Lakini kwenye kifungu cha 6 B "Muda wa Wajumbe". Anasema Wajumbe watasita kuwa Wajumbe wameeleza hapa kuna kifungu (a), (b) na (c), mimi niko kwenye (b). Anasema "Mtu atasita kuwa Mjumbe wa Bodi ikiwa: atakuwa na mgongano wa maslahi". Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri hebu anipe ufafanuzi mgongano wa kimaslahi ni upi.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa kupitia kwake Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, tulikuwa tumesikia hapa katikati kwamba wizara yako inategemea kujenga kituo kipya cha televisheni na wenzetu hawa wa China, sijui kama taarifa hiyo ni ya kweli na kama ina ukweli imefikia hatua gani. Kwa sababu Wachina ni wazuri tu katika mambo haya ya habari.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda sana kuvipongeza vyombo vyetu vya habari binafsi pamoja na redio zetu. Lakini nasema napenda sana kuvipongeza hivi vya redio binafsi kwa sababu vimeweza kujibadili, wakati wowote kukitokea tukio pale pale wanakwenda kwenye tukio wanakatisha matangazo yao moja kwa moja wanatoa ile taarifa.

Kwa mfano siku ile ilipoungua moto nyumba iliyo karibu na Wizara ya Elimu zamani pale, wengine tumepata ile habari kwenye redio tena tuko kwenye gari. Pale pale wametoka kwenye vipindi vyao vyengine wamekwenda kule baadae wakatangaza. Sasa hata redio yetu ya Zanzibar nayo kuna haja ya kubadilika iende na wakati, iende na matukio.

Mhe. Spika, baada ya hayo narudia kusema naunga mkono hoja hii kwa mara nyengine tena.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hoja ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo juu ya marekebisho haya ya Sheria ya Tume ya Utangazaji.

Mhe. Spika, kabla sijenda kwenye mswada huu nakuomba unipe nafasi kidogo kuwapongeza Wajumbe wetu wawili hapa walioteuliwa na Mhe. Rais kuungana nasi katika Baraza hili la Wawakilishi. Mhe. Spika, leo asubuhi uliwaapisha Waheshimiwa hao wawili lakini bahati mbaya nilikuwa na dharura sikuwepo wakati huo. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii ya kumpongeza Mhe. Juma Duni Haji mwenyeji wa Mkwajuni Wilaya ya Kaskazini 'A' kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Halikadhalika nampongeza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui mwenyeji wa Mitamani Shehia ya Pujini Wilaya ya Chake Chake kwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Spika, nivipongeze na vyombo vyote vilivyowateua hususan Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kutimiza majukumu yake Kikatiba ya zile nafasi kumi tulizompa atuteulie Wajumbe hawa. Naamini Mhe. Rais ametimiza kazi yake hiyo na ametuletea Waheshimiwa hasa kwa sababu ninawajua. Nimeelezea asili yao wanakotoka kwa muda mrefu mimi nawajua vizuri sana. Sasa nasaha zangu kwa maelezo niliyotoa hawa ni wazalendo kwa hivyo watumikie wananchi wao, watoe michango yao kwa maslahi ya Zanzibar. Mhe. Spika, huo ulikuwa ni utangalizi nakushukuru kwa kunipa nafasi hiyo.

Mhe. Spika, huu mswada ni mzuri unasaidia chombo chetu cha Tume ya Utangazaji kufanya shughuli zake vyema. Mimi michango yangu itakuwa mitatu juu ya mswada huu. Kwanza juu ya nafasi ya utangazaji.

Mhe. Spika, kwa kadri nilivyowasikia Wajumbe wenzangu wakichangia hapa kuwa tume hii ina kazi nzuri na muhimu sana. Kwa sababu kwanza inatoa fursa kwa vyombo vyenye kutuletea habari kuwawekea utaratibu. Televisheni, redio na vyombo vyengine vya kisasa ambavyo sivijui katika sayansi ya siku hizi. Lakini Mhe. Spika, kwa sababu huduma hizi zote zinatolewa na wanadamu. Kwa hivyo, ningependa kutoa mawazo kwa hawa watoa huduma hasa watangazaji. Kwanza lazima wawe na elimu ya kutosha kwa sababu vyombo hivi tunavihitaji sasa kwa elimu. Pia, wawe ni wenye kuenzi maadili ya nchi kama ilivyozungumzwa na baadhi ya wajumbe.

Mhe. Spika, baadhi ya redio zetu ni kweli niunge mkono Wajumbe zinapotosha maadili. Kwa hivyo, nafikiri chombo hiki kazi yake kubwa itakuwa nayo kuhakikisha vile vyombo ambavyo vinapotosha hii tume idhibiti kwanza kwa lugha zinazotumika.

Mhe. Spika, zamani redio zote za Afrika Mashariki utapenda wakati wote usikilize habari zao, mtangazaji wa Sauti ya Zanzibar, mtangazaji wa Redio Tanzania, mtangazaji wa Redio Kenya takriban wanasoma lafudhi na maneno sawa sawa tofauti na hivi sasa. Wenzetu wana vyombo vyao vya kutohoa lugha lakini bado sisi Zanzibar hatuna.

Kwa hivyo, nafikiri iko haja sasa hivi tume yetu ihakikishe watangazaji wanatumia lugha safi ile ya Wazanzibari. Sisi hatujawa na uhaba wa maneno. Wale wanaopewa leseni na tume hii wahakikishe wana uwezo wa kutumia lugha yetu ya Kiswahili vilivyo bila ya kuipotosha wala kututungia lugha za ajabu ambazo hazipo. Hili ni suala moja ambalo naipa kazi hii Tume ya Utangazaji na iweze kuwadhibiti kwa wale ambao watakuwa wanaonekana moja kwa moja au kwa kificho wanaharibu silka kwa kutumia lugha hii ya mtandao.

Mhe. Spika, kutokana na hilo mimi ningependekeza hawa watangazaji wote wawe na leseni kama watu wengine, hii itakuwa ni urahisi kuweza kumdhibiti yule ambaye atakuwa mtukutu wa kutofuata maadili ambayo yamewekwa chini ya kanuni za Tume ya Utangazaji. Kwa sababu siku hizi wanaweka lugha za kibiashara lakini wanatumia lugha za ovyo ovyo.

Tunataka vyombo hivi tunavyovipa ruhusa chini ya tume hii basi viwe vinatumia lugha safi, hiyo itakuwa ni njia moja ya kuienzi lakini pia kuitukuza lugha yetu ya Kiswahili. Maana yake siku hizi tunasema MTAMBUKA. Kwa hivyo, njia ya kupanua lugha yetu hivi sasa tunasema lugha ya sita, ili kuitangaza basi hivi vyombo vyetu ambavyo tunavidhibiti Zanzibar basi viweze kutumia lugha hii vizuri ili wengine na wao waweze kuikubali lugha yetu kuitumia katika mambo yao.

Mhe. Spika, kifungu cha 10 kuna eneo ambalo ningependa kusaidia. Kuna baadhi ya wakati hivi vyombo vya utangazaji vinafanya kazi kama ya ubia kama vile kwenye matangazo ya mpira, utaona redio sijui na mitambo ya *TTCL*, sijui TV na mitambo ya *ZANTEL* wanashirikiana kurusha mambo haya. Sasa inapotokezea kama hivi leseni ya nani inayotumika pale wakati ikifanya makosa iweze kudhibitiwa. Namuomba Mhe. Waziri hili anisaidie maana yake vinakuwepo vyombo viwili vinafanya kazi kwa ubia.

Mhe. Spika, jengine mbali ya kuwapa ruhusa wenye redio hizi lakini kuna shughuli zetu nyengine za kijeshi kuna redio. Je, tume hii itakuwa na mamlaka hayo katika hii mipaka iliyowekwa, watakuwa wanatoa leseni za kutumia hivyo. Namuomba Mhe. Waziri atueleze zile njia wanazozitumia wenzetu hao katika vyombo vya dola na hata vya ulinzi tutakuwa na mamlaka navyo sisi au watakuwa wanapata wapi njia za mawasiliano.

Mhe. Spika, nimezungumzia namna ya watoa huduma katika vyombo vyetu vya habari katika eneo moja tu, lakini bado kuna malenga hawa watungaji wa nyimbo, mashairi nao lazima watambulikane, ili wanapotunga nyimbo ambazo hazina maadili waweze kurekebishwa. Si mtu yeyote tu anakuwa na nyimbo yake akafika kwenye chombo cha habari itangazwe na kuoneshwa.

Tunayo kamati ya sensa lakini pia na hawa waweze kusajiliwa wajulikane, hii yote ni kuweza kuhakiki tunapata watu ambao hawatoharibu silka kwa kutumia vyombo vyetu vya dola. Kwa sababu ukitumia vyombo hivi vya redio na televisheni habari zinawaendea haraka sana, tofauti na msondo ukiupiga tu hapo uwanjani bila kutangaza atakayefaidika yule yule aliyekuja, lakini ukirusha hewani wataenea watu wote wa Zanzibar na vituo vyenginevyo. Kama zuri ndio zuri lakini kama baya hii yote imeshaenea kwa asilimia kubwa.

Mhe. Spika, la mwisho niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga kituo cha Redio ya Jamii Micheweni, nafikiri huu ni mwanzo wa safari ndefu, lakini pia iko haja kila wilaya na wao kuweza kupatiwa. Kwa sababu tumeshaona hapa uwezo wa redio yetu haukidhi kuchukua habari za sehemu zote za wilaya kutokana na matatizo chungu nzima, wataalam hata usafiri. Lakini serikali ikimudu angalau kila wilaya ikaweka kituo chao, basi wananchi wakiona shughuli zao za kila siku katika redio yao pale itasaidia kuwatia mori kujikaza zaidi kuleta maendeleo.

Mhe. Spika, lengo la redio ya Micheweni ni zuri sana na linakwenda sambamba na sera yetu ya Mpango wa Kupunguza Umaskini (MKUZA). Kwa sababu mtu akiwa hana habari peke yake anakuwa ni maskini. Watu wanafanya hili wewe huna lolote ulimwenguni maskini utasikia tu. Leo wanatoa matangazo ya kazi, wewe japo una elimu husikii utakuwa maskini, waliosikia habari wanakwenda kujaza fomu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, serikali kuimarisha vyombo vya habari kama huu mtambo wa redio ya Micheweni bado itakuwa ni silaha kubwa ya kuweza kupambana na hali ya kuondosha umaskini. Nimuhakikishie Mjumbe mwenzangu hapa Naibu Waziri wa Maji, mitambo iliopo pale ni ya kisasa.

Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba alitupangia kwenda kuona kule kwa sababu mradi ulikuwa chini ya Afisi ya Mkuu wa Mkoa, tuliwahi kwenda kule tukaona ni mitambo ya kisasa kabisa ina uwezo wa kutangaza habari katika Wilaya ile ya Micheweni na hata wale wa karibu, watu wa Shengejuu, Kangani na Kojani wanaweza kupata taarifa au kutumia huduma za mtambo huu. Kwa hivyo, wasiwe na wasi wasi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kwa niaba ya wananchi wa Koani, mimi naunga mkono hoja hii.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi hii saa hizi. Kwanza sina budi kuwapongeza wageni wetu hawa Wawakilishi wapya wawili walioapishwa leo ndugu Nassor Ahmed Mazrui na ndugu Juma Duni Haji. Kwa hivyo, nawapongeza sana kama walivyowapongeza wenzangu.

Mhe. Spika, mimi nitaanza na ombi, mapendekezo au rai ya hizi taminoloji au sijui ndio misamiati hii iliyochambuliwa. Huduma za maudhui, halafu imeelezwa maana yake ni kutoa huduma. Hapa mimi napendekeza kwa vile tunachambua neno huduma, basi tusilirejee tena hili neno huduma, kuwasilisha ujumbe mahususi. Nahisi kama tuweke neno, kuwasilisha ujumbe mahususi halafu tuendelee kama kawaida, kwenye hiyo ibara inayofuata.

Usambazaji wa ishara za ujumbe maana yake ni usambazaji. Kwa hivyo, madhali tumechambua neno usambazaji hapa pia naomba tuondowe hili neno usambazaji, tuweke utoaji au uenezaji halafu tuendelee kama kawaida.

Halafu Mhe. Spika, nina ombi au rai nyengine kwa Mhe. Waziri ya hawa waandishi wa habari. Kuna waandishi wa habari kazi yao siku zote kusema habari kinyume nyume sivyo wanavyozipokea, hususan za viongozi. Wao ikisemwa hivi wanabadilisha hivi. Nahisi hawa tuwawekee mikakati mahususi hasa au sheria maalum kwa wote wale wanaowasaliti viongozi kwa kusema wanavyotaka wao tuwachukulie hatua, napendekeza hilo kwanza.

Halafu pia tujitahidi kuboresha vyombo vyetu vya habari. Kwa kweli vyombo vyetu vya habari tuviboreshe kweli kweli, tukilinganisha na vya wenzetu basi tuko nyuma. Kama ni *actors*, basi tujaribu kufungua milango lakini kwa mazingira yetu ya Kizanzibari. Kwa kweli tunao *actors* wazuri kutokana nafikiri kama ni viwango au sijui ni kitu gani kilichokuwa ghali na *actors* wetu ni maskini, basi tujaribu kuwapangia mipango madhubuti au taratibu maalum ili kupata *actors* wazuri, ili na sisi hizi TV zetu au kama ni redio zetu basi zipendwe kama vinavyopendwa vyombo vyengine. Lakini kwa mpangilio halisi wa mazingira yetu ya Kizanzibari sio kama mazingira ya wenzetu.

Vile vile, namuomba Mhe. Waziri kufanya kama motisha maalum kwa hawa ambao watajitokeza ili wahamasike na tupate *actors* wazuri, watendaji wazuri pamoja na waandishi wazuri. Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru, yangu mimi ni hayo tu kidogo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa na mimi jioni hii ya leo kuungana na wenzangu kuchangia mswada huu wa habari.

Mhe. Spika, kwanza kabisa kwa ruhusa yako nakuomba uniruhusu niishukuru kamati ya maandalizi ya sherehe za Mapinduzi yaliyofanyika Kisiwani Pemba. Kwa heshima kubwa Mhe. Spika, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Sherehe za Mapinduzi iliyofanyika Pemba kwa kufanikisha ili ikafanikiwa vizuri sherehe ya Mapinduzi. Pia, nawashukuru wananchi wa Zanzibar wote kwa kujitokeza kwa wingi kushiriki katika sherehe zile za Mapinduzi.

Jambo la pili Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niungane na wenzangu kuwashukuru viongozi wetu waliofanya mazungumzo ya makubaliano mpaka kufikia leo tumeungana na wenzetu walioteuliwa na Rais wa Zanzibar kuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nashukuru sana.

Mhe. Spika, jioni hii ya leo napenda nimshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa kutekeleza ahadi yake tuliyokuwa tukishikana kila leo hapa Barazani. Nashukuru kwamba ahadi yale ile redio ya jamii ya Micheweni tayari imefunguliwa. Kwa hivyo, nashukuru sana kama imefunguliwa wakati muafaka, kwa sababu ni wakati ambao tunataka kusikiliza kutoka mfumo uliokuwa wa zamani na kuingia mfumo wa kisasa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na Serikali nzima ya Mapinduzi ya Zanzibar, ile redio ya jamii ya Micheweni naomba isiwe redio jamii ya Micheweni peke yake, kwa sababu sasa hivi tunasikiliza pale Micheweni mpaka Mapofu tu haisogei pengine. Kwa hivyo, naomba iboreshwe ile redio ili na wenzetu wengine wapate habari kutoka kule Micheweni, kwa sababu isiwawezeshe wale wa Micheweni tu itakuwa hatukufanya kitu. Kwa sababu matokeo ya Micheweni wakisikia wa Micheweni peke yao itakuwa hamna kitu, lakini wakisikia na wenzetu wengine basi watajua Micheweni kuna nini.

Kwa hivyo, naomba ile redio iwezeshwe kwa sababu sasa hivi haijajengewa mnara, yaani habari zake ni pale pale Micheweni. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali ile redio iwezeshwe ili iwe ni redio ya jamii lakini wanaoisikiliza ni watu wote sio pale Micheweni tu.

Mhe. Spika, kwa kweli ile redio imekuja wakati ndio na sisi wa Micheweni tumeipokea kwa mikono miwili na tunafurahia kwa kupata chombo kama kile. Kwa hivyo, nawaomba na hii redio jamii isiwe Micheweni tu na wenzetu wengine wafikishiwe ili na wao wapatekufaidika.Mhe. Spika, ni hayo machache, nakushukuru sana.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa Tume ya Utumishi wa Habari. Mhe. Spika, kabla ya yote kwanza nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na Katibu wa Chama cha CUF kwa kumkaribisha Ikulu na kumpatia maji yamekuwa na neema na yamezaa Wajumbe wawili hapa tuliokuwa nao. Kwa kweli kwa mchango wao mzuri ambao tumewaona leo hii tu wanavyochangia, basi wanaonesha dhahiri sura zao tu kama wataleta maendeleo.

Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Rais kwa juhudi hiyo. Ninawaomba Wajumbe hawa tushirikiane kama tulivyoamrishwa hapa na Mhe. Spika, wetu. Kwa hivyo, kati yetu mmoja akigeuka nyuma waswahili wanasema awe mwanga.

Mhe. Spika, nakuja katika kuchangia mswada huu. Mimi kwanza namshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri wa Wizara hii pamoja na Katibu Mkuu, kwa juhudi yao kubwa waliochukua kutuletea mswada huu ambao kwa kweli mswada huu ni pahala pake kutuletea. Naamini wazi kwa juhudi zake Mhe. Naibu Waziri na Katibu wake, basi Inshaallah mambo haya ya uandishi wa habari na wizara hii itazidi kuendelea na kuleta mafanikio.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka huko nyuma tunakotoka tulikuwa hatuna vyombo vya habari, ilikuwa mara nyingi tunatumia vyombo vyetu vya kiasili kupeana habari. Kwa mfano vijijini utakuta mtu kapanda kwenye mti mkubwa kama mnazi na tarumbeta yake basi tulikuwa tunaitana kwa njia kama hiyo. Au wengine walikuwa wanatumia ngoma kubwa tu kwa kuipiga kwa mshindo mkubwa na wanakijiji wakisikia ndio wanakusanyika na kujua nini kilichotokea.

Mhe. Spika, tukaendelea hivyo hivyo mpaka hatimae hapa kwetu Unguja tukawa na Sauti ya Unguja kwa kipindi hicho kwa kweli tukaenda vizuri na redio ya Sauti ya Unguja ile ikawa na hamu kwa wananchi na watu wote wakawa wameipenda na wakawa na hamu ya kuisikiliza.

Mhe. Spika, ilikuwa mara nyingi ukifungua Sauti ya Unguja utawasikia wasanii au waimbaji mbali mbali mahadhi yao na usanii wao. Kwa hivyo, kwa kweli tulikuwa tunaburudika, unatulia tu kama ulikuwa na mawazo finyu basi yalikuwa yanaondoka kabisa. Wengi walikuwa wana hamu kuisikiliza Sauti ya Unguja.

Kwa hivyo, tumekwenda mpaka tumeipata Sauti ya Tanzania Zanzibar. Bado mtandao ni ule ule wa kupendwa na wasikilizaji wengi tu kwa lahau zake na wasanii wake wanaorikodi na ku-*act* vipindi mbali mbali katika Sauti ya Unguja ilikuwa lile tabasamu zuri.

Mhe. Spika, ukiwa nje ya nchi hii mara nyingi ikifika vipindi vya michezo unapenda kuitafuta Sauti ya Unguja au Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa kupata kusikiliza habari au vipindi mbali mbali vinavyorikodiwa katika Sauti ya Tanzania Zanzibar. Kwa hivyo, ilitupa hadhi ya kutosha ya kutambuliwa na kututangaza Wazanzibari kwa Sauti yetu hii ya Tanzania Zanzibar.

Mhe. Spika, kubwa tunaloliomba Mhe. Waziri kwa kuwa Sauti yetu ya Tanzania Zanzibar ina vipindi vingi na baadhi ya wasanii wengi wanapenda kurikodi na michezo yao inapendwa na watazamaji wa nchi mbali mbali. Kwa hivyo, naomba tu katika mtandano huu tuliokuwa nao hivi sasa wa digital uwe wa uhakika na wa ukweli katika urushaji wa mawimbi, uchujaji wa sauti na mipangilio mbali mbali iwe ya uhakika ili irushe katika maeneo ya mbali kabisa ya Zanzibar.

Kwa mfano mtu akiwa Arusha aisikie Sauti ya Zanzibar, mtu akiwa Pemba aisikie kwa fasaha Sauti ya Zanzibar. Isiwe leo studio ngeni zikawa zina nguvu ya kusikilikana kama vile Arusha, ukija kwenye hii redio Zenj FM au redio Chuchu utazisikia zinasikilikana na ni redio za juzi tu, lakini ukija kwenye Sauti yetu ya Zanzibar haisikikani kule. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri katika mpango huu wa vifaa hivi vipya viwe vya uhakika, ili na sisi tusikikane katika nchi za wenzetu wa jirani.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka Sauti yetu ya Zanzibar ina lafudhi nzuri ya matangazo yake na wengi huwa wanaivizia pale inaporusha habari zake. Kwa mfano kama michezo ya kuigiza au vipindi vya mawio, huwa mara nyingi watu wanategea nyakati zile kwa kupata habari na kusikiliza. Kwa hivyo, mkakati huu unaotayarishwa sasa hivi, basi mimi ningemuomba Mhe. Waziri na watendaji wake wapewe nyenzo za kutosha ili kufanikisha suala hili.

Mhe. Spika, kwa kweli hivi sasa kuna haja kubwa ya kuimarisha kituo chetu hichi cha habari cha Tanzania Zanzibar, kama inavyoeleweka habari katika nchi ni muhimu sana, habari katika nchi kama zitatangazwa kwa uhakika basi zitaleta ulinzi, usalama wa nchi na utulivu wa wananchi. Kwa hivyo, chombo hiki ni vyema kama nilivyoeleza kikapewa nyenzo za kutosha ili kupata kujiimarisha vizuri zaidi kama walivyojiimarisha kwa baadhi ya vyombo vyengine.

Mhe. Spika, mimi niwapongeze zaidi waandishi wetu wa habari, watangazaji wa chombo chetu hiki kwa juhudi kubwa wanazochukua juu ya kuwa na baadhi ya mapungufu madogo madogo basi huwa wanastahamili, lakini mara zote wanakuwepo kazini ili kutekeleza majukumu yao. Kwa hivyo, kwa hili nawapongeza kwa juhudi zao kubwa wanazochukua.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 103 kifungu cha 6(b), naomba kunukuuu.

Kifungu cha 6(b)

> "Mtu atakayesita kuwa mjumbe wa bodi ikiwa atawasilisha taarifa ya kujiuzulu kwa mamlaka iliyomteua"

Hii Mhe. Spika, mtu kama keshakuwa Mjumbe wa bodi basi mtu yule aamuwe tu kwa binafsi yake kuamua kujiuzulu au kustaafu, kwa kweli inakuwa ngumu. Isipokuwa kipengele hiki ningeomba tu kwamba mtu huyu kama kenda kinyume na taratibu au maelezo yake sio sahihi katika kutekeleza bodi hi.Kwa hivyo, asingojewe mpaka ajiuzulu, alazimishwe kujiuzulu, kwa kumsubiria tu aandike barua ya kujiuzuli, kwa kweli hili sio rahisi. Wakati mtu anapata maslahi na shughuli zake zinakwenda vizuri kuwa ajiuzulu hapa patakuwa na utata. Kwa hivyo, ningeomba aangaliwe ikiwa pindipo anakwenda kinyume na taratibu basi alazimishwe kujiuzulu.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 104 katika kifungu cha 14. Naomba kunukuu.

Kifungu cha 14

> "Leseni ya Utangazaji na leseni nyenginezo zitatolewa kwa kipindi kitakachoamuliwa na tume, lakini haitozidi kwa maombi ya leseni ya utoaji huduma ya miaka mitano"

Mhe. Spika, katika kifungu hiki mimi ningependekeza masuala ya utoaji leseni yawe kama yaliyokuwepo sasa hivi jinsi ya baadhi ya taasisi nyingi zinavyotoa leseni zake kwa muda wa mwaka mmoja. Ili kwa muda huo wa mwaka mmoja utaweza kum-*control* mtu yule, ikiwa kenda kinyume na taratibu za masharti ya leseni ile. Ikiwa anakwenda sivyo kwenye mipaka aliyowekewa.Kwa hivyo, inakuwa ni rahisi kumzuia kwa muda ule wa mwaka au urahisi wa kumpa taratibu zote zile za adhabu ili kupata kutekeleza yale majukumu aliyokuwa kapangiwa. Lakini ukimpa muda wa miaka mitano, basi atakuwa anatamba na anadeka. Kwa hivyo, anaweza akafanya lolote na akasema leseni yake yeye inamruhusu kwa muda wa miaka mitano.

Kwa hivyo, kwa pale kwa kweli itakuwa mtu yule anatuparaganyia yale malengo tuliyokuwa tumekusudia. Kwa hivyo, ningeomba hapa paangaliwe zaidi katika utoaji wa leseni kwa taasisi hizi za habari.

Mhe. Spika, hapa baadhi ya Wajumbe wamezungumza mengi tu yakawemo yale ya kuleta vifaa mbali mbali vya kuelimisha wananchi wetu kwa njia ya

habari. Kwa mfano TV, video na vitu vingi vya habari kutoka nje. Suala hili kwanza mimi nalipongeza kwa kuweka uwazi na kuruhusu vifaa hivi kuvileta ili kila mwananchi akavipata.

Mhe. Spika, huko nyuma tunakotoka ilikuwa watu wetu wengi wanakosa habari, ilikuwa vifaa hivi hawavipati kirahisi. Ilikuwa ukenda dukani bei zake zinakuwa kubwa. Lakini leo Alhamdulillah kila pahali vipo, mtu hata wa kijijini anapata vifaa kama TV, redio, video na vifaa mbali mbali tena kwa bei nafuu tu. Kwa hivyo, hili limesaidia kuwaelimisha wananchi wetu kupata habari mbali mbali ambazo zinatangazwa na vyombo vyetu hivi vya habari. Isipokuwa kubwa tu ninalosisitiza kuwepo na uangalizi pale vinapopitia vifaa hivyo ili viwe vya uhakika na visiwe bomu, kama baadhi ya Wajumbe walivyozungumza. Vichunguzwe na vilivyokuwa sahihi vitiwe madukani kwa kuuziwa wananchi wetu.

Vile vile, Mhe. Spika, kama kuna taratibu za kuvihujumu baadhi ya vile vilivyokuwa vimeshakuwa vibaya kwa njia ya kuvizika au kwa njia ya kuvitia moto au kwa njia ya kuvitupa baharini. Kama itakuwa haviharibu mazingira basi ni bora vifanywe hivyo ili ule uletaji wa vifaa kama hivi viuzwe bei ndogo ndogo ili wafaidike wananchi wetu, vile vilivyokuwa na kasoro basi viangamizwe kwa njia hiyo ili kuepusha uharibifu wa mazingira.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu mimi nimeufahamu kwa kina. Kwa hivyo, namshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea hapa tuupitishe na kupangwa kanuni za sheria zake ili utumike na kuleta maslahi kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mswada huu nawaomba na Wajumbe wenzangu basi tuwe kitu kimoja tuupitishe ili upate kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa hapa naunga mkono mswada huu kwa kushirikiana na wananchi wenzangu wa Jimbo la Amani kwa asilimia mia kwa mia, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliwa leo kuwepo hapa jioni hii na kukamilisha majukumu yetu.Pili, naomba nitowe shukurani za dhati tena kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi wake kwangu mimi binafsi na uteuzi wake huu mpya alioufanya kwa Wajumbe hawa tuliokuwa nao hapa leo Barazani.

Pia, nimpongeze sana katika hotuba yake aliyoitoa Pemba siku ya sherehe za kilele cha kuadhimisha miaka 46 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika ukurasa wa 75 aliposema suala la mafuta la Zanzibar tayari yeye na mwenzake

wameshakubaliana, na litaondoshwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano na litabakia kwetu Zanzibar. Naomba nimpongeze sana kwa hatua hiyo kubwa iliyofikia.

Pia, nimpongeze sana Mhe. Mansour Yussuf Himid Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, ambaye tulikuwa naye pamoja na nyinyi nyote ni mashahidi katika jitihada hizo hadi kufikia kilele cha jitihada zake katika sherehe hiyo na katika hotuba ya Mhe. Rais. Ninaamini baada ya sera itafuta sheria nayo sote kwa pamoja tutaiunga mkono.

Mhe. Spika, naomba pia nikushukuru wewe kwa kuliendesha Baraza hili kwa ufanisi mkubwa, busara na hekima. Naomba nimshukuru Mhe. Waziri Kiongozi, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri Kiongozi, ambaye pia ni Waziri wangu wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa muongozo, busara na hekima zake za kutulea hadi kufikia hapa leo mwaka wa nne tunakaribia kuumaliza mwaka wa tano.

Naomba nimshukuru Kaimu Waziri Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kukaimu wizara hii na kupata miongozo yake mbali mbali, pamoja na Wajumbe wako wote, Mhe. Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba vile vile nishukuru michango ya Wajumbe na mimi nitakuwa na mchango wangu, kwanza moja kwa moja nitaingia kwenye sheria zote mbili. Sheria hii ya Kiswahili na sheria mama ambayo imeandikwa kwa Kiingereza kwa marekebisho mbali mbali yaliyotolewa na Wajumbe kadhaa ili sote tuweze kufuatilia kwa pamoja na iwe ndio imesaidia majibu au hoja ambazo zimeulizwa na Wajumbe mbali mbali na kutakiwa kutolewa ufafanuzi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa mwisho kabisa wa sheria ya Kiswahili katika ukurasa wa 165. Hili pia linamgusa Mhe. Moh'd Ali Salim, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na linawagusa na Waheshimiwa mbali mbali waliogusia vifungu hivi. Katika kifungu cha mwisho kabisa kinasema hivi.

Kifungu cha

> "Sehemu ya pili inaeleza marekebisho katika kifungu cha pili cha sheria mama hiyo, kufutwa kwa kifungu cha 4"

Kwa hivyo, Waheshimiwa kifungu cha 4 kizima kimefutwa, ikiwa pamoja na wale ambao wametoa hoja ya kwa nini TV iwe tofauti, kwa nini redio iwe tofauti. Kwa sababu katika sheria mama kifungu cha 4(2) kinasema

Kifungu cha 4(2)

> *"For the purposes of this section the Zanzibar broadcasting services may be constituted in two branches as follows. A branch of Voice of Tanzania Zanzibar we shall be responsible for radio broadcasting and a branch to be known as Television Zanzibar we shall be responsible for television broadcasting"*

Kwa hivyo, kifungu hiki kizima kimefutwa. Sasa hizo sheria nyengine zitakazofuata baadae labda za kufanya shirika, kama tulivyofanya Shirika la Magazeti, ililetwa hapa ile sheria ya Shirika la Magazeti la Zanzibar, sasa Zanzibar leo limekuwa chini ya Shirika la Magazeti Zanzibar. Kwa hivyo, itakapokuja sheria hiyo na vyombo hivi navyo vitaingia kwenye mwavuli huo huo, nadhani hapo nimefahamika.

Lakini paragraph ya mwisho inaendelea kusema kwamba marekebisho mengine yaliyofanyika ni ya kifungu cha 6, 7, 10, 12, 14 na 15 ya sheria mama.

Mhe. Spika, tatizo liliopo ni Sheria Mama ilipochelewa kufika hapa Barazani, nadhani tatizo limetokezea pale na Waheshimiwa Wajumbe watakubaliana na mimi, kwamba kuchelewa kwa sheria hii ndio imetubabaisha kidogo. Lakini natumai kwa maelezo haya sasa nitakuwa nimejibu mengi ya maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, nikiendelea na majumuisho kama nilivyoelezo hapo awali, ile sheria mama kifungu cha 6 sehemu ya kwanza kifungu (c) na Waheshimiwa Wajumbe pia waligusia kifungu hicho, kwamba *not less than four not more than eight*. Lakini na kifungu hicho nacho kimefutwa na sasa kuna kifungu kipya ambacho kinamdhibiti Mhe. Waziri asichague zaidi ya Wajumbe wanne, hii pamoja na kutokana na gharama pia za kuendesha tume kama hizi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ataruhusiwa kuchagua mmoja, wawili, watatu mpaka wanne, kati ya hao wanne wawili wameelezwa maelezo yake kuhusu taaluma zao pamoja na mambo mengine. Kwa mfano mmoja anatakiwa atokee katika chombo cha habari au taasisi binafsi, hiyo pia imewekwa wazi Mhe. Spika.

Vile vile, nikiendelea kwenye sheria moja kwa moja kuna kifungu cha 10 1 (b) ukusara wa 163. Mhe. Spika, naomba hapa ieleweke kwamba kampuni iliyosajiliwa Zanzibar na angalau yenye asilimia 51 ya hisa zake zinamilikiwa na Mzanzibari. Mzanzibari hapa alivyoelezwa sio *quantifier* na hii ni *qualifier* kuwa yule mtu ni Mzanzibari.

Kwa hivyo, naomba nikubaliane na hoja za Mhe. Said Ali Mbarouk pamoja na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, kwamba sheria hii inalinda maslahi ya

Mzanzibari hasa ukizingatia Sekta ya Habari. Kwa mfano wenzetu kule Dubai na United Arab Amerates nadhani wengine wengi watakuwa wanafahamu, kule huwezi kufungua biashara yoyote bila ya yule mzalendo wa pale kuwa na hisa zake.

Sasa siku moja nilipopata habari ya kutembelea pale nilikuwa nikiuliza mbona hawa wenyewe ikifika saa 7 au 8 wanakwenda kulala, kwa sababu kule kuna utamaduni wa watu wote kufunga kila kitu saa 8 kwenda kulala na kuamka saa 12 au 1 usiku ndipo maduka mengine yote yanafunguliwa.

Kwa hivyo, nilielezwa au nilipewa jibu kwamba hawa wote wanazo hisa zaidi ya asilimia 50, yaani kuanzia 51 na kuendelea na hiyo ni sheria yao ya serikali yao. Kwa maana hiyo, huwezi kufungua biashara bila ya kuingia mzalendo mwenye hisa hiyo.

Vile vile, hisa hiyo sio kama yule mzalendo anamiliki au ametoa fedha zake kuingiza hapana, hisa hiyo hata yule mwekezaji anakuja na kumpa mzalendo, ili yeye mwekezaji aweze kuwekeza pale. Sasa sheria hii tukiwa nayo sehemu zote hata kwenye sekta ya utalii, basi Mzanzibari ndiye atakayefaidika na uchumi wetu ndio utapata kama chumi za wenzetu zilivyopanda huko katika nchi ambazo zinaendelea hivi sasa. Mwenyezi Mungu akitujaalia hayo mafuta yatakapoanza kutoka basi ndio itakuwa zaidi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nadhani hili nimelieleza kikamilifu kwamba hii inam-*qualify* Mzanzibari na anaweza kuwa Mzanzibari mmoja au Wazanzibari wengi kwa pamoja, lakini kwenye sheria watajulikana kama ni kitu kimoja, yaani Wazanzibari. Kwa maana hiyo, wanaweza kujumuika hata watu 50 na kufungua jumuiya yao na kusema sisi tunataka kuomba leseni ya redio.

Kifungu cha 14 katika Sheria hii ya Kiswahili Nam. 7 Mhe. Mohammed Ali Salim alisema ikiwa baada ya leseni ya kutangaza kutolewa pale palikuwa panatakiwa pawe na koma, muda uliotajwa kwenye leseni hiyo kumalizika kabla ya kutangaza pamoja na masharti yaliyowekwa wakati wa kutolewa leseni hiyo, basi leseni hiyo inaweza kufutwa na Tume ya Utangazaji.

Lakini tayari katika Sheria Mama hiki kifungu kinafutwa hapa na imeandikwa huku. Katika sheria mama hiki kifungu kinakuwa Nam. 6. Maana yake ni kwamba inaweza kutolewa leseni kwa mtu na yule mtu akazuia yale mawimbi, kwa kukaa nayo miaka mitano na wala asifungue kituo cha redio wala televisheni, basi nchi inakuwa inapoteza rasilimali yake pale.

Kwa hivyo, sheria hii ipo kwenye vitu vingi vyengine pamoja na ardhi unapopewa kama hujaiendeleza baada ya miaka fulani, basi waziri anakuwa na

haki ya kuirudisha ile ardhi. Kwa maana hiyo, sheria hii hivyo hivyo inasema kwamba baada ya kipindi fulani kama hujaitumia ile leseni basi wewe unapoteza rasilimali ya wananchi na lazima irudishwe.

Mhe. Spika, katika sheria mama kinakuwa Nam. 6. Naomba nimsomee kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 14 (6) kinasema hivi:-

> *"If after a broacasting license is granted a prescribed period elapses before any broadcast is made under the license, the license shall lapse"*

Kwa hivyo, yale maneno yaliyokosekana kwa kiswahili yapo kwenye Sheria Mama kifungu Nam. 6.

Sasa niende kwenye baadhi ya mambo yaliyotolewa kwa jumla nikianza kwa Mhe. Subeit Khamis Faki. Tunamshukuru Mhe. Mjumbe kwa kushirikiana na sisi katika ufunguzi uliofanyika pale Micheweni ingawa yeye hajatukaribisha maji wala chakula cha mchana, lakini natarajia tukienda kufunga hiyo *antenna* hiyo anayoitaka mpya ambayo ipo kwenye *program* hiyo, basi hapo atatukaribisha rasmi chakula cha mchana *(Makofi).*

Mhe. Spika, naomba nimueleze Mhe. Mjumbe kwamba yeye amepata habari ya pekee, kwa sababu kijiji au jimbo lake ni jimbo la dhahabu kwa kuwa limo kwenye mpango wa *millennium*, yaani kinajulikana kama ni kijiji cha *millennium* ameomba hizi redio jamii zifike sehemu nyengine zote.

Kwa kweli sehemu nyengine sio vijiji vya *millennium*, kwa mfano Jimbo la Mpendae halimo kwenye *millennium*. Kwa hivyo, ni tabu sana kufika kwa redio hizi kote, kwa sababu ni redio ya jamii. Kwa maana hiyo, jamii ya Micheweni ndio iliyokusudiwa, sasa tukianza kupeleka mpaka Chake Chake na Mkoani.

Isipokuwa uwezo wa kufanya hivyo tunao baada ya kuweka *antenna* mpya na mashine yenye nguvu zaidi, ambapo uwezekano wa mashine ile kuongezwa nguvu upo, lakini tutakuwa tunavunja ile mikataba ya kimataifa ambayo tumefunga nayo wale wafadhili wetu. Kwa hivyo, hatuwezi kwenda kote huko.

Mhe. Spika, kwa ufupi Mhe. Mjumbe redio yao ya jamii ya Micheweni kwa mashine ile itakapoongezewa nguvu, basi inaweza kufika mpaka Mombasa Kenya, lakini tutakuwa tunavunja mikataba. Kwa hiyo, tunaomba Mhe. Spika kupitia kwako atukubalie kwamba kuna baadhi ya vifaa vitakapokamilika basi

itaendelea kupatikana katika eneo lile kwa sababu ni redio ya jamii. Kwa kweli nadhani wewe mwenyewe unapenda iongezeke zaidi, lakini ni redio jamii na lazima ibakie pale.

Suala jengine Mhe. Spika katika kituo hicho kuna Technolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT Centre)* inafungwa pale ambayo ni ya kisasa na wala hakuna jimbo lolote katika majimbo ya Unguja na Pemba, ambapo kuna kituo kama hicho cha aina yake. Sasa hiyo ni bahati pekee ambayo imefadhiliwa na *UNESCO* pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sote kwa pamoja tumefadhili na kitakuwepo hapo.Kwa hivyo, hicho kinaweza kutumika sana kituo hicho kwa ile rai aliyoitoa Mhe. Rashid Seif Suleiman ya kutoa vipindi vya elimu, yaani kutoa taaluma ya darasani moja kwa moja kwa watoto wa pale.

Kwa maana hiyo, hivi karibuni tunaweza kuona kwamba matokeo yanayotokea kutoka Micheweni yamepanda kwa kiasi kikubwa sana, wakiweza kutumia redio jamii ile na sio kwa maendeleo ya jamii pamoja na kutoa taaluma kama alivyoeleza Mhe. Rashid Seif Suleiman. Pia, kutoa vipindi tofauti vya masomo ambapo wanafunzi wataweza kufaidika katika redio jamii ile.

Mhe. Spika, kwa kumtaja Mhe. Rashid Seif Suleiman naomba nikubaliane naye kwa changamoto alizozitoa. Kwa sababu ni kweli hizi *Satellite* za Kimataifa zinazo vipindi mbali mbali ambavyo hutoa taaluma pamoja na kufundisha masomo ya skuli, yaani *Chemistry*, *Biology*, *Physics* pamoja na masomo mengine ya sayansi, ambapo wanafunzi hufaidika kuliko wanavyokwenda kwenye *tuition*. Kwa kweli kwenye vipindi hivyo wanafaidika zaidi na tunaomba kupokea changamoto hiyo.

Vile vile, changamoto ya pili aliyotupa ni ya kuipeleka TVZ au televisheni zetu kwenye *Satellite*. Mhe. Spika, suala hilo linakuwa na gharama katika sehemu maalum kwenye hiyo *Satellite*, yaani wanaita *space segment*, unalipia kwa masaa au siku nzima.

Sasa kwa kuwa vipindi vyetu vinakwenda kwa saa chache kwa siku basi inakuwa tabu sana katika malipo kulipia kule, kwa sababu itakuwa hatuutumii ule muda unaotakiwa. Kwa mfano mtu kuwa na *tank* la lita 1,000, lakini gari inayokuja nyumbani kwako ni lita 5,000, lakini wakati anapomaliza kukutilia lita 1,000 na lita 4,000 zimebakia kwenye ile gari na wewe unalipia zote lita 5,000 na kuondoka na gari. Kwa hivyo, nadhani tutakuwa kwenye hasara, basi vyema kusubiri kidogo kwa hili.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Ali Denge Makame kwa pongezi zake alizotupa pamoja na mchango wake. Kwa hivyo, naomba nimthibitishie

kwamba muda huo umeongezwa wa miaka mitano kutokana na gharama za uwekezaji, kwa sababu gharama za uwekezaji katika masuala haya ni kubwa hasa huko tunakoelekea kwenye *Digital*.

Sasa huwezi kumtisha mwekezaji na kumwambia baada ya miaka 5 naweza kufuta *license* yako au nitaifuta kabla ya miaka mitatu ama miwili. Hali hiyo inaweza kuwakimbiza wawekezaji.

Pamoja na hilo kwa wale Waheshimiwa Wajumbe walioiuliza *licenses* za TV, tayari tumeshatoa *licenses* za TV binafsi. *Licenses* mbili hizi tumetoa baada ya Mhe. Ali Juma Shamuhuna kuchaguliwa kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kupitisha zile kanuni za kushughulikia vyombo vya habari binafsi, lakini mpaka hivi sasa nasikitika kusema kwamba TV hizo mbili binafsi kwa hapa Zanzibar hawajaanzisha. Kwa kweli hivi karibuni tunatarajia kuwanyang'anya hizo *licenses* kupitia kifungu hiki cha sheria, kwa sababu ni mwaka wa nne hivi sasa tokea wapewe *licenses* hizo bado hawajaanzisha TV.

Mhe. Spika, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kifungu kile cha kuwazuia wawekezaji kuwekeza kwenye redio na TV pamoja kile hakipo na kimetajwa kwenye sheria kwamba kimefutwa kwenye sheria hii. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui alikitaja kifungu hicho pamoja na Waheshimiwa wengine akiwemo Mhe. Rashid Seif Suleiman walikitaja na kile hakipo.

Kwa hivyo, niwatoe hofu kwamba mwekezaji anaweza kuwekeza katika redio, televisheni, internet pamoja na mengine yote yanayohusiana na hayo haimzuii kama wanavyofanya wenzetu wa *IPP Media* kule Tanzania Bara na kama alivyokuwa akifanya Waziri Mkuu wa Italy Sylvio Berlusconi, yaani yeye anavyo vyombo vyote vya habari vinavyotolewa *license* pamoja na magazeti. Sasa hili halikatazwi Mhe. Spika, kama Mhe. Nassor Ahmed Mazrui anataka kuwekeza katika hilo basi asiwe na hofu.

Kwa hivyo, naomba nilithibitishie Baraza hili kwamba hiyo *license* moja wapo iliyotolewa basi aliyepewa ni mwenye chombo cha habari, yaani huyo mtu tayari anamiliki redio na hii *license* ya TV amepewa mtu huyo na mpaka hivi sasa redio imeshaanzishwa, lakini Televisheni bado hajaanzisha. Kwa hivyo, tunataka kumnyang'anya na mtasikia kwenye vyombo vya habari wakati tutakapomnyang'anya siwezi kumtaja hivi sasa.

Mhe. Spika, kwa kuendelea na majumuisho ya michango mbali mbali iliyotolewa Mhe. Juma Duni Haji aligusia suala la *plus two, five, nine*. Suala hii zaidi linahusiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa sababu wao

ndio wanaosimamia mawasiliano na sisi tunasimamia utangazaji, yaani sisi tuko kwenye upande wa *broadcasting* na wao *communication* pamoja na *telecommunication*.

Lakini kweli hili lipo na liliwahi kufuatiliwa sana na ndugu zetu wa *Zantel*, kwa sababu ile *license* ya *Zantel* Mhe. Ali Juma Shamuhuna wakati ule alikuwa Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mipango, suala hili liliwahi kufuatiliwa sana na yeye alikuwa mmoja wapo wa wafuatiliaji wakuu.

Kwa wakati ule Tanzania Bara kulikuwa na bwana mmoja ndugu Ole Kambaine ambaye alikuwa *Director General of Tanzania Communication, Regulate Authority*. Kwa kweli hii ni haki ya Zanzibar na bado ipo haki hiyo na kuna mapato yanayotakiwa yatokane na haki hiyo, lakini nafikiri ufuatiliaji wa karibu zaidi unatakiwa ufanyike.

Mhe. Spika, kwenye hotuba iliyotolewa hapa ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano alieleza wazi kipato kinachopatikana moja kwa moja kutoka *TCRA*, yaani mchango wao katika Bajeti ya Zanzibar.

Kwa hivyo, hilo lipo isipokuwa tunatakiwa tulifuatilie kwa karibu zaidi, kwa sababu hata sisi kwenye *broadcasting* kuna faida na sisi. Naamini Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wanaendelea kuliangalia hili kwa karibu zaidi kama jukumu lao moja wapo kama Wawakilishi.

Mhe. Spika, kuna mchango pia ambao Mhe. Mohammed Ali Salim aliutoa kuhusu vyombo vya zamani. Kwa bahati nzuri mimi katika vitu nilivyorithi nimerithi televisheni moja ya zamani sana aina ya *Phillips*. Kwa sababu zamani hapa Unguja televisheni ilipoanzishwa mara ya kwanza kabisa Unguja nzima pamoja na Pemba tulikuwa na televisheni za aina mbili moja ni *Phillips* na ya pili *Hitach*.

Kwa bahati ile ya *Phillips buttons* zake za kubonyeza tatu, sehemu ya juu ndio kuna kifaa cha kuzidisha sauti kwa kupeleka mbele au nyuma, kwa upande wa *Hitach* ilikuwa inazo *buttons* za kuzungusha na televisheni hizi. Kwa kweli televisheni hizi zilikuwa Unguja na Pemba nzima pamoja na *Television Showroom* ambapo watu walikuwa wanakwenda kuangalia.

Kwa hivyo, mimi nimerithi televisheni moja kutoka kwa Baba yangu mdogo (Ami) na wengi wanamjua Ami yangu hapa. Kwa bahati nzuri televisheni ile bado ninayo mpaka leo na kwa sababu ni kitu cha kirithi basi nimekiweka

kama kitu cha kuweka hifadhi na inafanyakazi mpaka leo. Isipokuwa lile *box* lake la nyuma lilikuwa la mbao, yaani la *chickboard*, sasa lote lile limeliwa na mchwa *(Kicheko)*.

Lakini hizi televisheni za kisasa zinakuwa na *plastic* nyuma na ukipata zile *flat screen* ndio kabisa zinakuwa na *plastic*. Sasa zile zenye *chickboard* ambazo zinabanduka, maana yake ni *chips* nyingi zilizokusanywa na kubandikwa kwa pamoja. Kwa bahati mbaya zote zimeliwa na mchwa, basi ukiiona ile televisheni kule nyuma inatisha vibaya sana hivi sasa, isipokuwa inafanyakazi. Mhe. Spika, naomba nimuhakikishe Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako kwa jumla, kwamba vitu vikongwe kama hivyo kama ulivyosema televisheni yako ina umri wa miaka 20, nadhani ya kwangu inazidi ya kwako kwa sababu nimerithi *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa kweli vitu hivi vipo na vinafanyakazi, lakini havifanyakazi kwa *band* zote. Kwa mfano hivi sasa televisheni ile ukiiunganisha na *Cable Television* hupati *channels* zote, kwa sababu mwisho wa televisheni zile kama sote tunakumbuka ilikuwa ni *channels* 10.

Sasa *Zanzibar Cable Television* inatoa zaidi ya *channels* 70, 79 na hivi juzi nimesikia 80. Kwa hivyo, televisheni ile nikilipia hivi sasa nikilipia *Zanzibar Cable* shilingi 10,000/- au 15,000/- kila mwezi, basi nitapata hasara ya *channels* nyengine 60.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana tukasema kwamba vyombo hivyo vilivyopitwa na wakati havitoweza kufanyakazi, vinafanyakazi lakini havitoweza kufanyakazi kwa mteja yule kufaidika kutokana na hii teknolojia iliopo hivi sasa. Nafikiri hilo limefahamika.

Vile vile, alizungumzia kwamba kuna udhibiti gani wa kuzuia vyombo vikongwe visiingie. Kwa kweli vyombo vikongwe vinaingia vingi sana na wala sio vikongwe tu pia kuna vyombo vipya ambavyo si madhubuti vinaingia hapa nchini. Kwa mfano Mhe. Spika, simu za Waheshimiwa Wawakilishi wengi za Kichina aina ya *Nokia* lakini za Kichina, tuzungumze ukweli tunanunua hapo Darajani.

Kwa sababu soko la kudhibiti vitu visivyo na ubora wa kiwango bado hatujawanalo, suala hili ni kutokana na hali halisi ya kimaisha. Kwa sababu mtu anamiliki shilingi 20,000/- naye anataka kufanya mawasiliano. Kwa hivyo, anatafuta simu ya shilingi 20,000/-. Kwa mfano anapoambiwa *Nokia* ipo hii Nokia ya shilingi 20,000/- hapo Darajani, lakini hakuna *Nokia* hata moja duniani utakayonunua kwa shilingi 20,000/- haiwezekani *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Spika, suala hili ni kutokana na hali halisi ambayo tunayo wananchi mpaka Waheshimiwa Wajumbe wengine wanazo *Nokia* humu ndani ambazo ni za China. Kwa bahati nzuri mimi ni fundi wa simu nazijua huwa ninaletewa, ndio maana nasema hivyo *(Kicheko/Makofi)*.

Kwa kweli mara nyingi huwa wananiletea wakati ile *Nokia Original* inapokataa kupeleka *file* au *message* kwenye *Nokia* haina ubora wa kiwango.Hali hii wengi watakuwa wameshagundua lakini hawasemi tu, lakini wengi watakuwa wameshagundua kwamba *original* haipeleki hata simu moja kwenye ile ambayo haina ubora wa kiwango, kwa sababu yule mwenye *original* ametengenezea kwa *software* ya *original*.

Kwa hivyo, *software* ya *original* haifanyikazi na ile ambayo haina ubora wa kiwango, lakini wengi hawaelewi hivyo na hili lipo. Sasa udhibiti wake tutaufanya vipi, kwa kweli ni gumu sana Mhe. Spika, kutokana na hali halisi kama nilivyoeleza kuwa watoto wetu wanataka mawasiliano. Kwa sababu ile simu inafanya mawasiliano na wala sio kama haifanyi, isipokuwa ina *limitations* zake pamoja na muda wake wa maisha ile simu, *battery charger* unakuwa ni mdogo sana.

Kwa hivyo, nimetoa mfano wa simu lakini kwenye vifaa vya *broadcasting* ni hivyo hivyo. Kwa mfano kuna redio hapa imeandikwa kama Sanyo, kumbe imeandikwa Sangey, lakini kama Sanyo yale maandishi yake. Mhe. Spika, redio ile ukinunua baada ya muda ule mshare wa kubadilishia *channels* unapinda, sasa unakuwa hujui kama uko *channel* ya juu au chini kutokana na kule kupinda *(Kicheko)*.

Mhe. Spika, nikiendelea na majumuisho kama nilivyosema kwamba udhibiti huo ni mgumu, vile vile unahitaji taaluma pamoja na vifaa ambavyo ni ghali sana kwa ajili ya kuangalia *original* na vina ambavyo havina ubora wa kiwango.

Kwa hivyo, tukiendelea kufanya tunaweza kukosa kodi ya baadhi ya maduka ambayo yanashughulika na vifaa hivi. Isipokuwa jambo la msingi ni kuwasisitiza wale wanunuzi pamoja na watumiaji kujua tofauti zilizomo kwenye vyombo hivi na kutoa taaluma kwa wanunuzi pamoja na watumiaji.

Vile vile, Mhe. Mjumbe aligusia kwamba tusifanywe jaa la wenzetu la kutupa vitu ambavyo tayari vimeshaharibika tena ni vingi. Kwa sababu visiwa vingi ulimwenguni tayari vimeshaweka sheria za jaa, navifahamu visiwa viwili, Singapore na Mauritius.

Kwa mfano, Singapore hakuna kitu chochote ambacho hakina ubora wa kiwango utakachoweza kununua kule hata ukitaka kununua, ndio maana wale wafanyabiashara wanaoshughulika na bidhaa au vitu ambavyo havina ubora wa viwango hawendi Singapore. Kwa upande wa Mauritius vile vile hakuna kuanzia shati, viatu, suruali mpaka vifaa vya *eletronic* hakuna visivyo kuwa na ubora wa kiwango.

Kwa kweli ulinunua kitu katika masoko haya ni *original* pekee, yaani wao waliunda sheria hizi za kudhibiti kwa sababu walikuwa hawana sehemu ya kutupa vile vifaa. Na Mhe. Rashid Seif Suleiman alitoa indhari nzuri sana, kwamba wataalamu wachukue masuala haya tunayozungumza kwa yale yanayowalenga wao kwa ajili ya kuyafanyiakazi. Jambo la pili kwa sehemu zile ambazo hakuna sheria, basi tufanye utaratibu wa kutunga sheria na hili linaweza kuanzia hapa Barazani *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa hayo nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba sheria hii ya kuteketeza bado haipo kwenye vifaa hivi, isipokuwa ipo kwenye vyakula pamoja na dawa ambayo tuliipitisha hapa Barazani. Lakini katika eneo hili sheria hii haipo.

Kwa mfano wenzetu Tanzania Bara wanayo Tume ya Mionzi kwa wale waliowahi kutembelea Waheshimiwa Wabunge. Tume hii ambayo *headquarter* yake ni Arusha ambako wamejenga sehemu maalum ya kutupa vitu.

Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa muda huu kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yanahitaji ufafanuzi na mengine yalitolewa ya kitaaluma zaidi. Kwa hivyo, masuala mbali mbali tayari nimeshayatolea ufafanuzi yakiwemo, sheria hiyo ya Mauritius, Singapore, marekebisho aliyoyataja Mhe. Mohammed Ali Salim pia nimegusia suala la Mhe. Rashid Seif Suleiman alilolitaja la kuharakisha mabadiliko ya sheria katika wizara pamoja na kuwasilisha kama hivi.

Nadhani Mhe. Mjumbe ataona jinsi tunavyojaribu sisi kwa wizara yetu kurekebisha mengi, ambayo yanatuhusu katika masuala hayo pamoja na lile la *Educational Television*, ndio nia ya marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa TVZ wakati alipofungua. Kwa kweli nia yake kuu kabisa ilikuwa ni hiyo na katika *speech* yake ya ufunguzi alieleza kuwa TVZ kwa ajili ya kuelimisha jamii, yaani TV kwa elimu. Kwa hivyo, hilo tutaendelea nalo na tutajitahidi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kuhusu ile Tume ya Mionzi pia Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi aliligusia suala hili na ninamshukuru sana kwa mchango wake wa kitaaluma sana alioutoa na kutaja, kwa sababu

yeye ni mkaazi wa Pemba zaidi siku hizi, alitaja suala la TVZ kuonekana pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine kule Pemba.

Sasa naomba nieleze kule Pemba TVZ inayo *transmitter* nzuri sana tena ya kisasa. Kwa kweli *transmitter* ya TVZ ya Pemba inaweza kufananishwa kwenye gari kama *benz*, lakini kwa bahati mbaya sana imekosa maringi, bila maringi hata ukiwa na benz mpya haiwezi kwenda na kwa nini naeleza hivyo. Kwa sababu wakati tuliponunua ile *transmitter* tulikuwa na kasoro ya *antenna*, kwa hiyo, *antenna* tulikuwa tukitumia ya zamani ambayo haiendani na ile mitambo ya kisasa.

Mhe. Spika, naomba niwahakikishie kuwa hivi sasa *antenna* mpya tayari imeshaagiziwa na inasimamiwa na mwenyewe Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na watendaji wetu wa wizara akiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na iko njiani inaweza kufika wakati wowote *(Makofi)*.

Lakini hii *antenna* mpya iliyoletwa pamoja na hii *transmitter* ya *Rhode and Schwarz*, ambayo mara nyingi naita *benz* kwa kule Pemba hata hapa Unguja hatuna kama ile. Kwa kweli hivi vinahitaji umeme ambao haupandi na kushika, yaani vinahitaji umeme ambao utaingia vizuri kabisa. Ndio maana pamoja na kuagizia *antenna* kuna *automatic voltage regulator* inabidi ifike nayo na ipo pale.

Vile vile, kuna kifaa kama *stabilizer*, ambacho kinafanyakazi ya *Uninterruptible Power Supply Unity (UPS)*. Lakini kwa umeme mzuri utakaotoka Tanga ambao ni umeme safi utakaokuwa haupandi na kushuka, yaani Pemba itakuwa na umeme mzuri kuliko Unguja *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi tusiseme hivyo, kwa sababu sisi tunawachangia wale wanaolipa kule, yaani tuna-*subsidize* umeme wa Pemba. Kwa hivyo, kule kutakuwa na umeme ambao ni mzuri, yaani haupandi na kushuka na mashine hizi za TV hazivumilii umeme unaopanda na kushuka.

Kwa maana hiyo, tunaamini umeme kukamilika, *antenna* kufika pamoja na vifaa vyengine vyote basi Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ataweza kuiona TVZ vizuri sana wakati atakapokuwepo Pemba pamoja na ndugu zetu wote walioko huko. Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako, kwamba watufikishie salamu hizo kwa ndugu zetu walioko huko *(Makofi)*.

Vile vile, aliuliza kuhusu kituo kipya cha TVZ. Kwa kweli naweza kusema tumo kwenye mchakato wa kupitia vifaa mbali mbali, ambavyo vitakuja kwa

ajili ya kukifanya kiwe bora zaidi kituo cha TVZ cha hapa na huko baadaye kuanzisha TV mpya. Suala hili tunaendelea nalo.

Mhe. Spika, nikiendelea na majumuisho ya michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Zakiya Omar Juma aligusia neno *paragraph* kama sijakosea na iandikwe kifungu, lakini kwa bahati mbaya katika sheria hii neno kifungu tumeshatumia kwa ajili ya *closes*. Lakini hii inakusudia ile *paragraph* ile maalum.

Sasa kutokana na utaalamu wa wanasheria wao wametushauri kwamba hatuwezi kutumia neno kifungu, sehemu wala aya kwa sababu hayo ni maneno maalum kwa vifungu maalum. Kwa hivyo, labda wanasheria wa Baraza Mhe. Spika watusaidie kama neno hilo halitokubalika na *paragraph*, basi watusaidie neno jengine, lakini sehemu, kifungu wala aya hatuwezi kutumia katika sheria hii inaweza kuleta mkanganyo.

Mhe. Spika, pia, tumepokea ushauri wake wa *radio activity* yaani mionzi. Hilo ni kweli na ni tatizo kwa wenzetu wengine wanasema yanaleta maradhi ya kensa kama saratani ya matiti na maradhi mengine mbali mbali lakini bado hakuna kitu kinachothibitisha juu ya hayo lakini kwa hapa kwetu tutajitahidi kuliangalia hilo na naamini ikishapitishwa sheria hii ikapata nguvu basi itasimamia hilo ipasavyo.

Mhe. Spika, kwa upande wa pili nakumbuka Mhe. Said Ali Mbarouk alisema sheria hii imechelewa lakini wenzetu wa Bara sheria hii bado hawajaipitisha na imekwenda mara mbili imerudishwa kwa sababu sekta ya habari nayo ilikataa kuchangia, wao bado mfumo wa *analogue* kwenda *digital* hawajapitisha kama sheria. Kwa hivyo, sisi tuko mbele kuliko wenzetu wa Tanzania Bara katika hili.

Mhe. Spika, pia, ilitajwa habari ya posho la uandishi wa habari, wafanyakazi wanaofanya kazi hapa katika kipindi cha Baraza. Hili nimeshawahi kuulizwa katika kipindi cha maswali na majibu na nimeeleza kwamba hili mara nyingi linakuwa ni jukumu la Baraza na wale wanaingia katika vifungu vya Baraza, kama vile wataalamu wengine wanapokuja kufanya kazi zao hapa Barazani wakapewa posho, basi na wale nao wanaingia.

Hili ni posho ambalo sisi kama Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo tumeweza kuwapatia wao, lakini hasa wanaingia Barazani. Mhe. Spika, kule Bungeni leo nilikuwa natizama leo kwamba wao wana kitengo kizima cha habari na wale wanaotoa taarifa zote za Bunge pamoja na wale wapiga camera, wanatoa habari wote hao huwa wanalipwa na Bunge. Mhe. Spika, hili nadhani umelisikia utalichukua katika mazingatio ya Baraza.

Mhe. Spika, pia, kuna mchango ambao umetolewa kuhusiana na sifa za mwenyekiti, lakini tunaamini mara nyingi sana yule anayemchagua mwenyekiti basi huwa na busara na hekima za hali ya juu ndio maana hatukuweka sifa za mwenyekiti. Huko siku za nyuma ilishatokea kwenye sifa za mwenyekiti zikiwekwa basi inakuwa ni Mwenyekiti Mtendaji sio mwenyekiti tena na kazi zake mara nyingi zinakuwa zinaingiliana na Katibu Mtendaji imekuwa ikitokezea migongano kadhaa kwamba mwenyekiti anataka kufanya kazi ile ya Katibu Mtendaji.

Mhe. Spika, tumeona jambo hilo kuliepuka ni kwamba tusimuweke huyu akawa ni *Executive Chairman* awe ni *Chairman* ambaye atachaguliwa na kiongozi wetu mwenye hekima na busara naamini kwamba atamchagua mtu mwenye hekima na busara na sio lazima awe wa fani ile ile, lakini awe na fani ya kuongoza ambapo tunaamini ataweza kuongoza vizuri. Kwa sababu Katibu Mtendaji ndio msimamizi mkuu na ndiye anayetakiwa apangiwe zile sifa.

Kwa hivyo, tukianza kumpangia mwenyekiti sifa zile ndio hapo migongano inapoanza kutokea kila mmoja anasema nani zaidi mimi mwenyekiti nimepangiwa sifa hizi na hizi, na mara nyingi ukimpangia sifa yule mwenyekiti anakuwa mtendaji *automatic* kutokana na sifa zile za *qualification* walizompangia. Kwa hivyo, hilo ndio maana tumeona tuliweke iwe ni mwenyekiti tu.

Mhe. Spika, nikiendelea na michango iliyotolewa kuna suala la *condom* na ulevi, hili limezungumzwa sana na limetajwa sana. Lakini sera yetu ya habari inatoa uhuru kiasi fulani kwa vile vyombo vyenyewe na nitaeleza na nitajaribu kufafanua.

Mhe. Spika, mara nyingi inakuwa ni maadili ya mwenye chombo mwenyewe na nitatoa mifano hai. Tuchukulie mifano ya Hoteli za Kitalii zipo hoteli nyingi za kitalii lakini mimi naijua Hoteli moja ya MAZSONS na TEMBO HOTELI iliyopo hapa Zanzibar. Mhe. Spika, hawa wenyewe wameamua kutokana na maadili yao wasiweke pombe katika hoteli zile, sio kama leseni yao ya biashara inawakataza wala leseni yao ya kitaalii inawakataza lakini wao wenyewe wameamua kwa maadili yao kuweka hivyo. Lakini hoteli nyengine zote nyingi hapa Zanzibar wanauza vilevi.

Mhe. Spika, kwenye *broadcasting* katika sheria ni maadili ya yule mwenyewe mwenye redio kama hiyo mifano niliyoitoa kwa hivyo sisi hatuwezi kumuingia moja kwa moja kwamba usiweke hili na hili, lakini ni maadili yao wenyewe. Mimi nazijua redio kadhaa ambazo zimekataa kutoa matangazo yanayohusiana na sigara, yanayohusiana na vilevi, yanayohusiana na masuala ya *condom.*

Nadhani redio moja au mbili tu ndio wanaotoa matangazo hayo, hata wao wenyewe wahusika wanapokuja huku Zanzibar wanapata tabu kweli kweli kutoa matangazo hayo.

Juzi tulipokuweko Pemba nilikuwa na rafiki yangu mmoja bahati nzuri yeye anavuta sigara, wakati tuko huko alihangaika sana kutafuta sigara mimi sijui na wala yeye hakujua kwamba maduka mengi ya Pemba wanasema sigara ni makruh, wenyewe wale wenye duka kwa maadili yao hawauzi sigara. Mhe. Spika, sitaki kukwambia masafa tuliyokwenda kutafuta sigara Pemba yalikuwa ni makubwa sana na mara ya pili alisema akenda yeye atachukua bomba lake zima kutoka hapa Unguja. Mhe. Spika, hayo ni maadili ya mtu mwenyewe.

Mhe. Spika, mfano mwengine ni kwenye michezo sisi Zanzibar tumeshaamua kwamba kwenye michezo hatutokubali matangazo ya vilevi, hatutokubali matangazo ya sigara, hatutokubali udhamini wowote unaohusiana na vitu hivyo viwili pamoja na *condom* tumeshaamua hivyo, hiyo ni kama sera yetu. Hata katika Uwanja wa Amani kwenye yale mabango ya matangazo wale wanataka kutangaza vitu vyao na wanalipa pesa chungunzima kwa ajili ya kutangaza lakini hatutoi.

Mhe. Spika, hata katika Gazeti letu la Zanzibar Leo hatutoi kwa sababu hayo ni uamuzi wetu wenyewe. Lakini timu yetu ya mafunzo ikenda kucheza Tanzania Bara katika ligi ya Kombe la *Tusker* akavaa *tusker* hiyo ni nje ya mipaka ya Zanzibar na yule aliyekwenda kushindana na imeshawahi kufanyika sio mara moja wala mara mbili wanakwenda kule kwa sababu tukianza kukataa *tusker* wale wa *coca-cola* watasema mbona coca-cola mnakubali lakini tusker mnakataa kwa sababu kule wakenda wanashindana na wanavaa hizo fulani lakini ni nje ya Zanzibar.

Kwa hivyo, hilo Mhe. Spika, nadhani liko wazi hatuwezi kumzuia moja kwa moja, hata ile kamati maudhui haitoweza kumzuia moja kwa moja kwa sababu serikali hiyo ina bodi yake nzima ya kutoa leseni ya vileo na bodi kisheria imepitishwa na Baraza hili la Wawakilishi. Katika hiyo leseni ya vileo naambiwa kwamba yupo mmoja anaingia kwa nafasi yake ya ushehe na mmoja pia anaingia kwa nafasi yake ya upadri. Kutokana na sheria hiyo hiyo kama ipo basi na wao inabidi wafanye kazi zao lakini tunawaomba kwa maadili yao wenyewe kama hiyo mifano niliyoitaja basi wao wataweza kuzuia mambo mengine.

Mhe. Haji Faki Shaali, pia aligusia mila, silka na hilo naona linazingatiwa na katika sheria hii ya Tume ya Utangazaji pia kuna *subcommittee* moja ambayo inashughulikia maudhui yaani inaitwa *content committee*. Hiyo itakuwepo na kanuni zake zinatiwa saini na Mhe. Waziri mwenyewe ili zitumike na

ninaamini waliokuwepo katika kamati hiyo watazingatia yote haya na pia Mhe. Waziri atasaini zile kanuni ambazo zitafanya kazi. Kwa hivyo, naomba nimuondoshee hofu Mhe. Haji Faki Shaali katika hilo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Haji Faki Shaali, alitaja kwamba hivi sasa kompyuta ni kila kitu, kompyuta hiyo ni redio, ni televisheni unaweza kutizama CNN humo humo, pia, ni video unaweza kutizama michezo mbali mbali na kompyuta hiyo hiyo inaweza kufanya mambo yote haya matatu au zaidi mpaka manane kwa wakati mmoja. Kwa hivyo, yote hayo kwa pamoja unaweza kuweka *screen* ndogo ukafanya hayo ni uwezo wa akili yako tu kupokea yote kwa pamoja sidhani kama utakuwepo, lakini kompyuta ina uwezo wa kufanya hivyo.

Katika masuala ya kompyuta hakuna bado udhibiti dunia nzima hata huko Arabuni kwenyewe ambako kuna maadili ya hali ya juu ya kidini tukichukulia Saudia Arabia, Iran ndio inayoongoza duniani wao walizuia kila kitu mwisho wakashindwa wakasema mwisho *internet* marufuku kwenye nchi ya Iran. Kweli internet kama marufuku basi huwezi kupata email yoyote kutoka Iran mpaka baada ya huyu kiongozi mpya Mahmoud Ahmed Dijat kuchaguliwa basi vifaa hivyo vikaanza kuruhusiwa na yeye anapigwa vita kwa kuruhusu baadhi ya mambo hayo.

Lakini kuna faida na hasara zake sasa ni juu yetu sisi kuzipima faida tukazichukua kwa sababu kompyuta hiyo hiyo ukitia kur-ani unaisikiliza vizuri na kompyuta hiyo hiyo ukitia CD ya kur-ani ya aya zinazohusiana na ndoa tu basi aya zote kompyuta hiyo itakusaidia kupata.

Mhe. Spika, Mhe. Haji Faki Shaali, pia aligusia suala la *cut of date* hivi vifaa vinavyokuja vya *second hand*, hili naamini serikali itakaa badae tunapokaribia kipindi hiki wakati tumeshaona vifaa vyote vya *digital* vimefika na vipo huwezi kuweka *cut of date* wewe mwenyewe hujajua vitafika lini hivo vifaa, na sasa hivi tuko kwenye mchakato wa kuzungumza pamoja na vyombo vya habari vya serikali na vyombo binafsi ili kuweza kushughulikia suala hilo.

Mhe. Spika, suala la dampo la vitu vya *second hand* hapa kwetu na kudhibiti kwake tayari nimeshalizungumza, Tume ya Utangazaji kweli ndio inayotoa kibali juu ya vifaa mbali mbali mpaka vilioko madukani vinavyouzwa. Hilo ni jukumu lake mojawapo lakini pia kuna Baraza la Sanaa ambalo linashughulikia masuala hayo pia kuna Bodi ya Sensa ambayo pia inashughulikia kuangalia maudhui, *film* na mambo mengine yanayohusiana na hayo ambayo sheria yake pia imeshapitishwa na Baraza lako tukufu. Pia, ametoa mfano wa mafriji na mafriza yanayowekwa nje pia nalo tumeliona hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh Salmin, pia, aligusia suala la kuhamia mfumo wa *digital* na vituo binafsi vilivyoanzishwa hapa Zanzibar na tayari nimesema kuna leseni mbili za TV ambazo zimetolewa katika vituo binafsi lakini mpaka sasa hivi hawajaanzisha bado na tumo katika mchakato wa kuliangalia hilo. Kwa hivyo, wale wote waliokuwa wanataka na wao kuanzisha vyombo kama hivyo tunawakaribisha Ndugu Ali Mwinyi Kai ndiye Katibu Mtendaji wa hii Tume ya Utangazaji wanaweza kufika afisini kwake wakapata maelezo yoyote ya kuomba leseni.

Mhe. Spika, suala la mwezi mtukufu wa Ramadhani limezungumzwa pia. Naomba nilijuilishe Baraza lako tukufu kwamba kuna kamati maalum iliyoundwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutoa taarifa hii. Leo wakati nalifuatilia suala hili mchana nimejuilishwa kwamba kamati ile kuwa na mwakilishi wa Afisi ya Mufti, inakuwa na mwakilishi wa Kadhi Mkuu, inakuwa na Mkuu wa Polisi, Mkuu wa Jeshi na viongozi wengine mbali mbali ambao wanahusiana na mambo hayo pia kuna msemaji mkuu ndani yake na wao ndio wenye kauli moja kama nchi kuthibitisha zile habari na kutoa.

Kwa hivyo, hizi redio nyengine za mitaani zinazotoa habari hizi sio za uhakika. Kwa hivyo, tuna wajibu wa kuwafundisha wananchi wetu kufuata kile chombo maalum kilichowekwa kwa kutoa habari hizo, sio redio yoyote.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili sisi kwa upande wetu tutajaribu kulifanyia kazi, lakini tunaomba jamii yetu pia ilifanyie kazi kwa sababu kuna kamati maalum ambayo mtu huenda akaapishwa. Nimeelekezwa mambo yote ambayo yanatakiwa yafanyike katika kamati ile na bahati nzuri kamati ile ina mtu wetu mmoja, ina Mkurugenzi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar na yeye ndio kazi yake kutoa matangazo kwa vyombo vyote husika vya habari.

Mhe. Spika, suala la vitendea kazi lilizungumzwa, mambo mbali mbali uwezo ukipatikana hivyo tunaendelea nalo kila siku. Mhe. Spika, leo naomba niseme mbele ya Baraza lako tukufu kwamba zile *camera* mbili mnazoziona pale ni *camera* mpya. Pia, naomba niwajuilishe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba zile *camera* wenzetu kutoka Bara wamekuja kuazima huku kwa ajili ya *broadcasting* ya sherehe za Mapinduzi Pemba hawakuja na vifaa vyao wakati tunarusha pamoja na *TBC* na *camera* moja pale imeshasafiri kwa kuazimwa kwenda mpaka Angola kunakochezwa Kombe la Afrika na imesharudi hivi sasa.

Kwa hivyo, zile ni *camera* za kisasa tena ni *full digital* zinaitwa *high definition television* kama mtapita pale wakati wa kutoka mkiangalia mtakuta kitu kimeandikwa *HDV* maana yake ni *High Definition Television* ndio mtu anapooneshwa kwenye *digital* TV akakatika vipande vipande halafu akaungana

akawa mmoja ndio *camera* zile. Kwa hivyo, Mhe. Spika, *camera* ni zetu lakini ziko kwenye ukumbi wako wa Baraza la Wawakilishi hivi sasa.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk, pia, alielezea kuhusiana na habari ya mitambo michakavu nimeshalielezea hilo, habari ya mionzi, fedha za TCRA aliuliza pia nimeelezea kwamba zile hutajwa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na kasma zao ambazo wanachangia wizara hiyo moja kwa moja.

Mhe. Spika, nadhani kwa kumalizia niseme kwamba sheria yetu ya *importation* ya Zanzibar imeweka asilimia 20 zaidi kwa vyombo vikongwe nayo hiyo ni katika kudhibiti vile vyombo vichakavu kuingia. Lakini kwa sababu huko nje wenzetu vitu hivi vingi vinapokuja hapa vinakuwa vimetupwa na wanatafuta pahala pa kuvipeleka. Kwa hivyo, hata ukiwaekea asilimia 20 zaidi kulipa hapa bado vyombo vile vinakuwa rahisi zaidi. Kwa hivyo, ni ngumu sana tayari serikali imeshafanya hilo na nimethibitishiwa leo kwamba asilimia 20 kwa vyombo vichakavu pamoja na magari makongwe ipo asilimia 20 zaidi. Lakini mnaona nyinyi wenyewe magari machakavu mangapi tunayo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nadhani nimeyapitia yote isipokuwa vifaa vipya nataka kuongezea tu hapa vifaa vipya vya televisheni hili tunatumia fungu letu lile la *MDRA* kuvileta kwa hapa Zanzibar, suala la Wachina kuanzisha idhaa yao. Ni kwamba Wachina tunashirikiana nao pamoja katika vifaa na wao tutakuwa tunachukua matangazo kutoka kwao. Kwa hivyo, ile idhaa inakuwa ni ya SMZ sio idhaa ya Wachina, wao tunashirikiana nao, tunafunga vyombo vyao, tunachukua *broadcasting* yao lakini chini ya leseni ya SMZ.

Kwa hivyo, hiyo itakuwa sio idhaa ya Wachina bali ni idhaa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na itaweza kutumika wakati wowote kwa shughuli nyengine za serikali ukiacha na hiyo *broadcasting* ya kuchukua CCTV kutoka China. Kwa hivyo, Wachina hapa hawapewi leseni wala lolote yote hayo yako chini ya serikali moja kwa moja.

Mhe. Spika, zimetangazwa zile redio za kidini nadhani hili liliguswa na Waziri Kivuli na Wajumbe wengine. Mhe. Spika, redio za kidini hizi tukizipa uwezo moja kwa moja basi naomba nilihakikishie Baraza lako redio nyengine zote nazo zitasema ni za kidini. Hilo la kwanza lilitokezea.

Mhe. Spika, la pili kama mtachunguza redio za kidini ndio zenye maadili makubwa zaidi kuliko redio nyengine zozote hapa nchini kwetu, hawatangazi masuala hayo tuliyoyataja ya *condom*, hawatangazi masuala ya vilevi hawachukui hata haya matangazo ya ovyo ovyo lakini wao matangazo wanayotoa kama utachunguza ni matangazo ya vifo na watu wanalipia matangazo ya vifo. Kwa hiyo, kila watu wakifa zaidi na wao hupata kipato

zaidi. Pia, wanatoa matangazo ya vyakula kama mtaangalia redio Adhana, Nour na redio nyenginezo wao wanatoa pia matangazo ya vyakula na mara nyingi wale wenye redio wenyewe ni wafanyabiashara. Hizo ni kama sadaka zao wanazielekeza kule katika kuelimisha jamii.

Kwa hivyo, mara nyingi unakuta analeta chakula na huyo ndiye mwenyewe anatoa faida yake na kuendeshea redio hiyo. Kama mtachunguza matangazo ya vyakula mengi yanayotolewa kwenye redio hizo ni vyakula vya wale wenye redio. Hili suala la redio Adhana lilikuja kwetu kwamba mwenyewe anataka kufunga na kadhalika, lakini Mhe. Waziri Kivuli nikuthibitishie mimi mwenyewe binafsi nilimfuata nikamwambia kama unataka kuuza kuna mtu tayari mwenye imani ya kiroho mwengine ambaye anataka kununua redio hiyo.

Je, uko tayari akasema hapana, siko tayari nitahangaika nayo mpaka nitafika kunakotakiwa. Kwa hivyo, alikataa baadae lakini kweli kulikuwa na lengo hilo. Kwa hivyo, ninachotaka kusema Mwenyezi Mungu wale amewajaalia biashara yao ni halali. Mhe. Spika, hilo haitowezekana sisi kutoa uamuzi moja kwa moja, lakini wanapoleta maombi maalum yakafika wizarani wanaweza wakaangalia kwani hilo lipo sote ni binadamu na sote bahati nzuri tuna roho na imani pia. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hilo linawezekana na wala halina matatizo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa naomba tena nitoe shukurani za dhati naona nimejaribu kuingia maeneo yote ambayo yametajwa. Kwa hivyo, na mimi naomba niunge mkono kwa yale ambayo labda sikuyagusa naamini Mhe. Waziri yupo atakuja kuyakamilisha na pale nilipokosea najua ataniongoza na kuniweka sawa. Kwa hayo, naomba niunge mkono hoja kwa niaba ya wananchi wote walionichagua kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, na mimi naomba kidogo nimalizie pale alipobakishia Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa namna alivyoweza kuchambua masuala yote ambayo waliyouliza Waheshimiwa, lakini pamoja na kuchambua masuala hayo alitoa taaluma zaidi ambayo kila mmoja alikuwa na hamu aendelee kutoa huu uchanganuzi. Kwa hivyo, tunamshukuru sana kwa hilo na kila nilipokuwa nikijaribu kuyaangalia yale niliyokuwa nimeyadondoa mimi naona yote alikuwa ameshayaramba yeye mwenyewe.

Kwa hivyo, mimi nitaamua nichukue nafasi kwanza kuwapongeza wale wote ambao wamechangia nikianzia na:

1.	Mhe.Ali Suleiman Ali	Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii.
2.	Mhe. Najma Khalfan Juma	Waziri Kivuli.
3.	Mhe. Haji Faki Shaali	
4.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	
5.	Mhe. Said Ali Mbarouk	
6.	Mhe. Zakiya Omar Juma	
7.	Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	
8.	Mhe. Juma Duni Haji	
9.	Mhe. Ali Abdalla Ali	
10.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	
11.	Mhe. Haji Mkema Haji	
12.	Mhe. Subeit Khamis Faki	
13.	Mhe. Ali Denge Makame	

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kwanza tunazipokea pongezi za Mhe. Subeit kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Mapambo Mhe. Waziri Kiongozi kwa kweli anakushukuru sana kwa niaba ya wizara yetu na serikali kwa jumla tunakushukuru sana.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu pamoja na marekebisho yale yaliyoelezwa na kamati wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Baraza

lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kupitisha mswada kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji ya Zanzibar ya Mwaka 2010

Sehemu Ya Kwanza

UTANGULIZI

Kifungu cha 1	Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 2	Kusomwa.

Sehemu Ya Pili

MAREKEBISHO YA VIFUNGU

Kifungu cha 3	Marekebisho ya kifungu Nam. 2 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 4	Kufutwa kwa kifungu Nam. 4.
Kifungu cha 5	Marekebisho ya kifungu cha 6 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 6	kuongezwa kwa vifungu vya 6A na 6B pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 7	Marekebisho ya Kifungu cha 7 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 8	Marekebisho ya Kifungu cha 9 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 9	Marekebisho ya kifungu cha 10.

Kifungu cha 10	Marekebisho ya kifungu cha 12.
Kifungu cha 11	Marekebisho ya kifungu cha 14.
Kifungu cha 12	Marekebisho ya kifungu cha 15.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia mswada huu nilitoa wasi wasi wangu kuhusiana na redio ambazo zinapewa leseni na halafu hutangaza mambo kinyume na maadili ya Wazanzibari. Na nikanukuu kifungu cha 15(c) ambacho chenyewe hasa ndicho kinachoelekeza umuhimu wa matangazo yajali mila na desturi ya Wazanzibari. Lakini bahati mbaya katika marekebisho ya kifungu hicho mpaka (m) kinafutwa kikiwemo hicho kifungu ambacho kinasisitiza utangazwaji kwa mujibu wa mila ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu majibu yake kwa kweli hayakunitosheleza, kwamba masuala haya hili ni jukumu binafsi la vyombo vya habari. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ikiwa kweli chombo hiki ambacho kazi yake zaidi ni ku-*regulate* mambo ya utengenezaji tukaachia masuala haya iwe ni jukumu la binafsi la chombo cha habari binafsi na akajaribu kutoa mfano kama hoteli za kitalii, nchi hii kwa kweli tunaipeleka pabaya.

Mimi nadhani kifungu hiki cha 15(3)(c) kingebaki ili kiipe nguvu hii tume iweze kudhibiti masuala haya. Hatuwezi hata kidogodogo Mhe. Mwenyekiti, kuacha masuala haya ndani ya mikono tu ya wafanyabiashara, wafanyabiashara wao kazi yao ni *maximize profit* wataipelekea nchi pahala pabaya. Kwa hivyo, bado sijaridhika na maelezo ambayo Mhe. Waziri amenipa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako tunakubaliana na hoja ya Mhe. Said Ali Mbarouk, lakini tunamhakikishia kwamba asiwe na wasi wasi. Kwa sababu baada ya kupitisha sheria hii vile vile Mhe. Waziri ana suala la kutengeneza kanuni. Kwa hivyo, haya yaliyotolewa hapa basi yata-*appear* kwenye kanuni katika ku-*regulate* hiyo namna ya kuweza ku-*handle* masuala ya utangazaji. Kwa hivyo, hili Mhe. Said Ali pamoja na kwamba kifungu 15(3)(c) ambacho kinaelezea namna ya kulinda maadili ya Wazanzibari basi kita-*appear* katika kanuni itakuwa halina wasi wasi suala hilo.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi, Mhe. Kaimu Waziri na Waziri mwenyewe na Naibu wake, Katibu Mkuu wake na Naibu wake, ni watu

ambao ninawaheshimu sana. Lakini suala hili Mhe. Mwenyekiti, lingehitaji nguvu zaidi ya kisheria kuliko sheria ndogo (kanuni), likipewa nguvu ya kisheria zaidi katika Baraza kanuni haipiti hapa Barazani, ikishapita kwa waziri huko basi inamaliza huko huko, lakini tungetaka tujiridhishe sisi kama Wajumbe wa Baraza hili kuona kwamba *values* ambazo nchi yetu inabidi kuzilinda kwa kweli tuna *guarantee* nazo. Hilo ni jambo ambalo bado nalisisitiza.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yako tunasema Wallahi na sisi Mhe. Said Ali Mbarouk tunamheshimu sana. Kwa hivyo, kwa heshima ile ile anayotuheshimu sisi basi tunakubaliana hiki kifungu (c) tu, tunakirejesha hapa ili kuweza kuipa nguvu hii sheria. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pia namshukuru Mhe. Kaimu Waziri tuendelee.

Kifungu cha 12 Marekebisho ya kifungu cha 15.

Mhe. Spika: Hii tumemaliza tena Mheshimiwa, marekebisho haya yanafuatana na yale maneno aliyosema kwamba sasa kifungu kile ***simu*** ile itatengenezewa kifungu ili kulinda hayo maadili ya wazanzibari.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima imeupitia mswada wangu vifungu kwa vifungu na kukubaliana na mabadiliko yote pamoja na masahihisho, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho mbali mbali wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar ya Mwaka 2010

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar No.7 ya Mwaka 1997 sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na Mhe. Waziri katika kusomwa mara ya pili kwa mswada huu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa tuliyoanza kuonesha kwenye mkutano huu wa 18 kwa Baraza letu hili saba. Nadhani tumeanza mwenendo mzuri kabisa, naridhika sana na mashirikiano makubwa tuliyoonesha na heshima kubwa tuliyopeana kama tulivyosikia. Wajumbe wakiheshimu mawaziri na mawaziri wakaheshimu sana Wajumbe wake. Sasa hili ni jambo la kupongezwa na Mwenyezi Mungu atujaalie tuendelee kwa utaratibu huu huu.

(Saa 1:40 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 21/01/2010 saa 3:00 asubuhi)